Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

_____

MAJADILIANO YA BUNGE

_____

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Pili – Tarehe 30 Januari, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 15

Kumalizia Jengo la Zahanati ya Milola - Lindi

MHE. RIZIKI S. LULIDA aliuliza:-

Jengo la Zahanati ya Milola limejengwa nusu na kuachwa zaidi ya miaka mitatu (3) bila kukamilishwa huku wananchi wakihangaika kutafuta sehemu ya kupatia matibabu:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha jengo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Zanahati ya Milola iliyopo Kijiji cha Milola katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi inaendelea kutoa huduma za afya kwa wananchi kwa Kijiji hicho na maeneo mengine ya jirani kwa saa 24. Ujenzi ambao umesimama uhahusisha jengo la huduma ya Mama na Mtoto *(RCH)* ambao umefikia kwenye '*lenter'* tangu mwaka 2010. Mradi huu unasimamiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, kupitia Uhisani wa Mfuko wa *Clinton Foundation*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii chini ya Uhisani huo wa *Clinton Foundation* upo katika hatua za kukamilisha ujenzi wa Zahanati hiyo ya Milola. Pamoja na juhudi hizo, Halmashauri katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 imetenga kiasi cha shilingi 12,000,000/= kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto *(RCH)* kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI inaamini Mfuko wa *Clinton Foundation* ukitoa fedha za kukamilisha jengo hili, fedha za Halmashauri zitatumika kununulia vifaa tiba na samani katika zahanati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI itafuatilia fedha hizo kwa karibu na kuhakikisha kuwa ujenzi wa zahanati hiyo unakamilika kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri na ninafikiri atafuatilia hilo suala la kujenga hiyo zahanati. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu kuwa Mkoa wa Lindi sasa hivi unakabiliwa na tatizo kubwa la wafanyakazi, wafanyakazi wengi ambao inabidi wakafanye kazi katika zahanati, wengi hawapo na baadhi ya zahanati nyingi zimefungwa?

Kwa mfano, zahanati ya Madangwa imefungwa, zahanati ya Zingwa Minguruwe imefungwa na kuna baadhi ya zahanati nyingi ambazo zimefungwa kwa ajili hakuna manesi au madaktari ambao wanakwenda katika zahanati hizo?

La pili, mimi ni mjumbe katika Kamati ya LAAC, lakini katika fedha za miradi ambazo zinakwenda katika Halmashauri nyingi zimeelekezwa na wafadhili kama ni fedha za posho, semina na sasa hivi posho zimeishakuwa nyingi na matokeo yake zahanati nyingi zimebaki hazina madawa, hazina vitendea kazi.

Je, Naibu Waziri anasema nini ili kuboresha mazingira haya?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukubaliana kwamba ni kweli kwamba zahanati nyingi na Vituo vya Afya vingi kama tulivyoeleza jana hapa ni kweli havina watumishi ambao Mheshimiwa Mbunge amesema. Hiyo ni kweli na tulieleza hapa kwamba wapo watu wengine ambao wanapangwa katika maeneo yale, lakini hawaripoti na hawaendi kule. Hilo ni moja.

Lakini ukicheki ile ikama, ikama hapa maana yake ni *establishment* ndani yake unakuta pia kwamba Mkoa wakati mwingine unagawiwa watumishi wanakwenda pale lakini *concentration* inakuwa ni maeneo ya Mjini. Nitakwenda kukaa na Mheshimiwa Lulida ili niweze kuona hili tatizo likoje na tuone kuna vibali vimetolewa na vibali vimekwenda kule lakini ukitafuta watumishi ambao wana sifa hizi za kwenda kule pia ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, sasa hili la pili, kuhusu posho, semina na kwamba hakuna dawa na vitu vingine. Kwanza, maelekezo ukichukua hizi fedha anazozisema za *Local Government Capital Development Grant* huruhusiwi kwenda kulipa posho na nitataka kujua kutoka kwake kama ni hizi fedha alizozisema hapa kwa maana ya miradi haziwezi kwa sababu makubaliano ni kwamba fedha hizi zitumike kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwa maana ya *project.* Sasa nitataka kujua hilo.

Lakini la pili, kwamba tunafanya nini ili kuondokana na tatizo hili. Jana tumesema hapa huu Mfuko unaitwa *CHF* na *NHF* ambao tumeanzisha katika Halmashauri zetu ni Mfuko ambao utatuondolea sana tatizo hili ambalo Mheshimiwa Lulida amelizungumzia na kama tulivyokubaliana hapa tutakaa naye nisikie ili niweze kujua undani wa jambo hili, halafu niweze kushughulika na tatizo hili. *(Makofi)*

Na. 16

Kupunguza Kero ya Maji katika Mji wa Magu

MHE. MANSOOR S. HIRAN (K.n.y. MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU) aliuliza:-

Serikali ilishaahidi kutoa fedha kwa ajili ya kupunguza kero sugu ya maji katika Mji wa Magu:-

Je, utekelezaji wa ahadi hii imefikia hatua gani?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Jimbo la Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo la maji katika Mji wa Magu, Serikali imepanga kutekeleza mradi katika awamu mbili. Awamu ya kwanza inahusisha kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina pamoja na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kutoa maji kutoka Ziwa Victoria na kuyafikisha katika Mji wa Magu. Zabuni ya kupata orodha ya wataalam Washauri watakaoshindanishwa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo imetangazwa tarehe 4 Julai, 2012 na taarifa ya tathmini imepelekwa Benki ya Dunia mwezi Oktoba, 2012 kwa ajili ya kupata kibali. Utekelezaji wa Awamu ya kwanza ya mradi utagharamiwa na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP).*

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili itahusisha uboreshaji wa huduma ya Majisafi na Majitaka katika Jiji la Mwanza, kujenga miundombinu ya Majitaka katika Miji ya Bukoba na Musoma; na ujenzi wa miundombinu ya maji katika Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi.

Serikali kwa kushirikiana na Mashirika ya Wahisani ya *European Investment Bank* (EIB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AFD)* wametenga fedha kiasi cha *Euro* milioni 14.2 kwa ajili ya Miji mitatu ya Magu, Misungwi na Lamadi na *Euro* milioni 90.8 kwa ajili ya Mwanza, Bukoba na Musoma. Utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi utaanza mara baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya mipango ya uboreshaji wa maji katika Mji wa Magu kukamilika, upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Magu utakuwa wa uhakika na wananchi watakuwa wameondokana na kero sugu ya maji inayowakabili hivi sasa.

MHE. MANSOOR S. HIRAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji ilituahidi wananchi wa Wilaya ya Kwimba kwamba baada ya mradi wa maji ukishafika Magu watauendeleza huo mradi mpaka ufike Mgudu Mjini. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anipe majibu kwamba mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kufika Magu utafika lini na wamejipanga namna gani kutuletea bomba la maji kutoka Magu mpaka Wilaya Kwimba katika Mjini mdogo wa Ngudu?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali iliahidi kupeleka maji katika Mji wa Ngudu na katika jibu langu la msingi nilipoelezea kwamba unafanyika upembuzi yakinifu

na usanifu wa Mji wa Magu, usanifu huu unahusisha pia kupeleka maji Ngudu na katika usanifu huu tutapata chanzo kimoja ambacho kitajengwa kwa ajili ya kupeleka maji Magu na kwa ajili ya kupeleka maji katika Mji wa Ngudu na wananchi ambao watapitiwa na bomba hilo likitoka kwenye chanzo cha maji Ziwa Victoria kwenda Magu na kwenda Ngudu nao pia watapata maji.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Silinde, sasa Magu na Mbozi ndiyo tatizo linaanzia hapo.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa kero ya maji kwenye hili Taifa limekuwa ni kubwa sana, kabla ya uhuru na hata baada ya uhuru.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ni chini ya asilimia 30 ya Watanzania wanaopata maji safi na salama. Nilitaka nifahamu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri ni nini mkakati mbadala katika kipindi cha miaka hii iliyopo sasa hivi, kipindi kifupi kwa maana mpaka mwaka 2015 kufikia asilimia 50 ya Watanzania wote kupata maji safi na salama? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Serikali ili kuhakikisha kwamba inawapatia wananchi wake maji. Kwanza, imetunga Sera ya mwaka 2002 na baada ya kutunga Sera imeweka programu ya Maji ambayo ilianza kutekelezwa mwaka 2007.

Katika programu hiyo na Sera hiyo tumejiwekea mipango ya miaka mitano mitano ambayo inasema kwambwa kufikia 2015 maji vijijini tuwe tumefikisha asilimia 65, na sasa hivi siyo kweli kwamba ni asilimia 30. Sasa hivi tupo kwenye asilimia 57.8, na tumesema kwamba katika mkakati huo pia kufikia mwaka 2025 basi vijijini tuwe tumefikisha asilimia 90. Kwa hiyo, kinachofanyika sasa hivi ni utekelezaji wa hiyo programu na tumeishaanza kutekeleza na tuna hakika kwamba tutafikia hayo malengo ambayo tumejiwekea. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Godbless Lema kwa kurudi tena ndani ya Ukumbi huu wa Bunge. Tunamtakia ufanisi mwema wa kazi yake. Hongera sana Mheshimiwa Lema kwa kurudi tena. (*Makofi*)

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema, atauliza swali linalofuata.

Na. 17

Kupima Malori yaliyo Matupu

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA aliuliza:-

Kuna mizani ya magari makubwa katika Kijiji cha Kilototoni, Jimbo la Vunjo – Moshi Vijijini ambayo hulazimisha magari yote yenye tani zaidi ya 3.5 kupima hata kama gari halina mzigo; lakini mizani hiyo huharibika mara kwa mara na kuleta usumbufu na foleni ndefu kijijini hapo kwa abiria wa mabasi na malori:-

(a) Je, kwa nini mizani hiyo hupima malori yaliyo matupu na kusababisha kero na foleni kubwa wakati mizani nyingine hazipimi malori yasiyo na mzigo?

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kuhamisha mizani hiyo iliyo katikati ya Kijiji cha Kilototoni ili kuondoa usumbufu?

(c) Je, Serikali ya kijiji inapata mapato kiasi gani kutokana na mzani huo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika kijiji cha Kilototoni Jimbo la Vunjo – Moshi Vijijini kuna kituo cha mizani kilichopo njia panda ya Himo. Kituo hiki kama vingine kinasimamiwa na Wakala wa Barabara – *TANROADS* na kinapima magari yote yakiwa na mzigo au matupu yenye tani 3.5 na kuendelea kama kanuni Na. 7(1) ya Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30 ya 1973 inavyotamka. Lengo ni kuhakikisha vituo havitoi mwanya kwa magari kupita bila kupimwa kwa kisingizio chochote.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuuhamisha mzani wa Himo. Mpango wa Serikali ni kujenga mzani upande wa pili wa barabara ilil magari yanayotoka njia ya Dar es Salaam yasivuke barabara kufuata mzani. Hii itasaidia kupunguza msongamano wa magari katika mzani wa sasa katika kituo hicho cha Himo.

(c) Mheshimiwa Spika, fedha zote zinazokusanywa kwenye vituo vya mizani nchini huwasilishwa kwenye Mfuko wa Bodi ya Barabara (*Road Fund Board*) ili hatimaye zitumike kwenye matengenezo/ukarabati wa barabara kuu za Mikoa na Wilaya na hivyo kufidia uharibifu wa barabara.

Hii ni pamoja na barabara za Jimbo la Vunjo. Ni vyema ieleweke wazi kuwa nia ya kuweka mizani ni kuzuia uharibifu wa barabara na siyo kukusanya fedha au kufanya biashara ambayo pengine vijiji husika vingefaidika moja kwa moja.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri ile mizani pale njiapanda ya Himo wale wananchi wa kijiji cha kilototoni wanaichukulia kama kitega uchumi chao kikubwa na kinaingiza mapato mengi.

Wale watu wa Kilototoni ambao sasa ni kama wapo Mjini, kuna athari ya mazingira inayojitokeza kunapokuwa na msururu wa magari, moshi mwingi wanavuta, ajali zinatokea pale, barabara ni nyembamba na watoto wao wanakufa na kadhalika.

Sasa mimi nilichouliza wale wenyeji wa Kilototoni wale wananchi wa pale watafaidika vipi moja kwa moja na kile kitega uchumi ili na wao waweze kupata manufaa. Kwa mfano, wana Zahanati pale mngeweza kusema wakipata ule moshi watasaidiwa namna gani au waweze kwenda mahali pengine pa kupata matibabu.

Sasa ukisema tu kwamba zile fedha zinatengeneza barabara na zile athari za mazingira, moshi wa magari na ajali zinazotokea pale. Serikali inawafikiria vipi kama inavyotaka kuwafikiria wananchi wa Mtwara na gesi yao.

Je, wananchi wa Kilototoni na mizani yao watanufaika vipi?

SPIKA: Mimi naona gesi hapo imeingizwa tu. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema hatuna namna ya kuwapa wananchi wale moja kwa moja.

Kwa mfano, labda waone faida ya mzani, lakini faida ya mzani ni kwa Taifa ni kwa sababu ya uharibifu ambao utatokea kwenye barabara na Taifa zima linapata shida na ndiyo maana tumeona kwamba zile fedha kidogo zinazopatikana kwa wale ambao wanavunja sheria tunazitumia katika kuwatengenezea barabara. Sasa hiyo ni faida ambayo wanaipata *indirectly.* Kwa hiyo, si kweli kwamba hawapati faida. Kwa hiyo, faida wanaipata.

Kwa hiyo, mizani hii hasa sana sana ni kwa ajili ya kuzuia uharibifu wa barabara ndiyo maana tumeweka mizani karibu nchi nzima.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kuna malalamiko ya wasafarishaji kwamba wanapopima magari yao katika mizani mengine yanakuwa na uzito mzuri, lakini yanapopimwa katika mzani wa Himo uzito unaongezeka na kwa sababu hiyo wafanyakazi wa pale wanatuhumiwa sana kwa matatizo ya rushwa.

Je, Serikali inalifahamu hili na ipo tayari kufanya uchunguzi wa hii mizani?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na malalamiko kwamba mwenye gari anaweza akapima kwenye kituo kimoja gari ikawa imeweza kukidhi kiwango kinachotakiwa, akaenda kituo cha pili ikaonekana kwamba amezidi uzito.

Kinachotokea ni kwamba magari mengi unakuta kwamba mzigo ule unaweza kuhama na kinachopimwa pale ni *axel* siyo ule mzigo ile *gross weight* ni ile *axel***.** Sasa mzigo ukihama lazima kutakuwa na tofauti ya vipimio na sheria imezingatia hilo kama unaweza kumwambia mwenye gari auhamishe aupange vizuri na ukapima tena ili aweze kuendelea na safari yake.

Suala la pili, kuhusu rushwa ni kweli kwenye mizani kumekuwa na rushwa na wafanyabiashara sana sana ndiyo wanaosababisha kwa nini umpe rushwa yule anayepima wakati unajua kipimio kimeshaonyesha na faini inajulikana na wewe kwa nini umpe fedha. Kwa hiyo, kosa lipo pande zote mbili kwa wafanyabiashara na wafanyakazi.

Sasa hivi Wizara yangu inashughulikia suala la *modernizing* hii mizani kwamba akifika mahali akishapima unaona kabisa inakwambia ni fedha kiasi gani unatakiwa kulipa.

Kwa hiyo, hakuna kitu cha ku-*discuss,* na vile vile tunataka tufanye pale kwenye mizani watakuwa hawapokei fedha taslim ili kuondoa kishawishi cha rushwa, hayo masuala yote tunayashughulikia.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika barabara nyingi nchini kumekuwa na misururu mikubwa na mirefu sana ya magari kutokana na ucheleweshaji katika mizani.

Katika maeneo mengine magari hulazimika kusubiri kwa masaa kadhaa ili kusubiri muda wao wa kupimwa Serikali inalitambua hili na kama inalitambua ina mkakati gani wa makusudi na wa haraka kuwezesha *fast process* katika utaratibu huu wa mizani pengine kwa kuongeza idadi ya mizani katika eneo lile ili kuwaondolea wasafirishaji wakubwa adha kubwa ya kusafirisha katika nchi yetu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tunatambua kweli kuna maeneo ambapo huwa inatokea msululu mkubwa wa magari na maeneo mengine unakuta mzani uko upande mmoja.

Sasa tunachokifanya sasa hivi ni kujenga mzani na upande wa pili ili kuondoa ule msongamano. Mara nyingine msongamano unaweza ukatoka pengine mzani ule umeharibika. Kwa hiyo, suala hili tunalitambua na ndiyo maana tunataka tu-*modernise* tu-*replace* hii mizani ya zamani tuwezeke mizani ya kisasa ambayo itaweza kuondoa tatizo la msongamano.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, kwa naiba yake atauliza Mheshimiwa Abdallah Njwayo.

Na. 18

Barabara ya Kidahwe - Nyakanazi

MHE. ABDALLAH J. NJWAYO (K.n.y. MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE) aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Kidahwe – Nyakanazi itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kidahwe – Nyakanazi yenye urefu wa kilometa 310 utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kimetengwa kwa ajili ya kufanya matayarisho ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Aidha, barabara hii ipo katika orodha ya miradi iliyopewa kipaumbele katika miradi iliyoainishwa katika mpango wa maendeleo wa barabara za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Nchi Wanachama inatafuta fedha za ujenzi kutoka kwa wafadhili mbalimbali.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya kutia matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza ili kuharakisha sekta ya usafirishaji na kuongeza uchumi wa nchi yetu hivi ni kwanini Wizara ya Miundombinu isiweke mkakati maalum wa kuhakikisha barabara zilizopo pembezoni mwa nchi yetu na ambazo zimekuwa zikisaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza uchumi wa nchi yetu barabara kama vile za Kigoma, Rukwa, Mtwara na mahali pengine zisipewe kipaumbele maalum na kuhakikisha zinajengwa na kumalizika mara moja yaani *timeframe* na hivyo kuboresha uchumi wa nchi yetu?

Kwa sababu barabara hii ya Kidahwe Nyakanazi kiuchumi inafanana sana na ile barabara ya Mtwara – Tandahimba –Newala hadi Masasi ambapo kwenye Bajeti iliyopita ilitengewa kiasi cha pesa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu lakini hadi sasa upembuzi huo haujaanza. Naibu Waziri anaweza kuliambia Bunge hili ni lini sasa upembuzi yakinifu huo utaanza na lini lami itawekwa kwenye barabara hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa barabara zile ambazo zinaongeza uchumi wa nchi tumeziweka katika kipaumbele cha Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Kwa hiyo, hilo suala limeshazingatiwa.

Pili kuhusu barabara ya Mtwara – Tandahimba – Masasi kwenye Bajeti tumeweka fedha za kuanza kufanya usanifu barabara ile kwa kujenga kwa kiwango cha lami. Sasa utaratibu wa kawaida ni kwamba tunatengeneza mpango kazi tunapeleka Tume ya Mipango, Tume ya Mipango ikishaidhinisha fedha basi ndiyo tunaanza kazi maana ndiyo utaratibu ambao upo katika Sheria ya Manunuzi. Kwa hiyo, suala hilo linazingatiwa kwa kufuata taratibu hizo.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nilitaka kuuliza swali dogo tu. Kwenye Bajeti ya mwaka jana zilitengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mayamaya Kondoa hadi Babati. Barabara hiyo mpaka sasa hakuna kinachoendelea lakini pili hata hii ambayo inajengwa kutoka Dodoma mpaka Mayamaya ujenzi wake unasuasua ningeomba kujua Serikali inawaambia nini wananchi wa Dodoma, Kondoa na Babati?

SPIKA: Mheshimiwa Juma Nkamia huyu alikuwa anauliza barabara ya Nyakanazi sasa tena Kondoa swali jingine kabisa. Lakini kwa sababu Naibu Waziri una mtandao wa barabara uko kichwani basi naomba ujibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba niliarifu Bunge hili kwamba barabara ya kutoka Mayamaya Kondoa mpaka Babati *tender* zimeshatangazwa. Kwa hiyo, hilo ni hatua nzuri na mwezi wa pili *tender* zinarudishwa tunapata mkandarasi na baada ya hapo kazi itaanza na fedha zipo. *African Development Bank* na JICA wameshatoa fedha. Kwa hiyo barabara hii itajengwa. Wananchi wa Kondoa waanze kufurahi kwamba barabara hii itajengwa.

Kuhusu barabara hii kutoka Dodoma mpaka Mayamaya kasi imeshabadilika na sasa hivi inakwenda vizuri baada ya muda si mrefu wataanza kuweka lami. Kwa hiyo na suala hilo tunalifuatilia tuhakikishe kwamba barabara hii itaisha kwa muda uliopangwa. *(Makofi)*

Na. 19

Mradi wa REA Makambako

MHE. DEO K. SANGA aliuliza:-

Mji wa Makambako umebahatika kuwa na mradi wa Umeme Vijiji *(REA)* lakini mpaka sasa haujaanza kutekelezwa:-

(a) Je, mradi huo utaanza lini ili uweze kuwasaidia wananchi?

(b) Je, mradi huo utakapoanza utakamilika lini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kaseyenda Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi unaotekelezwa chini ya ufadhili wa *REA* Makambako ni kufikisha umeme katika mitaa ya Kitisi, Majengo, Kilimahewa na Kivavi. Mradi huu umechelewa kuanza na ulitarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, mwaka jana na hii imetokana na kuchelewa kupata vifaa vya ujenzi ikiwa ni pamoja na waya, vikombe na bolti. Aidha tumekubaliana na Mkandarasi kumaliza mradi huu kabla ya mwezi mei mwaka huu 2013.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri napenda niulize swali la nyongeza. Naibu Waziri alipotembelea Mji wa Makambako alijionea mwenyewe hali halisi ya tatizo kubwa ambalo linaukumba mji ule na aliwaahidi wananchi wangu kwamba ifikapo mwezi wa nne suala hili litakuwa limekwisha. Je, anawaambia nini wananchi wa Makambako kwamba kama alivyoahidi alipokuja Makambaku suala hili litakuwa limetekelezwa tayari lini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, ni kweli nilitembelea Makambako na nashukuru wananchi wale walinipokea vizuri na kwa kweli uhitaji wao wa umeme kwa mazingira yalivyo ni pale pale Makambako. Lakini mitaa mingine ina umeme na mitaa mingine haina umeme haileti furaha kwa wananchi wale. Niliwaahidi na napenda niwahakikishie wananchi wale na Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi hii ya Serikali itatekelezwa kwa wakati ambao tulikubaliana yaani kabla ya mwezi wa tano miradi hii itakuwa imekamilika.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, kwa sababu tatizo la huduma ya umeme vijijini vilevile ni tatizo kubwa Wilayani Mbarali hasa ukizingatia kwamba tuna Kata 20 lakini ni kata nne tu ambazo zimepitiwa na umeme na niliomba kwamba Wilaya ya Mbarali nayo iingizwe katika mpango wa huduma ya umeme vijijini. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini wananchi wa Mbarali wataingizwa kwenye mpango huo?

SPIKA: Swali jipya kabisa ila kwa sababu mtandao wenyewe uko kwenye digitali basi naomba ujibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali tumedhamiria kabisa kwa dhati na kwa sasa dhamira yetu ni kuhakikisha Wilaya zote mpya zinapata umeme na Waheshimiwa Wabunge tulikubaliana na mlipitia orodha ya maeneo yenu yatakayowekwa umeme. Tumejitahidi sana na sasa hivi yapo katika hatua ya utangazaji wa *tender* na tunaamini wakati wowote kuanzia mwaka huu miradi hiyo itaanza kutekelezwa. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote akiwemo Mheshimiwa Kilufi kwamba Mbarali imo katika taratibu zinazoendelea sasa za mchakato wa *tender* ili tuweze kutekeleza mradi huo.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua kuna mradi wa *REA* kutoka njia nne hadi Kipatimu, Mheshimiwa Waziri mwenyewe alifika katika eneo hilo na aliahidi utekelezaji wake ungeanza mwezi wa Januari. Mpaka hii leo hakuna jambo lolote ambalo limefanyika na Januari inakwisha kesho. Je, anatoa kauli gani?

SPIKA: Sasa nitaanza kukataa maswali yanayoingizwa tu bila utaratibu. Kwa sababu hii *REA* ya Kilwa inatoka wapi? Mheshimiwa Naibu Waziri jibu na ni swali la mwisho.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, ni kweli nilitembelea Kilwa na nikaweza kuona na niliahidi na ninataka kukuhakikishia kwamba pamoja na wakandarasi wetu kuwa wanachelewa na hii inatokana na miradi mingi

sana inayotekelezwa kwa pamoja na sehemu zinazopatikana vifaa wakati mwingine ni sehemu hiyo hiyo moja.

Kwa hiyo, wakati mwingine unakuta kuna foleni katika upataji wa vifaa ikiwemo nguzo na vifaa vingine. Kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge kwamba pamoja na kuwa tunaahidi miradi itaanza kutekelezwa wakati fulani lakini hawa wanaotekeleza wanahitaji vifaa kutoka kwenye sehemu moja na hivyo ucheleweshaji unatokana na hasa zaidi na sababu hiyo. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi ule wa Kilwa lakini nadhani wakati wowote kuanzia sasa utekelezaji wake utaanza.

(Swali Na. 20 liliondolewa na Mwuliza swali)

MHE. MURTZA ALLY MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia utamaduni na busara ya kibunge naomba swali namba 20 liondolewe mpaka pale Kamati ambayo umeiundwa na Ripoti ya Waziri Mkuu itakayokuja.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali kwa Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub atauliza swali hilo kwa niaba yake Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

Na. 21

Uchakavu wa Vituo na Nyumba za Polisi Zanzibar

MHE. YAHYA KASSIM ISSA (K.n.y. MHE. JAKU HASHIM AYOUB) aliuliza:-

(a) Je, ni sababu gani zilizosababisha vituo vya Polisi Bumbwini, Dunga, Mitini na Chwaka kukabiliana na uchakavu mkubwa na kupoteza sifa ya kuwa ni vituo vya Polisi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvifanyia matengenezo vituo hivyo ili kuondoa kero kwa askari na wananchi wanaotumia vituo hivyo?

(c) Je, Serikali ilitenga kiasi gani cha fedha katika mwaka wa fedha 2010/2011 kwa ajili ya kufanyia matengenezo majengo ya Polisi na nyumba za Askari Makao Makuu ya Jeshi Zanzibar.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vituo alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge na vingine vinahitaji kufanyiwa ukarabati kwani ni muda mrefu sasa tangu vimejengwa jambo ambalo linapunguza ufanisi wa huduma.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunaendelea na ukarabati wa kituo cha Polisi Chwaka na tayari tathmini ya vituo vya Dunga na Bumbwini imeishafanyika. Vituo hivyo vitakarabatiwa mara tu fedha zitakapopatikana.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Serikali ilitenga jumla ya shilingi 600,000,000/- kati ya hizo shilingi 400,000,000/- ni kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Polisi Mkokotoni, shilingi 200,000,000/- ni kwa ajili ya ukarabati wa jengo la ofisi zilizopo Makao Makuu, Zanzibar. Aidha katika mwaka wa fedha 2010/2011 hazikutengwa fedha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za askari.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kituo cha Chwaka katika ujenzi wake haukuwa dhamira hasa ni ujenzi wa kituo; na kwa kuwa kituo hicho hivi sasa kiko katikati ya kijiji hakuna siri yoyote ambayo inaweza kuzungumzwa isitoke nje.

Je, huoni kwamba ilikuwa ni vizuri kuweza kujenga kituo kipya na wakati maeneo yapo?

La pili, kwa kuwa kituo cha Dunga kimepasuka na kuna hatari hata hao askari kuangukiwa na kituo hicho. Je, Serikali haioni ni vizuri kuweza kujenga kituo kipya ili kuweza kuwanusuru askari hao katika kituo hicho?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Yahya Kassim Issa kwa kujua undani wa vituo hivi ambavyo viko kwenye Jimbo lake.

Pili kwenye suala la kituo cha Chwaka ni kweli kwamba kituo hiki ni nyumba ambayo ilirithiwa na pengine haina *design* ambayo ni nzuri kwa kuwa kituo cha polisi. Kwa sababu Mheshimiwa amejitokeza basi namwomba tushirikiane naye ili tupate eneo na tuwahamasishe wananchi.

Sisi tuko tayari tujenge kipya ambacho kitakuwa na hadhi ya karne hii. Hivyo hivyo kwa upande wa Dunga ni kweli kwamba tulitaka tufanye kituo hiki lakini kama kuna mawazo na ushirikiano wa Mbunge na wananchi wake basi nacho tutakijenga upya kwa vile ambavyo vitakuwa vinaruhusu kufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa. *(Makofi)*

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninas wali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kituo chetu cha Mkokotoni kilipata ajali ya kuungua moto na nashukuru Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho; na kwa kuwa tangu Bajeti ilipopitishwa sasa hivi ni zaidi ya miezi sita. Namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze ni hatua gani ya maendeleo ya Kituo cha Mkokotoni hadi hivi sasa imefikiwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kituo cha Mkokotoni kiliungua na katika harakati za kurudisha huduma za Kipolisi pale tulitenga pesa kwa ajili ya kukijenga upya.

Naomba nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi umeanza na uko katika hatua ya *linter.* Tunategemea kwamba fedha nyingine ambazo bado hazijatoka zikitoka tutapiga hatua na lengo ni kukifanya kituo kimalizike kwa wakati uliopangwa.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri napenda kumwuliza kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa shughuli nyingine zinahitaji fedha nyingi. Lakini hivi Wizara yako inayo habari kuwa Kituo cha Madema pale Unguja kina tatizo sugu sana la maji ambapo hata wale Mahabusu wanaoingizwa pale wanashindwa kupata maji ya kunywa?

Je, hata hili linahitaji kuchukua muda mrefu bila kutengenezwa?

Mheshimiwa Spika, ni kweli ninafahamu kwamba, kuna tatizo la maji kwenye Kituo cha Makao Makuu ya Polisi. Ninaomba nitoe taarifa kwamba, tulikuwa tunatafuta ufumbuzi wa suala hili, nimepata taarifa za kufurahisha kwamba, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni, ana Mradi wa Maji ambao anataka kuugawa katika maeneo yake. Kituo hicho kipo kwenye Jimbo hilo, tunaendeleza mazungumzo tuone sisi tunaweza kuchangia kiasi gani ili tuweze kufanya kazi hiyo kwa pamoja. Ninampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Kikwajuni, kwa kukubaliana na sisi kwamba, tuanze mazungumzo ya suala hili.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Kazi na Ajira, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, atauliza swali hilo.

Na. 22

Wafanyakazi wa Hotelini

MHE. RASHID ALI ABDALLAH aliuliza:-

Ibara ya 23(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasisitiza mwajiriwa kupata malipo kulingana na kiasi na sifa za kazi anazofanya kwa kuzingatia Sheria na Mikataba ya Kazi na Katiba ya Nchi; lakini wako Wafanyakazi wengi wa Hotelini wanafanya kazi kuanzia saa moja asubuhi hadi saa tatu usiku kwa malipo kidogo sana:-

(a) Je, Serikali inalifahamu jambo hili; na inachukua hatua gani?

(b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa Ibara ya 23(i) ya Katiba inatekelezwa ipasavyo?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Serikali inafahamu kuwa, baadhi ya Waajiri wanakiuka Sheria za Kazi. Kwa kuzingatia ukweli huo, Kaguzi za Kazi zinafanywa mara kwa mara katika maeneo ya kazi kwa lengo la kubaini upungufu na kuchukua hatua stahiki. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa Wafanyakazi na Waajiri kuhusu haki na wajibu wao kwa mujibu wa Sheria za Kazi, pia kuwafikisha Mahakamani Waajiri wasiorekebisha mienendo yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, Waajiri wanaamriwa kuwalipa Wafanyakazi malipo ya kazi zilizofanyika nje ya muda wa kawaida wa kazi au katika siku za sikukuu au mapumziko mwishoni mwa juma. Vilevile vipo Vyombo vya Kisheria vinavyoshughulikia stahili zitokanazo na kazi; vyombo hivyo ni pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi na Mahakama ya Kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ni kwa kila Mfanyakazi kujua wajibu wa haki zake. Pale ambapo anaona anatendewa visivyo, basi achukue hatua, ama yeye mwenyewe ama kwa kushirikisha Chama cha Wafanyakazi kwa kuvitaarifu vyombo husika; mfano, Idara ya Kazi au hata kufungua shauri katika Tume ya Usuluhushi na Uamuzi ili tatizo linalomkabili lipatiwe ufumbuzi

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya mambo yaliyoifanya Tanganyika kudai Uhuru wake ni kuondoa unyonyaji na utumwa. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, bado tatizo hili linaonekana kuwa kubwa, Wafanyakazi wanafanya kazi kubwa kwa malipo madogo:-

(i) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kulieleza Bunge hili ni hatua gani ya makusudi anaweza kuchukua ya kuweza kuondoa tatizo hili la unyonyaji?

(ii) Kwa kuwa tatizo hili lipo katika hoteli mbalimbali; je, Wizara imepata mikataba yoyote ya Wafanyakazi hawa na kujiridhisha ili kuona wanalipwa malipo sahihi?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ambalo Wafanyakazi na Waajiri wazingatie ni kujielimisha kuhusu Sheria za Kazi. Kama kila mtu atajielimisha kuhusu Sheria za Kazi, ambazo kwa bahati nzuri Wizara yetu imezitafsiri hata kwa Lugha ya Kiswahili, kila mtu atajua haki zake na matatizo kama haya yakijitokeza itakuwa ni rahisi kwa Mfanyakazi kufikisha shauri lake kwenye mamlaka inayohusika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sisi tunaendelea na kaguzi kama nilivyosema; nitoe mfano kwa mwaka jana Wizara yetu ilifanya kaguzi elfu mbili mia nne na moja nchi nzima, kuangalia kama Taratibu za Kazi na Sheria za Kazi zinafuatwa na Waajiri mbalimbali. Pale ambapo Waajiri wamekuwa sugu tumewapeleka Mahakamani na kuna waajiri 14 ambao tumewapeleka Mahakamani na mmoja ametozwa shilingi 500,000. Hizi ni baadhi ya hatua ambazo sisi kama Serikali tunachukua, lakini elimu ni ya msingi sana.

Mheshimiwa Spika, sisi hatuungi mkono hata kidogo suala la unyonyaji katika kazi na ndiyo maana tumetunga Sheria ya Kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikataba, ni kweli kabisa kuwa, mikataba inatofautiana kati ya Mwajiri na Mwajiri; jambo la msingi, ukijua Sheria za Kazi, utaelewa kabisa mkataba wako ule unataka upewe nini na ndiyo maana tumeweka kuna Vyama vya Wafanyakazi na kuna Mikataba ya Hiari ambayo inatakiwa Mwajiri aifuate kama alivyokubaliana na kusainiana na Mfanyakazi husika. Pale anaposhindwa, aje *CMA* tuweze kushughulikia matataizo hayo.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, kumekuwa na unyanyasaji mkubwa sana hasa kwa hawa Wafanyakazi wa Hoteli kwa Wawekezaji pindi Wafanyakazi hawa wanapodai haki zao hutishiwa kufukuzwa kazi na wengine kumwagiwa maji ya moto. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri una mikakati gani ya kuwadhibiti hawa wawekezaji ili Watanzania hawa wa kipato cha chini wanaofanya kazi za chini wanapodai haki zao wazipate kwa wakati mwafaka?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nitumie Bunge lako hili, kuwaonya Waajiri wote ambao wananyanyasa Wafanyakazi, waache mara moja, kwa sababu wamekuja nchini kwetu kuwekeza kuinua Uchumi wetu, lakini kutupa ajira yenye staha kwa Wafanyakazi wetu. Kuwanyanyasa ni kinyume cha Sheria. Vilevile nitoe wito kama nilivyosema, kila mmoja azingatie Sheria za Kazi.

Mheshimiwa Spika, mfanyakazi ajue haki zake na pale anapoonewa achukue hatua za kufikisha suala mahali husika, sisi tutaendelea na kaguzi na pale ambapo tunakuta unayanyasaji unaendelea tutaendelea kuchukua hatua za kisheria kama nilivyoeleza pale mwanzoni**.**

Na. 23

Uwanja wa Ndege Singida Kutengenezwa
***Running Way* kwa Kiwango cha Lami**

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Uwanja wa Ndege wa Mjini Singida ulishapanuliwa na kukarabatiwa na kuweza kuruhusu ndege ndogo kutua ila kikwazo katika Uwanja huo ni kutokuwa na *running way* ya kiwango cha lami:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kutenga fedha katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012 ili kutengeneza *running way* kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo kuwa, kuna haja ya kuboresha Kiwanja cha Ndege cha Singida na vingine, kwa kuimarisha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami. Mikakati ya Serikali ni kuimarisha miundombinu ya Viwanja vya Ndege vyote ya Mikoa kwa kujenga barabara za kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Taifa na Uchukuzi ya Mwaka 2003 *(National Transport Policy).*

Mheshimiwa Spika, kiwango cha kuboresha miundombinu ya Kiwanja cha Ndege cha Singida kwa kiwango cha lami umewekwa pia kwenye Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Uchukuzi *(Transport Sector Investment Program).* Kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, itaanza utekelezaji wa mpango huo kwa kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa lengo la kukarabati na kuboresha Kiwanja hiki kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ya Uchukuzi imepanga kuboresha viwanja vya ndege 20 kwa kiwango cha lami. Utekelezaji wa Mpango huu, utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya Kwanza ya Mpango huu itahusu Viwanja vya Ndege kumi ambavyo ni Iringa, Kilwa Masoko, *Lake Manyara,* Moshi, Musoma, Mtwara, Njombe, Songea, Singida na Tanga.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi bilioni 3.2 kwa ajili viwanja kumi vilivyotajwa hapo juu kikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Singida, tayari zimepatikana kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Baada ya hatua hii, kazi ya ukarabati kwa kiwango cha lami zitafanyika kwa viwanja vyote kumi.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Singida kimeshaimarishwa na Serikali kwa urefu wa kilomita moja kwa kiwango cha changarawe na ndege zenye abiria mpaka 20 zinaweza zikatua hata wakati wa masika. Je, Serikali haiwezi kuimarisha kwa kiwango hicho hicho cha changarawe angalau mita 600 ili Kiwanja hicho kiwe na urefu wa kilomita 1.6 ili hata ndege za abiria 50 ziweze kutua?

(ii) Kwa kuwa Wananchi hawapendi sana kusikia neno upembuzi yakinifu, usanifu au mchakato; je, Serikali haiwezi kuwatajia Wananchi wa Mikoa hii iliyoainishwa kwamba ujenzi wa viwanja vyenu kwa kiwango cha lami utaanza mwaka fulani kwani upembuzi umeanza kutamkwa muda mrefu hata Mheshimiwa Rais alipokuwepo Singida aliwaambia hivyo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, hatua ambayo hivi sasa inachukuliwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege baada ya kupatikana hii fedha ni kufanya huo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa hiyo, kama hatua ya uimarishaji wa hicho Kiwanja, tutazingatia maoni ya Mheshimiwa Chilolo kuwa, tuimarishe kwanza kwa kiwango cha changarawe wakati tunatafuta fedha na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, maneno niliyoyataja, bahati mbaya ni hatua za lazima za kupitia katika ukamilishaji wa Miradi yoyote; ni kweli kabisa kuwa yanachosha kusikika lakini kwa sababu ni lazima yatajwe. Ninapata tabu kuyakwepa wakati ndiyo hali halisi tuliyonayo kwa sasa kwamba, tuko kwenye hiyo hatua na hatuwezi kutaja hatua nyingine; lakini kama itampendeza, baada ya upembuzi yakinifu sasa tutasema ukarabati au ujenzi utaanza lini.

SPIKA: Huwezi kubadilisha tu kwa sababu ya kubadili! Nilimwona Mheshimiwa Mbatia, lakini Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwanza.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, ninapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika viwanja kumi vya ndege alivyovizungumza, ambavyo vinafanyiwa upembuzi yakinifu na Serikali ni pamoja na Uwanja wa Ndege wa Moshi. Uwanja huu umekuwepo kwa zaidi ya miaka 50 na umejengwa kabla ya Uhuru; na kwa muda mrefu sana hasa baada ya kufungua Uwanja wa Kimataifa wa *KIA,* Uwanja huu umekuwa *idle* na umekuwa hauna matumizi yoyote ya kiuchumi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri una taarifa kuwa kwa zaidi ya miaka miwili sasa Wizara yako imeombwa kwa muda mrefu kuachia Uwanja huu uweze kugeuzwa kuwa Chuo cha Marubani?

Serikali kwa muda wote huu imekaa kimya bila kujibu maombi haya na kama ni hivyo inakuwaje sasa uingizwe katika mpango wa kufanyiwa upembuzi yakinifu wakati maombi ya kuugeuza Uwanja huu kuwa Chuo hayajafanyiwa kazi mpaka leo wala hakuna majibu ya msingi yaliyotolewa na Serikali?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri ya Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la Uwanja wa Ndege wa Moshi kutokuwa na matumizi siyo kwa sababu ya Uwanja wa Kimataifa wa *KIA* ambao uko pale karibu isipokuwa ni *size* ya Uwanja, lakini kikubwa zaidi ni uchakavu wa ile barabara ya kutua na kuruka ndege. Laiti ile barabara ya kutua na kuruka ndege ingekuwa nzuri, Uwanja wa Ndege wa Moshi ungeendelea kupata matumizi. Kwa sasa ndege chache bado zinatumia Uwanja huo kwa shida. Ndege zote za *JET* haziendi Uwanjani pale hata kama ni ndogo kwa sababu ya kuogopa zile kokoto ndogondogo kuweza kuharibu ndege.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maombi ya Kampuni ya *Precision Air* kutumia Uwanja ule kama Chuo cha Marubani, Wizara ilikwishawakaribisha *Precision Air* waje kwa mazungumzo,

lakini wao wenyewe ndiyo hawakutokea baada ya kuambiwa kuwa tuko tayari kuwa-*offer* huo Uwanja kwa ajili ya matumizi yao ya Chuo cha Marubani.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kasi ya mawasiliano hasa ya sayansi na teknolojia inakua kwa kasi kubwa na sekta zingine za mawasiliano kama barabara na nyingine nazo zinakua kwa kasi, viwanja alivyovitaja Mheshimiwa Naibu Waziri vipatavyo 20 kasi yake ya kukua au ujenzi wake hauendani na kasi ya kukua kwa uchumi:-

Je, Serikali haioni ni bora viwanja vyote hivi vikajengwa kwa utaratibu wa *Public Private Partinership (PPP)* ili kasi iende kwa haraka na ikiwezekana wakubaliane na makusanyo yanayopatikana yaende kwenye Mradi wa Ujenzi wa Viwanja hivi ikiwemo *Terminal Three* ya *Julius Nyerere International Airport*?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kasi ya matengenezo ya hivi Viwanja ni kweli kabisa haiendi kama mahitaji ya kiuchumi yalivyo, ndiyo maana sasa hivi tumeingia katika huu mpango mkubwa ambapo tunatarajia viwanja kumi vya awali vyote vitafanyiwa matengenezo kwa kiwango cha lami kwa pamoja. Viwanja hivi vipo katika hali mbaya na uchakavu mbalimbali, kwa mfano, Kiwanja cha Moshi hakipo katika hali ya uchakavu kama Kiwanja cha Mtwara na kadhalika; kwa hiyo, mahitaji ya fedha huenda hayatakuwa makubwa sana kama tulivyodhani awali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwahusisha watu binafsi katika matengenezo ya viwanja hivi, Wizara na Serikali kwa ujumla, inakaribisha wawekezaji wenye nia ya kufanya hivyo. Kiwanja cha Ndege cha Mji wa Mugumu huko Wilayani Serengeti, kitafanyiwa matengenezo kwa utaratibu huu huu wa *PPP.* Kwa hiyo, kama yupo mwekezaji, nitumie nafasi hii kuwakaribisha waje kwa ajili ya mazungumzo kuhusu utaratibu huu.

Na. 24

Ujenzi wa Jengo la Shirika la Reli Mpanda

MHE SAID AMOUR ARFI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Jengo la Shirika la Reli lenye hadhi katika Stesheni ya Reli Mpanda?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Serikali ina dhamira ya kuboresha miundombinu yote ya Shirika la Reli yakiwemo majengo ya stesheni zote nchini kama sehemu ya Mpango wa Maendeleo ya Muda Mfupi, wa Kati na Mrefu wa *TRL.* Mpango huu utatekelezwa kwa awamu kadiri fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, kama hatua za awali, Serikali imeelekeza nguvu zake katika kufufua usafiri wa treni kwa kukarabati vichwa vya treni na mabehewa ya abiria na mizigo, kuimarisha tuta la reli na kuondoa reli zote nyepesi na kuu kuu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wananchi kwa ujumla kuwa, mpango wa kujenga majengo yenye hadhi katika stesheni zetu za

reli utafanywa kwa awamu hasa baada ya kuhakikisha huduma za usafiri wa treni na miundombinu yake imeimarika kiasi cha kuweza kutoa huduma siku zote za wiki.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yasiyoleta matumaini hata kidogo, namshukuru Naibu Waziri lakini naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Naibu Waziri umetembelea Stesheni ya Mpanda wewe mwenyewe nikupongeze sana. Stesheni ya Mpanda inahudumia wasafiri watokao Sumbawanga na maeneo mengine na kwa utaratibu wa sasa wa kuuza tiketi za safari siku ya safari imeleta adha na usumbufu mkubwa kwa wasafiri hasa kwa kuwa Stesheni ya Mpanda haina kibanda cha kusubiria wasafiri *(Waiting Room),* pamoja na vyoo hasa kipindi hiki cha mvua. Pamoja na matatizo yote, Serikali sasa ipo tayari kuliagiza Shirika la Reli kukarabati *waiting room* iliyokuwepo pale na kutengeneza vyoo ili kuondoa adha kwa wasafiri wanaotumia Stesheni ya Mpanda?

(ii) Pamoja na mipango mizuri ni lini sasa Watanzania wanaotumia usafiri wa reli wategemee kwamba safari za garimoshi zitakuwa za kila siku; lini zinaanza? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kushauriwa na Kamati ya Bunge, iliagiza Shirika la Reli Tanzania kutafuta utaratibu mwafaka ambao utazuia watu wasio waaminifu kutumia uhaba wa nafasi katika treni zetu kulangua tiketi. Kwa hiyo, utaratibu wa kukata tiketi siku ya safari kwa kutumia vitambulisho ndiyo uliioonekana njia ya muda mfupi inayoweza kupunguza tatizo hili la ulanguzi wa tiketi. Ni hatua ambayo kwa upande mmoja imeondoa kweli suala hili la ulanguzi wa tiketi, lakini kwa namna fulani imesababisha adha kwa wasafiri ambao wanatoka sehemu ambazo tiketi hazikatiwi huko.

Mheshimiwa Spika, hili ndiyo tatizo lililopo katika Stesheni za Kigoma, Mpanda na maeneo mengine ya njiani.

Mheshimiwa Spika, lakini usafiri wa reli utakapoimarika, tuna hakika kwamba, tatizo hili litakwisha lenyewe kwa sababu nafasi katika treni zitakuwa za kutosha kwa wote wenye nia ya kusafiri na treni.

Kwa sasa nauchukua ushauri wa Mheshimiwa Arfi kwamba, tukarabati hivyo vibanda lakini ni pamoja na stesheni zingine zote kwa sababu adha wanayopata wasafiri wa Mpanda ndiyo wanaopata wasafiri wa vituo vingine vya reli kama nilivyosema hapo awali.

Kwa hiyo, jitihada sasa zinawekwa kwenye kuimarisha usafiri wenyewe na hatua itakayofuata itakuwa ya kukarabati hivyo viwanja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lini usafiri wa treni utakuwa *regular* kwa maana ya kila siku, hatua ambazo zimechukuliwa sasa hivi na Serikali kama zote zitatekelezwa kama inavyotarajiwa kwa maana ya kununua mabehewa 22 ya abiria, kununua vichwa vya treni vipya na kukarabati vingine kwa fedha iliyotolewa katika bajeti ya mwaka huu, tutarajie kwamba, mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwaka kesho, treni za kwenda Bara kote; Mwanza, Kigoma na Mpanda, zinaweza kuwepo kila siku.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika ahsante. Kwa kuwa Stesheni ya Reli ya Kigoma ni jengo la kihistoria na sasa hivi linavuja na hali hii ikiendelea jengo lile linaweza kudondoka. Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka ili kuweza kunusuru hali hii?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli Stesheni ya Kigoma jengo ni la kihistoria na ambalo tumedhamiria kuliweka katika hadhi yake linavuja. Katika ziara yangu kwenye Stesheni hiyo mwishoni mwa mwaka jana, nilitoa maelekezo kwamba, *TRL* watafute fedha haraka waweze kulifanyia angalau ukarabati wa kuzuia huo uharibifu unaoendelea sasa hivi.

Na. 25

Kuhalalisha Eneo la Hifadhi na Kupimwa Viwanja

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Wananchi wamejenga makazi ya kudumu kuzunguka eneo la Hifadhi ya Mlima wa Kihesa hadi Kilolo katika Halmashauri ya Iringa Mjini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhalalisha eneo hilo na kuwapimia viwanja wananchi hao?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, naomba kutoa maelezo machache kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Msitu wa Hifadhi wa Iringa *(Iringa Local Authority Forest Reserve),* ulianzishwa mwaka 1953 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali *(GN. 109/10/04/1953)* kama Msitu wa Serikali Kuu kwa madhumuni ya uzalishaji *(Productive Forest).*

Mwaka 2002 umiliki wa msitu huu ulihamishwa na kutangazwa kuwa Msitu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kwa *GN. 37/11/1/2002.* Msitu huu una hekta 260 na una mchanganyiko wa miti ya kupandwa, miti ya asili, mbuga zenye uoto wa majani na miinuko yenye mawe makubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, ninaomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmsahuri ya Manispaa ya Mji wa Iringa imeomba matumizi ya eneo hilo yabadilishwe kutoka Msitu wa Hifadhi na kuwa na matumizi mengine yanayokusudiwa na Halmashauri hiyo ambayo yamechanganuliwa kama ifuatavyo:-

(i) 16% - Kuendeleza Ukanda wa Kijani *(Green Belt Development);*
(ii) 15%- Eneo kwa ajili ya kupanda miti;
(iii) 9% - Kuendeleza Utalii;
(iv) 2% - Maegesho ya magari; na
(v) 58% - Eneo kwa ajili ya Asasi *(NGOs)* za Kimataifa na za ndani, ujenzi wa Kambi za Makongamano na kuwekeza shughuli mbalimbali za kitalii.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu na lazima kwa Halmashauri na Miji yote nchini kutenga maeneo rasmi ya uoto wa asili na kupanda miti ili kutunza na kuboresha mazingira na hivyo kunufaika na uwepo wa Ukanda wa Kijani *(Green Belt).*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia *GN. 37/11/1/2002,* Serikali Kuu ilikabidhi rasmi Msitu wa Hifadhi wa Iringa wenye hekta 260 kwa sharti kwamba, Manispaa ya Mji wa Iringa iwajibike na matumizi endelevu ya msitu huo.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa, kabla sijauliza swali nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri ambayo ametupatia; kwa sababu msitu huu kwa kweli ulikuwa ni tatizo kubwa sana kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yaliyo karibu ukizingatia kwamba kuna Chuo cha Tumaini karibu na Msitu huo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi kuuliza swali moja tu la nyongeza. Huu msitu bado haujahaulishwa rasmi ndiyo tatizo kubwa ambalo Halmashauri inauliza. Je, ni lini utahaulishwa rasmi ili haya matumizi ambayo Halmashauri imeomba iweze kutumia?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Kabati, kwa kufuatilia sana suala hili la Msitu wa Iringa. Amezungumza na sisi Wizarani mara kwa mara na tunaamini ufumbuzi rasmi ikiwa ni pamoja na hili suala la kuhaulisha utapatikana.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba, Serikali ilipofika mwaka 2002 baada ya maombi ya Wanairinga, ilikubali kuwakabidhi Msitu huu sasa uwe wa Manispaa ya Iringa. Kwa hiyo, huu Msitu siyo wa Serikali Kuu tena.

Pili, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Manispaa ya Iringa wakiwepo Wabunge wote na Madiwani wote, wanawajibika moja kwa moja na mpango wa kuuendeleza huu Msitu na tutashirikiana nao katika yale yatakayojiri, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba dukuduku zao za kuhaulisha huu Msitu zinafanikiwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Pamoja na majibu mazuri aliyotoa lakini kimsingi pale hakuna msitu, wananchi wanapanda mahindi na vitu mbalimbali ijapokuwa kwenye makaratasi inaonekana kama ni msitu. Kinachosumbua kikubwa ni kwamba, Wizara yako inachelewesha kulifanya lile eneo liwe *gazetted* ili Mipango ya Manispaa yetu iweze kupangika vizuri?

SPIKA: Ahsante, una-*gazette* mahindi sasa! (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nirudie tena kama nilivyoanza, nimshukuru tena Mheshimiwa Msigwa na niseme tu kwamba, katika kufuatilia kilichopo hapa ni jinsi gani matumizi ya huu Msitu yatafanyika na ninakubaliana sana na Mchungaji Msigwa kwamba, kimsingi, Msitu huu uliharibiwa sana muda mrefu na ndiyo maana wao katika Halmashauri ya Iringa, walikubaliana kwamba ni muhimu wakaomba kubadilishwa matumizi.

Mheshimiwa Spika, kwa suala la ku-*gazette,* tayari katika Tangazo la Serikali *(GN. 37),* ilishatoka na tulishatoa hilo Gazeti la Serikali kuruhusu huu msitu uwe chini ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na kuuendeleza utakuwa ni wajibu wa Halmashauri ya Iringa.

Mheshimiwa Spika, sisi katika kuhakikisha kwamba wanafanikiwa, mchanganuo huu ambao niliueleza mwanzo wa asilimia zote ikiwa ni pamoja na kuupanda upya ndiyo *concern* kubwa sana ya Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mchungaji Msigwa na vilevile nimhakikishie Mheshimiwa Kabati kwamba, tutashirikiana nao kwa karibu tuweze kuona usumbufu au ucheleweshwaji wowote usio wa lazima uliotokea unaondolewa ili mipango mizuri ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa iendelee kutekelezwa.

Na. 26

Maeneo ya Ranchi za Kagera

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA (K.n.y. MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI) aliuliza:-

Mkoa wa Kagera ulikuwa na Ranchi za Kitengule, Missenyi, Mabale, Kagoma - Muleba na Kikulula - Karagwe ambapo baadhi ya maeneo yake yalikuwa yanamilikiwa kihalali na vijiji vinavyozunguka maeneo hayo wakiyatumia kwa shughuli za ufugaji lakini kutokana na ukiritimba wa kiutendaji wa kufanya maamuzi bila kufikia maeneo husika, baadhi ya vijiji na wananchi wake wamebinafsishwa:-

(a) Je, kwa nini wananchi waliokuwa wakiishi maeneo hayo wasiruhusiwe kuendelea na maisha yao kama walivyokuwa awali?

(b) Je, kwa nini Serikali isiyarudishe maeneo hayo kwani waliopewa wanayakodisha kwa wafugaji toka nchi jirani?

(c) Je, ni Watanzania gani kwa majina waliogawiwa maeneo kwenye ranchi hizo?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Mbunge wa Maswa Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatia uamuzi wa Serikali wa kumilikisha baadhi ya maeneo ya Ranchi za *NARCO* kwa Wawekezaji Watanzania, utekelezaji wa Ranchi za Mkoa wa Kagera ulifanyika mwaka 2005 kwa kugawa maeneo hayo katika ranchi ndogondogo. Jumla ya ranchi ndogo ndogo 52, zenye ukubwa wa kati ya hekta 500 na 2500 zilipatikana. Kati ya hizo, ranchi 14 zilitolewa kwa wanakijiji ili waweze kuyatumia na kuendeleza maisha yao na ranchi 38 zilitolewa kwa Wawekezaji wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini wawekezaji waliokiuka makubaliano kati yao na *NARCO* ya kufuga kisasa na kibiashara na badala yake kukodisha vitalu hivyo kwa wafugaji kutoka nchi jirani na wamiliki wa vitalu watakaobainika kukiuka mikataba yao, watachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

(c) Mheshimiwa Spika, orodha ya majina ya Wawekezaji Watanzania waliogawiwa maeneo hayo ya ranchi ipo, nitaomba kukutana na Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa ili nimkabidhi orodha hiyo.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika nakushukuru. Naomba kwanza nitamke wazi kwamba, majibu ya Mheshimiwa Waziri hayaendani na hali halisi iliyopo Mkoani Kagera na baadhi ya matamko ambayo yamekuwa yakitolewa hapa Bungeni:-

(i) Je, ahadi yako kwamba baadhi ya vitalu vitafutwa ilikuwa ni ahadi ambayo haiwezi kutekelezeka?

(ii) Kwa kuwa umesema kwamba orodha ya Wawekezaji Watanzania unayo hapa, mimi ningeomba orodha hiyo isomwe hata kama ni majina ya wawekezaji ambao siyo Watanzania isomwe hapa hadharani ili tuweze kuwajua. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, mkakati wa kugawa Vitalu vya NARCO ulianza kuzungumzwa mwaka 2002 na vitalu 124 viligawiwa, vitalu 44 havijapata hati (*sub lease*), lakini vitalu 80 tayari vina hati. Mwaka 2008 tulifanya tathmini na tukagundua kwamba, Kitalu Na. 11 cha Missenyi kilikuwa na matatizo, mwenyewe alikuwa anakodisha kwa wafugaji kutoka nje na tukamwandikia barua ya kutaka kumnyang'anya, lakini kesi hiyo iko mahakamani na imetajwa mara ya mwisho Oktoba, 2012.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 tulifanya tathmini vilevile tukagundua kwamba, kuna vitalu vinne; vitatu vya Mzeri Hill na kimoja cha *Uvinza Block No. 33.* Kkwa sasa vitalu vitatu vya Mzeri Hill vinafanya vizuri na kile cha Uvinza hakifanyi vizuri na hivyo juzi tulimwandikia barua ya kutaka kumnyang'anya. Mzeri wanaendelea vizuri kama nilivyosema, lakini mwaka huu tulifanya Mzeri, Uvinza na Usangu.

Mheshimiwa Spika, tunaposema tunanyang'anya, tunanyang'anya kweli, lakini kwa sababu yule ni Mtanzania ana haki, alimilikishwa kwa mkataba na ana haki ya kumiliki, ni lazima tuhakikishe kwamba kama ametekeleza vigezo vyote. Hatuwezi kumnyang'anya mtu ambaye hajapata hati miliki wala hajapata nguvu ya kukopa na kuendeleza. Kwa hiyo, kuna kucheleweshwa kupata hati miliki kutokana na matatizo mbalimbali, lakini tupo *serious* na tunanyang'anya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na orodha ya Wawekezaji Watanzania, ninayo hapa na ninaweza kuisoma kama Spika unaniruhusu lakini ni ndefu kidogo.

SPIKA: Kama ni ndefu, Kanuni zetu zinasema utasambaza.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Na. 27

Mahitaji ya Viwanda vya Nyama Nchini

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED aliuliza:-

(a) Je, Tanzania inahitaji viwanda vingapi na vya ukubwa gani vya nyama ili kukidhi ongezeko la idadi ya mifugo iliyopo nchini na kupanuka kwa soko la nyama duniani?

(b) Je, hivi sasa kuna viwanda vingapi vya nyama na vinasindika kiasi gani cha nyama?

(c) Je, viwanda vya kusindika samaki vipo vingapi na vinahitajika vingapi kukidhi idadi ya samaki waliopo?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania inahitaji viwanda ama machinjio makubwa takribani 16 yenye uwezo wa kuzalisha nyama tani 133 kwa siku kwa kila kiwanda au kila machinjio.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa kuna machonjio saba yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya tani 36,500 kwa mwaka. Machinjio hayo ni Sakina-Arusha tani 13,000, *Tendaji Foods Limited* kilichopo Morogoro tani 5000, SAAFI Sumbawanga tani 5000, *Orpul Limited* kilichopo Simanjiro kinazalisha tani 2,500 na *Manyara Ranch* tani 2,000 kwa mwaka. Aidha, Machinjio ya Dodoma ina uwezo wa kuzalisha tani 9,000 za nyama kwa mwaka.

(c) Mheshimiwa Spika, Tanzania ina jumla ya viwanda 19 kwa ajili ya kusindika samaki na mazao yake. Kati ya hivyo, viwanda saba vipo Ukanda wa Pwani kwa ajili ya kusindika samaki aina ya pweza, ngisi, kamba miti na kamba koche. Aidha, viwanda 11 vipo katika Ukanda wa Ziwa Victoria na vinasindika samaki aina ya sangara na kiwanda kimoja cha kusindika samaki aina ya migebuke katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimwia Spika, viwanda tisa vilivyopo Ukanda wa Ziwa Victoria vinatosheleza, kwa sasa kuna upungufu wa samaki katika maeneo hayo. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi katika eneo la Ukanda wa Bahari ya Hindi, ili kutumia rasilimali inayopatikana katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu. Aidha, Serikali inahamasisha uwekezaji katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa ambapo hapajawa na viwanda vya kutosha kutumia kikamilifu rasilimali ya samaki iliyopo.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Mheshimiwa Spika, kutokana na utafiti wa Serikali uliofanywa na Serikali, *UNIDO, FAO* na *IFAD* mwezi Septemba, 2012 wenye kichwa cha maneno kinachosema: *Tanzania Red Meat/Leather Value Chain;* Tanzania inasafirisha tani 200 tu za nyama wakati wenzetu Kenya wanasafirisha tani 400,000 kupeleka katika Soko la Ulaya tu peke yake. Kwa takwimu alizotoa Waziri hapa, inaonesha kwamba, viwanda hivi 16 vingeweza ku-*process* tani 760,000. Uzalishaji wa sasa ni kama asilimia 0.047 tu. Je, Serikali ipo *serious* kuvuna mazao haya ya mifugo ambayo ni karibu milioni 21.3 na kutoa ajira ya si chini ya watu milioni saba wanaotumia kwa mazao ya mifugo; je, Serikali kweli iko *serious* kwamba mpaka leo tunazalisha 0.047 tu ya nyama Tanzania wakati tuna nafasi kubwa ya kutoa ajira na kuongeza mapato katika nchi yetu?

(ii) Ukiangalia Sera ya Serikali ya *Fisheries* ya 1997, lengo kuu ilikuwa ni kuendeleza Sekta hii ya Uvuvi na kuhakikisha kwamba, watu wanapata ajira na kuongeza lishe. Hadi sasa ni Ukanda wa Ziwa tu ndiyo tumeweza ku-*export* thamani ya dola milioni 197. Kwa upande wa Bahari Kuu ni *zero* na Waziri katika majibu yake hapa amethibitisha kwamba, hakuna hata kiwanda kimoja cha samaki ukiacha ngisi na vitu vingine ambavyo vinachangia asilimia kumi tu. Je, Serikali kweli iko *serious* katika suala zima la kuvuna mazao yetu na kuwasaidia wananchi wetu?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hamad Radhid Mohamed, kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali wakati wote ipo *serious,* lakini nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba, mwanzoni mwa miaka ya tisini, Serikali ilifanya mabadiliko ya kuhodhi viwanda na biashara kuvipeleka kwa sekta binafsi na kuendesha badala ya Serikali yenyewe kuendesha viwanda na kufanya biashara, Serikali haifanyi biashara. Serikali inachofanya ni kutengeneza mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje kufanya biashara ama kujenga viwanda kama hivi vya samaki na machinjio. Kwa mfano, katika vivutio vya kujenga viwanda vya nyama ama machinjio, Serikali imetenga maeneo ya Themi, maeneo ya Ruvu, maeneo ya Kyaka, Magu pamoja na Bunda, kwa ajili ya kujenga machinjio na kodi

zimepunguzwa kwa mashine za kuchinjia pamoja na vifaa vya kufungashia kwenye viwanda vya nyama. Mikopo ya *TIB* inatolewa kabla hatujaanzisha Benki ya Kilimo ili watu waweze kukopa na kujenga viwanda vidogo vidogo na viwanda vikubwa. Tunatoa elimu ya unenepeshaji kusudi nyama zinazopatikana ziwe bora kutokana na ng'ombe wanaopatikana na mifugo mingine ikiwa ni mizuri.

Vile vile tunatoa ruzuku ya kuzuia magonjwa mbalimbali. Kila mwaka tunatoa ruzuku na tunahamasisha masoko ya ndani kuweza kununua nyama yetu inayozalishwa humu humu ndani ya nchi. Matokeo yake tuna machinjio ya Dodoma, tunajenga machinjio Ruvu, kule Sumbawanga kuna kiwanda cha kuchinja kile cha Mzee Mzindakaya, kule Arusha viwanda vipo pamoja na Simanjiro.

Kwa hiyo, juhudi hizo zinafanyika, sasa katika uwekezaji wa Ukanda wa Bahari, tatizo kwa wawekezaji wa ndani ni kwamba, inahitaji uwekezaji mkubwa, inahitaji mtaji mkubwa. Sasa tunafanya nini? Cha kwanza, tumeanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu iweze ku-*monitor* hali halisi ya uvuvi na kusimamia hata zile meli zinazotoka nje. Tumehamasisha kupitia *TIFA*, wenye viwanda na wanao-*process* samaki, waweze kwenda kuvua samaki kwenye Bahari Kuu. Vile vile kuna kodi ambazo zimepunguzwa za vifaa vya uvuvi ambazo zilikuwepo hapo nyuma sasa hivi tumeziondoa na sasa hivi Wizara yangu inaongea na Wizara ya Fedha waweze kuondoa *fuel levy* kusudi wenye meli kubwa waweze kwenda kwenye Bahari Kuu wakaweze kuvuna mazao yaliyoko kule. Kwa hiyo, juhudi za Serikali zipo na Serikali ya CCM iko *serious.*

Na. 28

Kilimo cha Ufuta – Mchinga

MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. SAID M. MTANDA) aliuliza:-

Kilimo cha Mazao ya Biashara hasa ufuta kimekuwa tegemeo kubwa kwa Wananchi wa Jimbo la Mchinga:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali haitoi kipaumbele kikubwa kwa zao hili ili Wananchi wapate moyo wa kulima mashamba makubwa na kuongeza tija?

(b) Je, ni pembejeo kiasi gani zimetolewa kwa Wananchi wa Mchinga kwa ajili ya kuendeleza Zao la Ufuta?

(c) Je, kwa nini malipo ya pili ya ufuta kupitia stakabadhi ghalani yanachelewa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa kipaumbele katika uzalishaji wa mazao nchini likiwemo Zao la Ufuta kwa lengo la kupanua nadharia ya Wakulima wa Tanzania kuwa na Mazao Makuu na Mazao Mbadala, ambayo kwa pamoja yote yanamwongezea uwezo wa kiuchumi mkulima wa nchi yetu. Serikali inafanya hivyo kwa kuboresha huduma za ugani, kutoa ruzuku ya pembejeo na kusambaza teknolojia mbalimbali kwa wakulima.

Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, katika kuongeza uzalishaji wa Zao la Ufuta, imenunua matrekta madogo ya mkono *(power tillers*) 101 na kuyakopesha kwa vikundi na watu binafsi katika Majimbo ya Mchinga na Mtama ili kuboresha kilimo likiwemo Zao la Ufuta. Aidha, Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo mfano, Shirika la *Care International* linaendesha mafunzo ya kilimo bora cha ufuta kupitia mashamba darasa.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, ilitumia jumla ya shilingi 7,500,000 kutoka Mfuko wa Pembejeo wa Wilaya kununulia dawa za kudhibiti wadudu waharibifu wa Zao la Ufuta, ambapo dawa hizo zilisambazwa kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi katika Majimbo ya Mchinga na Mtama. Mwaka 2011/2012, Halmashauri ilinunua tani tatu za mbegu ya ufuta zenye thamani ya shilingi 13,000,000 katika Kituo cha Utafiti cha Naliendele. Mwaka unaokuja (2013/2014), Halmashauri inakusudia kutumia jumla ya shilingi 30,000,000 kununua mbegu za ufuta na kuzisambaza kwenye Vijiji vinavyolima ufuta kwa utaratibu wa Kopa Mbegu kupitia Vyama vya Msingi vya Ushirika.

(c) Mheshimiwa Spika, mfumo wa stakabadhi ghalani kwa Zao la Ufuta Mkoani Lindi ulianza kutumika katika msimu wa 2009/2010 na 2010/2011 baada ya Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Lindi kuona manufaa yaliyopatikana katika mfumo huu kutokana na Zao la Korosho ambapo wakulima wa ufuta walikuwa wanalipwa kiasi cha shilingi 1,000 kwa kilo na baada ya mauzo wakulima walikuwa wanaongezewa fedha kutokana na ziada iliyokuwa ikipatikana. Malipo ya nyongeza yalitofautiana kutoka chama kimoja na kingine ambapo vyama vingine vilipata shilingi 1,200 kama bei na vingine vilipata shilingi 1,600 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa wakulima wa mazao ya nafaka na mazao mengine kama ufuta wanapata soko zuri na la uhakika bila ya kupunjwa, Serikali imeanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambayo ina jukumu la kununua mazao mchanganyiko ikiwemo Zao la Ufuta. Aidha, Serikali pia ipo katika mchakato wa kuanzisha utaratibu wa *Commodity Exchange,* ambao utawezesha uwepo wa uwazi zaidi kati ya mwuzaji na mnunuzi kwa manufaa ya wote wawili.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge hili kupitia Serikali yetu ilianzisha Sheria iliyounda Bodi ya Mazao Mchanganyiko na Bodi hiyo ndiyo ilikuwa maalum kabisa kwa ajili ya kukuza na kuboresha mazao hayo ili kuwapa tija wakulima, lakini mpaka sasa Bodi hiyo bado haijawezeshwa ipasavyo na Serikali ili kufanya kazi yake kama inavyotakikana:-

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ataliambia nini Bunge ili liweze kufahamu ni lini Serikali itaona umuhimu wa Bodi hiyo ili iweze kuboresha na kutoa huduma ipasavyo kwa mazao hayo mchanganyiko?

(b) Kwa kuwa ukomo wa Bajeti wa Serikali unapelekea Halmashauri nchini kushindwa kutenga fedha za kutosha kuhudumia mazao haya kama alivyosema yeye mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri; Halmashauri kule Mchinga imetenga shilingi milioni 30 tu kwa ajili ya zao hili la ufuta na Halmashauri nyingine ikiwemo Halmashauri yangu ya Wilaya ya Songea. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuandaa mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba wakulima wanaolima mazao haya mchanganyiko ambayo ni mazao yenye tija hayahitaji gharama kubwa ya uzalishaji waweze kupewa fedha inavyotakikana kuboresha mazao hayo na kuwaongezea kipato Wananchi wa Tanzania?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Bodi ya Mazao Mchanganyiko haijaanza kazi zake sawa sawa. Mpaka sasa hivi ni uteuzi wa Uongozi tu uliofanyika na bado kuna kazi ambazo zinajaribu kutenganishwa baina ya Bodi hiyo ya Mazao Mchanganyiko na majukumu yake na yale ya *NFRA* kwa maana ya *National Food Reserve Agency.* Kwa hiyo, hili jambo linafanyiwa kazi, tunaona umuhimu wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko, Serikali inaona umuhimu wa uwepo wake na ndiyo maana Bodi hii ilianzishwa. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Jenista kwamba, utaratibu unafanyika ili mgawanyo sahihi wa majukumu na mali ukamilike haraka iwezekanavyo na Bodi hii iweze kuwezeshwa ili ianze kutekeleza majukumu yake haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, hili la ukomo wa bajeti na kwamba labda wakulima ambao wanalima mazao mbadala wangepewa pesa moja kwa moja na Serikali, linaweza likawa gumu kidogo; isipokuwa kama nilivyosema na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo nae amelisema sana ni kwamba, tunajaribu kuhamasisha kwa jitihada ya makusudi kabisa kwamba pale ambapo wakulima wanaonekana wana mazao makuu lakini wana jitihada zao wenyewe za kuendeleza Mazao Mbadala ambayo yanayapa kinga yale Mazao Makuu yanapopata matatizo, Serikali iingilie kati kupitia kwenye Halmashauri, lakini na Serikali Kuu nayo kwa utaratibu wa kwamba kama watakuwa kwenye Vyama vya Ushirika wanakuwa rahisi kukopesheka na kuwezeshwa.

Na. 29

Vyama vya Ushirika Kufanya Ubadhirifu

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA aliuliza:-

Kumekuwepo na malalamiko kuwa Vyama Vikuu vya Ushirika hufanya ubadhirifu wa fedha za ushirika:-

Je, hali hiyo inapotokea Serikali husaidiaje?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, yapo matukio ya ubadhirifu wa fedha na mali za baadhi ya Vyama vya Ushirika. Aidha, inapotokea kuwepo ubadhirifu wowote ndani ya Chama husika, Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2003, kwanza, inawataka wanachama wenyewe kuchukua hatua, lakini pia inamruhusu Msajili wa Vyama vya Ushirika kwa niaba ya Serikali kuwachukulia hatua za kisheria wakosaji kulingana na makosa yao.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo huchukuliwa baada ya kufanyika ukaguzi au uchunguzi ili kubaini na kuthibitisha ubadhirifu huo. Aidha, watuhumiwa wa ubadhirifu huweza pia kuchukuliwa hatua za kisheria kupitia Vyombo vingine vya Sheria kama vile Polisi na TAKUKURU, kutegemeana na hali halisi ya tuhuma na mazingira yake. Hadi sasa kuna Vyama Vikuu na vya Msingi vilivyo katika hatua za ukaguzi na uchunguzi kufuatia malalamiko ya wadau wake kuhusu ubadhirifu. Kwa mfano, katika Mikoa ya Ruvuma, Mtwara, Lindi, Pwani, Mwanza, Kagera, Kilimanjaro na Tabora.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baada ya kuzingatia mazingira ambayo Sheria hii ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2003 inavyofanya kazi katika mazingira ya kiuchumi na kijamii ya sasa ya wakati huu, Serikali na Wadau wa Ushirika wamesisitiza ulazima wa kufanya mabadiliko ya msingi ili Sheria ya Ushirika ikidhi mahitaji ya wadau wake kwa wakati huu. Pamoja na maeneo mengine mengi, vipengele vinavyoainisha adhabu na hatua stahili zimeonekana kutokidhi. Kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali inaleta hapa Bungeni na leo Muswada utasomwa kwa mara ya kwanza, Muswada wa Mbadiliko ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013 ili kuboresha usimamizi wa rasilimali na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu na dhamana za Vyama vya Ushirika katika ngazi zake zote.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Napenda nimuulize Waziri kwamba yapo malalamiko makubwa kabisa juu ya ubadhirifu uliopo katika Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Kagera, *KCU 1990 Limited* na malalamiko hayo yako mezani kwako tangu mwaka jana. Hadi hivi sasa hatujapata matokeo ya malalamiko hayo na napenda kuuliza ni kwa nini Serikali inachukua muda mrefu kushughulikia malalamiko haya ambayo yanaweza kufanya wale wanaotuhumiwa kupata nafasi ya kujipanga?

(ii) *COASCO* ni Chombo ambacho kinafanya ukaguzi wa Ushirika. Mwaka jana yalitokea malalamiko kutoka kwa Wafanyakazi walio Mkoani kwamba Mkaguzi Mkuu wa *COASCO* amewaelekeza wasikague Vyama Vikuu vya Ushirika wakague Vyama vya Msingi tu. Katika malalamiko hayo, inaonesha kwamba Mkaguzi Mkuu ana namna alivyo na mahusiano na Vyama Vikuu vya Ushirika. Kutokana na majibu yako ya msingi Mheshimiwa Waziri, umetaja baadhi ya Vyama ambavyo vimetuhumiwa kwa ubadhirifu. Je, katika hali hiyo nani ambaye atakagua Vyama hivyo na kupata matokeo mazuri?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tumepokea malalamiko ya *KCU* Wizarani na kwa bahati nzuri walikuja Viongozi wenyewe wa *KCU* na Mheshimiwa Waziri nae amekwenda kuzungumza nao. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linafanyiwa kazi. Zipo tuhuma za aina nyingi kwa pande zote, kuanzia mgogoro wa tangu uchaguzi wenyewe ulivyofanyika ndani ya *KCU.* Kwa hiyo, lile jambo liko *complex* kidogo, halina wepesi wa kulifanyia maamuzi ya leo na kesho. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kuchelewa kidogo kufanya maamuzi hali inaweza ikawa ina matatizo kidogo, lakini naomba nikuahidi kwamba, Mheshimiwa Waziri analifanyia kazi na bahati nzuri na mimi mwenyewe alinipa maelekezo na nimekuwa nalifanyia kazi hili jambo. Hili jambo ni zito kidogo, kwa sababu lina mgogoro wa namna nyingi pale *Kagera Cooperative Union,* lakini tutalipatia ufumbuzi haraka iwezekanavyo katika maeneo yake yote ili tatizo hili lisijirudie tena.

Mheshimiwa Spika, hili la *COASCO*; *COASCO* kama Chombo cha Ugakuzi cha Vyama vya Ushirika ni kweli limepatiwa malalamiko na limefanyiwa malalamiko kote siyo kwa masuala ya Kagera tu, hapana na kwa kiasi kikubwa tumejaribu kufanya mabadiliko ndani ya *COASCO* lakini kiukweli kabisa, mfumo wa usimamizi wa Ushirika una matatizo baina ya usimamizi na uhamasishaji. Kwa hiyo, ndiyo maana tumesema Sheria hii mpya inakuja kutenga majukumu maalum ya usimamizi na adhabu zake na kadhalika na watu wake wa kushughulikia hilo na upande mwingine uhamasishaji na watu wake wa kushughulikia hilo. Tunaamini kabisa

kwamba, katika utaratibu huu, mabadiliko mapya haya ya Sheria ambayo itasomwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni leo, yatatuondolea matatizo haya kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na maswali yamekwisha, naomba tuendelee na hatua inayofuata. Kwanza kabisa, napenda nitambue wageni tulionao hapa Bungeni. Leo tumefikiwa na Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Bunge la Uganda, wamekuja kwa ajili ya kuonana na kushirikiana kufanya kazi pamoja na Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Wajumbe wa kutoka Uganda wanatoka Kamati inayoitwa Kamati ya Jinsia, Kazi na Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, wapo hapa Bungeni wanaongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Nokrach William; tafadhali msimame, ahsante. Karibu sana.

Wabunge wengine waliofuatana na Kiongozi huyu ni Mheshimiwa Nuwat Rosemary; ahsante sana na Mheshimiwa Kabahenda Flavia; ahsante sana. Kuna Mheshimiwa Babadiri Margaret, ahsante sana. Tuna Mheshimiwa Ssentongo Teopista Nabulya, ahsante sana. Hawa ndiyo Waheshimiwa Wabunge, lakini wamefuatana na Maafisa wa Bunge; kuna Afisa wa Bunge anaitwa Manzi Victor, asimame; ahsante sana. Yupo Msaidizi wa Mbunge, Oyet Daniel, ahsante. Kuna mwingine Msaidizi wa Mbunge, Apia Susan; ahsante sana.

Tunawakaribisheni sana katika maeneo yetu hapa Dodoma na mjisikie mko huru, watakuwa na Kamati lakini saa tano watakutana na Naibu Spika, kwa ajili ya *courtesy call,* mimi nitakuwa hapa ndani. Kwa hiyo, mnakaribishwa sana, mjisikie mpo nyumbani. Tuna Mheshimiwa Dkt. Ad Koekkoek, Balozi wa Uholanzi nchini, ambaye ameambatana na Afisa wa Ubalozi, Bi. Agnes Hanti; ahsanteni sana na karibuni sana.

Wageni wengine waliofika kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 30 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wanaosoma Shahada ya Uzamili katika Uhusiano wa Kimataifa, ambao pia ni wanafunzi wenzake Mheshimiwa Juma Nkamia. Naomba wasimame walipo wanafunzi hao wa *UDOM;* karibuni sana. Ninaamini kabisa mnafanya bidii kusoma. Bila kusoma sasa dunia itawaacha pembeni, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 kutoka kikundi cha *Amani Group* cha Dodoma, wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Jairos Magawa Lekutu. Hawa wako wapi Amani? Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu kutoka Shirika la *Tanzania Cheshire Foundation* la Morogoro; sijui hawa wako wapi, wako watatu. Karibuni, nadhani watakuja. *(Makofi)*

Wageni wengine, tunao wageni watano (5) wa Mheshimiwa Meshack Opulukwa, ambao ni kikundi cha waendesha pikipiki, maarufu *Bodaboda,* kutoka Meatu wakiongozwa na Katibu wao ndugu Charles Masanja pamoja na Mwenyekiti wa Tawi la Mshikamano la CHADEMA Meatu, ndugu Majula Nsulwa. Nategemea hamkuendesha *Bodaboda* mpaka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi; Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo tarehe 30, kutakuwa na kikao cha Kamati pamoja na wageni wa Bunge, kutoka Uganda. Kikao ambacho kitafanyika katika Ukumbi Namba 219, Jengo la Utawala, saa tano na nusu asubuhi. Kwa hiyo, Kamati ya Maendeleo na Jamii, wakutane chumba namba 219, kukutana na hawa wageni wenu. Naomba mfike pale, isionekane kama hampo.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, watakuwa na Kikao leo, saa saba mchana katika ukumbi wa Msekwa B.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama Katibu wa *Caucus* ya Chama cha Mapinduzi Bungeni, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM kuwa, leo tarehe 30, saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati cha chama, ukumbi wa Msekwa. Saa saba mchana, *Caucus* ya CCM watakuwa na kikao chao.

Mheshimiwa David Silinde, yeye ni Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kuwa, leo tarehe 30, saa saba mchana kutakuwa na kikao kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa hiyo, wote hao mnaombwa mhudhurie kunakostahili.

Tunaendelea, Katibu!

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa kwa Mara ya Kwaza)

Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2013
(The Cooperative Societies Bill, 2013)

Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2013 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2013)*

(Miswada iliyotajwa hapo juu Ilisomwa
Bungeni kwa Mara ya Kwanza)

HOJA BINAFSI ZA WABUNGE

Hoja binafsi ya Mheshimiwa Mwigulu L.N. Madelu kuitaka Serikali iwasilishe Bungeni Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Elimu ya Juu
(The Higher Education Fund Act)

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuwasilisha Hoja yangu Binafsi, mbele ya Bunge lako Tukukufu.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijatoa hoja hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 61(1), inayomtaka Mbunge, kuweka wazi maslahi binafsi kwenye jambo analotaka kulizungumzia kabla hajalizungumzia. Niweke wazi kwamba, mimi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, ninafanya *PhD* ya Uchumi lakini la pili, niweke wazi kwamba na mimi ni mnufaika wa mikopo, nilikopeshwa lakini nilishalipa, sidaiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, nifanye marekebisho kidogo kwenye Hoja. Kwenye sababu nilizosema zimesababisha nilete Hoja hii, nimeongeza sababu ya nne (4) kama ambavyo itasomeka na nilileta kiambatanisho hicho kwenye Kiti chako.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye kipengele kilichokuwa kinaelezea vyanzo pale paliposomeka *TICRA,* iondoke ile (*l)* ibaki *TCRA,* palikuwepo na (*l)* katikati.

Mheshimiwa Spika, lakini na kwenye Mapendekezo pale palipokuwa panasomeka “Mototo”, pasomeke “Mtoto”.

Mheshimiwa Spika, baada ya marekebisho hayo, naomba sasa niende kwenye Hoja yenyewe. Hoja yangu inakusudia kuliomba Bunge lako Tukufu, liazimie kwa kauli moja kuitaka Serikali kuleta Bungeni Muswada wa Sheria wa Kuanzisha Mfuko wa Elimu ya Juu *(The Higher Education Fund Act).* Sheria hii ni Sheria itakayowezesha kuundwa Chombo cha Mfuko wa Elimu ya Juu na ikiwezekana kipewe hadhi ya kibenki, ili kiwe na uwezo wa Kisheria kiufuatiliaji wa madeni ya wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, lakini Sheria hii pia itaipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia elimu ya juu kwa bajeti ya Serikali, inayoumiza Idara nyingine za Wizara. Kwa mfano, takribani ya 80% ya matumizi mengineyo *(OC)* ya bajeti ya Wizara ya Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2012/2013, ilielekezwa kwenye mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii pia itawezesha kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato na mfumo wa kukopesha wanafunzi wa Vyuo Vikuu kupitia Taasisi za Kibenki, kama vile Mifuko ya Hifadhi za Kijamii pamoja na Benki. Hii itawezesha kukopesha kila mwanafunzi aliyepata nafasi ya kujiunga na elimu ya juu kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msingi wa Hoja yangu ni madhara yanayojitokeza kutokana na mfumo uliopo wa utoaji wa mikopo unaokwamisha nia njema ya Serikali ya kutoa elimu ya juu kwa Watanzania walio wengi, hususan watoto wa maskini kama ifuatavyo; kwa mfano, kwa mfumo uliopo hautahimilika kadiri idadi ya wakopeshwaji itakavyoendelea kuongezeka, kiwango cha mikopo kitakavyoendelea kuongezeka kutokana na kupanda kwa gharama za maisha na kushuka kwa thamani ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano uliopo, kwa mwaka 2004/2005 zilitumika zaidi ya shilingi bilioni tisa (9) kwa ajili ya wanafunzi zaidi ya 16,000 kwa kiwango cha 2,500/= kwa siku na kwa mwaka 2005/2006 kwa wanafunzi 42,729 zilitumika takribani shilingi bilioni 56.1 na kwa mwaka 2011/2012 zilitumika shilingi bilioni 320 kwa ajili ya wanafunzi 94,773 kwa kiwango cha 7,500/= kwa ajili ya chakula na malazi. Hii ni kwa mujibu wa Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013 tunakoelekea 2013/2014 idadi ya wanafunzi itaongezeka, zitahitajika zaidi ya shilingi bilioni 500 na tufikapo mwaka 2019/2020 zitahitajika zaidi ya shilingi bilioni 830 ili kukopesha takribani wanafunzi 170,000 wenye sifa. Kwa hiyo, kwa takwimu hizo tukiendelea na utaratibu huu itafika wakati ambapo Bodi haitaweza tena kuhimili ukopeshaji wa wanafunzi wa elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu kuu ya pili; mfumo uliopo unawanyima wanafunzi wenye sifa kupata mikopo na unatoa mikopo kwa utaratibu ambao ni vigumu kufanya kwa haki na usawa, licha ya uwazi na utaratibu unaotumika kuwatambua. Mfano, katika msimu wa maombi uliopita 2011/2012, jumla ya maombi yalikuwa 113,356 na wapya wenye sifa walikuwa 38,541. Takwimu zinaonesha kwamba, wanafunzi 26,538 tu ndio walioweza kukopeshwa hivyo wanafunzi elfu 12,003 walikosa mikopo na kupoteza fursa ya masomo kwa kusitishiwa udahili. Inaonekana wanafunzi wa familia masikini inatokea anakosa mkopo au anapata 10% au anapata 20% ambazo hazitoshelezi mahitaji na wakati uleule mwenye uwezo anapata. Uwepo wa Mfuko wa Elimu ya Juu utawezesha yeyote aliyefaulu na kupata nafasi chuoni, kupewa mkopo kwa kiwango anachohitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhaba wa fedha kwa ajili ya mikopo unaathiri taaluma za wanachuo. Uchunguzi niliofanya, mosi, unasababisha wanachuo kuwa na maisha magumu, usumbufu wa wanafunzi na kupoteza muda kwa kufuatilia mikopo. Lakini la pili, uchunguzi niliofanya inasababisha wanafunzi wengine kwenda kusoma taaluma wasizozipenda kwa kuwa tu zinamuwezesha kupata mkopo kirahisi. Kwa mfano, Serikali ilipotangaza kutoa mkopo kwa 100% kwa taaluma ya Ualimu, inawezekana imesababisha wanafunzi wengi kujiunga na Ualimu bila kupenda kuwa Walimu. Hivyo, akimaliza na kupangiwa kwenda kufundisha, haendi kuripoti na badala yake anatafuta nafasi nyingine ya kusoma Shahada ya Uzamili ya taaluma nyingine tofauti na Ualimu au kufanya shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu. Kwa kuwapa yatima mikopo 100% inawezekana kwamba, akawa yatima lakini aliachiwa miradi ama mali kwa hiyo, akapata 100% wakati yule mwenye wazazi hawana uwezo, akapata 10%. Kwa hiyo, kuna taarifa baadhi ya wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kulipa ada, wameanza kusingizia kwamba, wazazi wao walishafariki na kupewa Hati za Bandia za Vifo, ili kuweza kupata mkopo kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, sababu ya nne. Urejeshwaji wa mikopo hauridhishi ni takribani 30%, unasababisha Bodi isiweze kujiendesha na kuwa endelevu. Hii inatokana na wanafunzi na wazazi na walezi na jamii kwa ujumla, kuchukulia mikopo kama ruzuku kutoka Serikalini na ni tofauti na mikopo mingine. Mfano, hadi Agosti 2012, ni takribani wahitimu 43,000 kati ya 110,000 ndio waliopatikana na takribani shilingi bilioni 22 ziliweza kupatikana kati ya shilingi bilioni 160 ambazo zingepatikana kama wote wangeweza kutambulika. Hii ni tofauti na sehemu nyingine kama Afrika Kusini, ambako marejesho ni zaidi ya 70% ambayo yanawezesha Bodi kujiendesha na kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba sasa nibainishe vyanzo vya mfuko kabla ya kuliomba Bunge lako Tukufu kuazimia. Napendekeza ili kutunisha Mfuko wa Elimu ya Juu, Serikali ianze na kuuza Hati Fungani ya Elimu *(Education Bond)* ya kipindi kitakachokubalika na soko ili kupata fedha ambazo zitaingizwa katika Mfuko wa Elimu ya Juu kwa ajili ya kukopesha wanafunzi. Katika soko la awali la Benki Kuu ya Tanzania, kuna Hati Fungani za aina nne (4) zinazokuwa tayari ambazo ni za miaka 2, 5, 7 ama 10 ambazo zinaweza kuwekwa sokoni kwa niaba ya Serikali na Benki Kuu. Vigezo vilivyowekwa vitatumika kupima uwezo wa Serikali wa kibenki, bila kuathiri jitihada za ndani za chombo hicho kudhibiti mwenendo wa ujazi wa fedha zitabainisha kiasi kitakachouzwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri jambo hili liende sambamba na Mfuko wa Kulipia Madeni *(Sinking Fund),* kwa ajili ya kutoa fedha za kutosha kulingana na kuiva kwa Hati Fungani *(Bond's Maturity)* na kulipwa Mfuko wa Elimu ya Juu utakaosaidia kuratibu mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kupitia taratibu za urejeshwaji wa mikopo. Mfuko huo utasimamiwa kwa pamoja na Benki Kuu ya Tanzania na Serikali itawajibika kwa deni katika kipindi cha uhai wa Hati Fungani. Serikali, inaweza kupata takribani shilingi bilioni 100 kwa ajili ya Mfuko wa Elimu ya Juu kutokana na kujihusisha kwenye soko hilo.

Mheshimiwa Spika, upo mfano wa jinsi Serikali inavyoshiriki katika kutoa Hati Fungani. Katika kipindi cha mwezi Januari 2011 mpaka Januari 2012, Serikali ilitenga Hati Fungani zenye thamani ya shilingi bilioni 865 lakini iliweza kutoa shilingi bilioni 654.7 hii ilisababisha kuwa na upungufu wa kifedha *(Financing Gap)* wa shilingi bilioni 210. Tangu Juni 2011, riba imekuwa ikiongezeka katika Hati Fungani za aina zote ikionesha ongezeko la gharama za programu ya ukopaji wa ndani wa Serikali, kwa hiyo, hili linawezekana.

Mheshimiwa Spika, chanzo kingine; zipo hisia kwa Watanzania kuwa, makampuni ya simu za mikononi hayaweki wazi mapato halisi ya makampuni yao na hayalipi inavyostahili. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA),* ifunge haraka mtambo utakaoonesha mapato halisi ya makampuni ya simu. Uzoefu wa nchi zenye mitambo ya kuonesha mapato halisi ya kampuni za simu zinanufaika sana na inaonesha kuwa Tanzania ina uwezo wa kupata bajeti yote na zaidi, ya elimu ya juu kutoka chanzo hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Ghana yenye takribani watumiaji wa simu milioni 18, inakusanya zaidi ya 10% ya mapato ya ndani ya Serikali. Watumiaji wa simu nchini Tanzania wameongezeka, kutoka 280,000 mwaka 2000 mpaka zaidi ya milioni 28 kwa mwaka 2012. Hivyo basi, Tanzania ikikusanya 10% tu kutoka kwenye eneo hili itakuwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 850 na kupeleka moja kwa moja kwenye Mfuko wa Elimu ya Juu na kukopesha 100% kwa yeyote aliyepata kudahiliwa na aliyefaulu kwa kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara zinazosimamia moja kwa moja rasilimali za Taifa mfano kama Maliasili na Utalii, Nishati na Madini, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mifugo na Uvuvi, zipangiwe kiwango cha fedha cha kuchangia kwenye Mfuko wa Elimu ya Juu kila mwaka. Rasilimali zinazotoka hapa kama madini, zikichimbwa hazirudi ardhini; hivyo kiuchumi ni vyema kutumia rasilimali kama hiyo, kuwekeza, kuendeleza rasilimali watu ili kukuza uzalishaji katika maeneo mengine ya uchumi, ili kuweza kupata kodi hata kama madini yakiisha. Kitengwe kiwango kitakachotoka katika sekta hizi kwenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa Elimu ya Juu. Vilevile napendekeza mchango wa Serikali, kwenye Mfuko wa Elimu ya Juu, usipungue 20% ya makadirio tutakayoanzanayo ili Mfuko huo uweze kuimarika na kuwa Mfuko endelevu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali itilie maanani kodi ya ardhi, majengo na pango ili hiki nacho kiwe chanzo cha kudumu cha uhakika kuchangia katika Mfuko wa Elimu ya Juu. Moja ya kodi ambazo hazijakusanywi vizuri, zinakusanywa kwa kiwango cha chini hapa nchini, ni pamoja na kodi ya ardhi na majengo. Ifanyike sensa ya majengo na urasimishwaji ardhi ili kuweza kukusanya kodi na kutunisha mfuko. Kwa sasa sio ajabu kukuta mtu amejenga maghorofa, halipi kodi na mwanaye anapata mkopo Serikalini lakini mtoto wa mwenye nyumba ya tembe anakosa mkopo. Kukiwa na orodha ya nyumba na ardhi zikipimwa na wamiliki wake wakajulikana ni rahisi kukusanya kodi.

Mheshimiwa Spika, chanzo kingine, naomba ieleweke wazi kuwa, tunatoa mkopo, tunawakopesha wanafunzi wa elimu ya juu lakini tunapodai anayerejesha mkopo ni mnufaika wa mkopo ambaye yuko kazini, mwenye kipato, ili tukopeshe wanafunzi wengine wasio na uwezo na wasio na kipato. Napendekeza mikopo itozwe riba kidogo kuliko inayotozwa kwa sasa kwa kupitia madirisha maalum ambayo nitayaelezea. Kwa kiwango cha riba kama itachanganuliwa iwe sawa na ukopaji wa Serikali yaani *Government rate of borrowing,* hii itasaidia kulinda thamani ya mkopo na kusaidia mkopo usiolipwa kuongezeka kwa kiwango sawa na kile cha uuzwaji wa dhamana.

Mheshimiwa Spika, mikopo ni gharama, kuna gharama ya kufuatilia, kuna gharama ya kuendesha mfuko, kwa hiyo, napendekeza hii ili iweze kusaidia katika mambo mawili. Jambo la kwanza, faida ya kuweka riba kidogo kwa wale wanaotokea makazini itasaidia kulinda thamani ya mkopo lakini pia itasaidia kuwezesha mifuko ya hifadhi ya kijamii kuanzisha dirisha au fao maalum la elimu ya juu ili kuwakopesha wanachama wao na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hii itapanua upatikanaji wa mikopo kwa wale wanaotokea makazini. Kwa miaka mitatu sasa wanafunzi wanaotokea maofisini hawapati mikopo kutokea bodi, likianzishwa dirisha maalum kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kwa wanachama wao,

itawasaidia kupunguza msongamano kwenye mfuko wa Elimu ya Juu ambao utahudumia wanafunzi wanaotokea Sekondari.

Mheshimiwa Spika, pia riba itawezesha wanafunzi ambao wanatokea maofisini kukopa moja kwa moja kutokea kwenye Taasisi za kibenki yaani Mabenki kwa kutumia vitambulisho vyao vya chuo na vya uraia kwa dirisha maalum ambalo benki hiyo itakayokopesha itakuwa imekopa kwa riba nafuu kutoka benki kuu. Hii itailazimu tu Serikali iweke kwenye bajeti yake malipo ya riba itakayotozwa wakati wa kipindi cha neema yaani *grace period* ambayo mwanafunzi hataweza kulipa riba wakati wakiwa masomoni. Fedha hizo zinaweza kuwekwa benki kuu kama mfuko maalum ambao mabenki yatakayokopesha wanafunzi yatapewa mkopo kwa riba nafuu na hii itawezesha riba inayotolewa iwe ndogo kuliko hii ya kisheria ya sasa ambayo inawataka walipe kwa 6%.

Mheshimiwa Spika, chanzo kingine, hotuba ya Waziri wa Fedha ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012 na 2012/2013 iliweka wazi lengo la kupunguza misamaha ya kodi mpaka kufikia 1% ya pato la Taifa. Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (*CAG)* juu ya makusanyo ya mapato yatokanayo na kodi yanayoonyesha kuwa kuna ongezeko kubwa la misamaha ya kodi toka shilingi bilioni mia sita themanini kwa mwaka 2009 hadi shilingi trilioni moja nukta sifuri moja kwa mwaka 2010/2011 sawa na ongezeko la shilingi bilioni mia tatu thelathini na tano. Kwa kuwa Serikali inajaribu kufuta baadhi ya misamaha ya kodi mwaka 2010/2011 hoja hiyo ikapata upinzani Serikali ipunguze misamaha ya kodi mpaka 1% ya pato la Taifa ili kuweza kusaidia kuwa na uwezo wa kufidia fedha hiyo itakayotoka moja kwa moja na ikapelekwa moja kwa moja kwenye mfuko wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa niwasilishe hoja yenyewe, hoja hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, Kanuni ya 54(i).

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA asilimia kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu ni watoto wa maskini ambao wazazi ama walezi hawana uwezo wa kumudu gharama za elimu ya juu;

NA KWA KUWA, kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi wenye sifa wanaodahiliwa kujiunga na vyuo vikuu na kufanya Serikali kushindwa kuwapa mikopo wote wanaohitaji kwa 100% kwa kutumia bajeti ya Serikali;

NA KWA KUWA, kumekuwa na uhitaji wa nyongeza ya viwango vya mikopo kutokana na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania na kupanda kwa gharama za maisha kutokana na mfumuko wa bei;

NA KWA KUWA, kumekuwa na urejeshwaji duni wa mikopo kutokana na mikopo kutolewa kama ruzuku hivyo kuwanyima fursa wanafunzi wengine kupata mikopo;

NA KWA KUWA, mfumo mzima uliopo siyo endelevu na hautahimilika tunakoelekea kutokana na idadi ya wakopeshwaji itakavyokuwa inaongezeka;

HIVYO BASI, naliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuitaka Serikali, kwa haraka itakavyowezekana, ilete Muswada wa sheria Bungeni wa kuanzisha Mfuko Elimu ya Juu. Pamoja na mambo mengine, sheria itakayoweka taratibu mbalimbali zitakazowezesha upatikanaji wa fedha kutoka kwa wadau wa elimu, kutoka kwenye kodi na tozo kwenye taasisi mbalimbali kugharimia elimu ya juu kwa kuanzisha Mfuko wa Elimu ya Juu yaani *The Higher Education Fund.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Naona hoja hiyo imeungwa mkono, sasa nitamwita Waziri wa Elimu aweze kufanya *amendment* zake kutokana na mawasilisho yaliyopo, nafikiri *document* hiyo umesambaza pia kwa wote.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, *document* inasambazwa, sasa kwa ruhusa yako, naomba nianze kusoma.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Uchangiaji wa Gharama za Elimu ya Juu inatekelezwa nchini kama ilivyo katika nchi nyingine za Afrika zikiwemo Kenya, Afrika Kusini na Ghana. Kwa Tanzania, Sera ya Uchangiaji ilianza rasmi mwaka 1992 kwa Waraka wa Utumishi Na.6 wa mwaka 1992 na utekelezaji wa sera hii umefanywa katika awamu tatu.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza imetekelezwa kati ya mwaka 1992 hadi 1994. Katika awamu ya kwanza, mwanafunzi, mzazi ama mlezi au mdhamini alichangia kugharimia mambo yafuatayo:-

(i) Posho ya elimu ya juu;
(ii) Fedha za tahadhari;
(iii) Michango ya Jumuiya ya Wanafunzi;
(iv) Usafiri wa kwenda na kutoka vyuoni; na
(v) Matibabu.

Mheshimiwa Spika, gharama nyingine zote za elimu ya juu zilizogharimiwa na Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Ada ya mafunzo;
(ii) Mahitaji ya vitivo;
(iii) Chakula na malazi;
(iv) Gharama za mafunzo kwa vitendo; na
(v) Utafiti. Hivi vyote viligharimiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika awamu hii, Serikali ilikuwa na Vyuo Vikuu viwili tu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Narudia tena, katika kipindi hicho, Serikali ilikuwa na Vyuo Vikuu viwili tu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, aidha, kulikuwa na vyuo vingine vya elimu ya juu vilivyokuwa vinatoa stashahada ya juu. Kwa wakati huo hapakuwa na vyuo vya elimu ya juu vya binafsi.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya Sera ya Uchangiaji ilitekelezwa kati ya mwaka 1994 hadi mwaka 2005. Baada ya tathmini ya awamu ya kwanza, awamu ya pili ilianza Julai mwaka 1994. Pamoja na gharama za awamu ya kwanza, wanafunzi walitakiwa kuchangia gharama za chakula na malazi kwa wastani wa shilingi 350,000/=. Kwa kuzingatia kuwa Watanzania walio wengi wasingeweza kumudu kupata fedha hizo, Serikali ilianzisha utaratibu wa kutoa mkopo kwa wahitaji. Utaratibu wa utoaji mikopo ulisimamiwa na iliyokuwa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004, Serikali ilipitisha Sheria Na.9 ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, kwa Kiingereza *The Higher Education Students' Loan Board Act, Cap*. 178. Sheria hii ilianzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kama chombo cha kusimamia utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, awamu ya tatu ilianza kutekelezwa mwaka 2005 na imeendelea mpaka hivi sasa. Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilianza kazi mwaka 2005/2006 na awamu ya tatu ya uchangiaji gharama za elimu ya juu ikaanza kutekelezwa. Katika awamu hii, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Mheshimiwa Spika, niwie radhi nadhani kuna *page* moja hapa ina-*miss,* aah, nimeipata.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilipewa mamlaka ya utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ikiwemo urejeshwaji wa mikopo iliyotolewa tangu mwaka 1994. Kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, gharama zinazotakiwa kulipiwa na wanafunzi kwa njia ya mikopo ni zifuatazo:-

(i) Chakula na malazi;
(ii) Ada ya mafunzo;
(iii) Vitabu na viandikwa;
(iv) Mahitaji maalum ya vitivo;
(v) Mafunzo kwa vitendo;
(vi) Gharama za utafiti; na
(vii) Mahitaji maalum kwa wanafunzi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, utoaji wa mikopo katika awamu hii unazingatia kigezo cha uwezo wa kiuchumi wa mwombaji, uyatima na programu za kipaumbele za Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ilikuwa ni hatua kubwa kwa Serikali katika jitihada za kuwezesha wanafunzi walio wengi kujiunga na vyuo vya elimu ya juu. Lengo kuu hasa lilikuwa ni kuwezesha wanafunzi wenye sifa za kitaaluma lakini ambao ni wahitaji au hawana uwezo wa kifedha waweze kupata fursa za kujiunga na elimu ya juu kwa kuchangia na hivyo kutekeleza kwa vitendo dhana ya uchangiaji wa elimu ya juu hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Tume ya Rais ya mwaka 2011, inaonyesha kuwa, idadi ya wakopeshwaji imekuwa ikiongezeka kwa kiasi cha 15% kwa mwaka na kiwango cha mkopo kinaongezeka kwa 19% kwa mwaka. Hii ina maana kwamba hali halisi ya ongezeko la matumizi kwa ajili ya mikopo ilikuwa kwa kati ya 35% hadi 36% kwa mwaka. Kasi hii isipodhibitiwa, bajeti kwa ajili ya mikopo itaongezeka hadi kufikia kiasi cha 69% ya bajeti yote ya elimu itakapofikia mwaka wa fedha 2014/2015. Ni dhahiri kwamba bajeti ya Serikali haitaweza kuhimili mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi wanaokopeshwa na Bodi ya Mikopo kwa mwaka imeongezeka kutoka wanafunzi 42,729 mwaka 2005/2006 hadi kufikia wanafunzi 93,149 mwaka wa masomo wa 2011/2012. Aidha, fedha za ukopeshaji zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 56.1 mwaka 2005/2006 hadi kufikia shilingi bilioni 326 mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka wa masoma 2011/2012, idadi ya wanafunzi ambao wamenufaika na mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iliyoanza kazi rasmi mwaka 2005 ni wanafunzi 228,701 na hapa nataka kurekebisha namba ile ambayo

ipo katika taarifa ambayo nimeisambaza. Jumla ya mkopo ambao umeshatolewa chini ya usimamizi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ni shilingi trilioni 1,133,386,869,067.58. Aidha, idadi ya wanafunzi wote walionufaika na mikopo kati ya Juni mwaka 1994 hadi Juni 2012 ni wanafunzi 277,079, tena naomba kurekebisha idadi ile ambayo imeandikwa kwenye taarifa ambayo nimeisambaza, fedha zilizokwishatolewa kama mkopo wa kipindi hicho ni jumla ya shilingi trilioni 1,184,490,554,983.58.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kati ya shilingi trilioni 1,184,490,554,983.58 zilizokopeshwa, mikopo ambayo haijaiva ni trilioni 1, 023,759,668,644.50 na mikopo ambayo imeiva kwa ajili ya kurejeshwa kutoka kwa walengwa jumla yao 110,529 walionufaika mikopo hiyo iliyoiva ni shilingi bilioni 160,730,886,339.

Mheshimiwa Spika, kati ya shilingi hizo zilizoiva bilioni 160,730, 886,339 za mikopo iliyoiva, mikupuo ama *installments* inayopaswa kuwa imerejeshwa ni shilingi bilioni 43,558,020,863.33 ambapo hadi kufikia mwezi Desemba mwaka jana 2012, fedha ambazo zimerejeshwa jumla yake ni shilingi bilioni 28,010,000,000.43 sawa na 64% ya mikupuo ambayo ilitakiwa iwe imerejeshwa. Asilimia 64 ya fedha ambayo ilitakiwa iwe imerejeshwa kwa mikupuo imerejeshwa.

Mheshimiwa Spika, pesa nyingi haijafikia muda wake wa kurejeshwa hivi sasa kwa hivyo trilioni na mabilioni yale ambayo yametolewa bado hayajaiva kuweza kurejeshwa. Ufinyu wa fedha zilizorejeshwa hadi sasa umechangiwa kwa kiasi kikubwa na baadhi ya wanufaika kukosa uzalendo wa kurudisha mikopo kwa hiari baada ya kunufaika. Sababu nyingine ni kwa wanufaika wa mikopo hiyo pamoja na jamii kwa ujumla kuchukulia kuwa mkopo ni ruzuku kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Mwigulu L.N.Madelu katika wasilisho la hoja yake.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba mikopo iliyoiva inarejeshwa, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imeanzisha mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na ifuatayo: kuelimisha wadaiwa, kuelimisha waajiri na wananchi kwa ujumla juu ya dhana ya urejeshwaji wa mikopo kwa njia ya matangazo katika vyombo vya habari. Mkakati mwingine ni kuendelea kutumia taarifa za watumishi walioajiriwa Serikalini kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuwatambua wadaiwa mahali walipo na kuwatumia mawakala wa kukusanya fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazofanywa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, mwitikio wa kurejesha mikopo bado sio wa kuridhisha. Napenda nichukue fursa hii kuwasihi Waheshimiwa Wabunge na wananchi kutoa ushirikiano katika urejeshwaji wa mikopo iliyotolewa kwa sababu ndiyo msingi mkuu wa kuifanya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iwe endelevu. Tunaweza kuongeza fedha kwa njia mbalimbali lakini kama wakopeshwaji hawatarejesha mikopo yao na kurejesha kwa wakati azma ya kufanya utaratibu huu kuwa endelevu haitoweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu kuwa uwezo wa Serikali kugharimia mikopo ya wanafunzi unazidi kupungua kulingana na ongezeko kubwa la wanafunzi wa kidato cha sita na wengine wenye sifa linganifu ambao ndiyo wadau wakuu wa mikopo inayotolewa na Serikali. Kwa mfano, kati ya waombaji wapya 45,788 katika mwaka huu wa masomo 2012/2013 ni wanafunzi 30,144 ndiyo waliopangiwa mikopo.

Mheshimiwa Spika, aidha, uchambuzi unaonyesha kuwa mbali na ongezeko la wahitaji wa mikopo, wengi kati yao wana uwezo mdogo wa kuchangia elimu ya juu kwa mwaka. Asilimia 72.17 ya waliopangiwa mikopo kwa mwaka huu wa masomo 2012/2013, wana uwezo wa kuchangia chini ya shilingi 500,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia changamoto za kuongezeka kwa idadi ya wahitaji na uwezo mdogo wa waombaji, ni wazi kuwa uwezo wa Serikali kugharimia mikopo ya wanafunzi utapungua na idadi kubwa ya wahitaji wanaweza kukosa fursa hii adimu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali iliunda Kamati na Tume mbalimbali zilizotoa ushauri jinsi ya kuwa na mfumo endelevu wa kugharimia elimu ya juu. Ushauri huu upo katika ripoti zifuatazo:-

(i) *Financial Sustainability of Higher Education in Tanzania* ya mwaka 1998;

(ii) *Review of Financial Sustainability in Financing Higher Education* in Tanzania ya mwaka 2005;

(iii) Ripoti ya Kamati Maalum ya kushughulikia matatizo ya utekelezaji wa Sera ya Uchangiaji Elimu ya Juu ya mwaka 2009;

(iv) *Financing of Higher Education through Students' Loans Scheme: Proposals for Sustaining Expansion in Higher Education* ya mwaka 2010; na

(v) Ripoti ya Tume ya Rais ya kutayarisha Mfumo Mpya wa kugharimia na kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Kamati na Tume hizi ambazo zimefanya kazi muda mbalimbali, zilitoa mapendekezo mbalimbali kuhusu mfumo endelevu wa kugharimia elimu ya juu ikiwa ni pamoja na ifuatayo:-

(i) Kuanzisha Mfuko Maalum wa Dhamana ama *Endownment Trust Fund;*

(ii) Kuanzisha Mfuko wa Elimu kama ulivyo mfuko wa barabara;

(iii) Kushirikisha Taasisi mbalimbali za Umma na binafsi ili zichangie sehemu ya pato lao kugharimia elimu ya juu;

(iv) Wanafunzi kukopa moja kwa moja kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na mabenki; na

(v) Serikali kuuza Hatifungani ya elimu ama education note ili kupata fedha za kukopesha wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, ili kubaini njia endelevu ya kugharamia elimu ya juu mwezi wa Novemba, 2011 Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi iliunda Kamati ya Wataalam ambayo ilianza kazi Januari, 2012 kuchambua kwa kina mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na Kamati na Tume zilizotajwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu ulizingatia urahisi wa utekelezaji wa kila pendekezo, faida zilizokuwepo na changamoto zilizopo katika kutekeleza mapendekezo hayo. Kutokana na uchambuzi huo, Kamati imetoa mapendekezo ya njia bora na endelevu ya kugharamia elimu ya juu kwa kuzingatia vigezo vya kiasi cha fedha kinachoweza kupatikana, faida ya mfumo huo na changamoto na uendelevu wa mfumo unaolengwa au unaokusudiwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mifumo au njia zilizopendekezwa na Kamati hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mifuko ya Hifadhi za Jamii na Taasisi za Kifedha hasa mabenki kukopesha wanafunzi wa elimu ya juu. Hapa inapendekezwa kwamba Mifuko ya Hifadhi za Jamii ibuni na kutoa kwa wanachama wao fao la elimu ya juu au mikopo kwa wanachama wao kwa ajili ya faida za wanachama na watu wengine.

Vile vile Taasisi za Kifedha zitenge fungu ambalo linaweza kukopeshwa kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa kuzingatia masharti ambayo hayatahatarisha uendelevu wa fungu linaloanzishwa. Fungu hili la kukopeshwa linaweza kuongezwa kwa kupata michango kutoka kwenye vyanzo vingine vya fedha kama hati fungani ya elimu na maeneo mengine ya Serikali ambayo yanaweza kuzalisha fedha za ziada.

(ii) Pendekezo ni kuwa, Serikali kuuza hatifungani ya elimu ama *education bond* ili kupata fedha za kukopesha wanafunzi. Katika mfumo huu inapendekeza kuuza hatifungani ya elimu ya kipindi kitakachokubalika na soko ili kupata fedha ambazo zitaingizwa katika fungu kwa ajili ya kukopesha wanafunzi wa elimu ya juu. Kiasi kitakachouzwa kitategemea vigezo vinavyowekwa kuweza kupima uwezo wa Serikali kukopa, lakini inakisiwa kwamba fungu lisilozidi shilingi bilioni 100 lingeweza kupatikana.

(iii) Mfumo unaopendekezwa na Kamati ni kuanzisha Mfuko wa Elimu kama ilivyo Mfuko wa Barabara. Katika mfumo huu inapendekezwa kuanzishwa Mfuko wa Elimu kwa kutumia mfano wa Mfuko wa Barabara. Ingawa vyanzo vya fedha vya kuanzisha Mfuko huu si vingi, inapendekezwa ianzishwe tozo kwa wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu kama chanzo cha awali.

Vile vile Serikali itazame uwezekano wa kupitia upya maeneo mengine ambayo yanaonekana kuwa na mapato makubwa yanayoweza kuingizwa kwenye fungu la mapato ya Taifa na kuchangia katika kukuza Mfuko wa Elimu. Maeneo haya ni pamoja na mapato yanayokusanywa na taasisi za Serikali kama vile *EWURA* na *TCRA* na taasisi nyingine kama hizi.

(iv) Inapendekezwa na Kamati kutoza riba itakayoweza kulinda thamani ya fedha na kuondoa dhana kuwa mkopo unaotolewa ni ruzuku. Kamati inapendekeza kwamba, riba itozwe kwa kiwango cha soko ambacho Serikali ingelipa kama ingekopa sokoni kwa kipindi chote cha mkopo. Riba ya kiwango cha soko itatoa uwiano mzuri kati ya njia zote za kugharimia elimu ya juu na itaondoa msongamano au mlundikano wa wakopaji wanaojitokeza kwa sababu ya mvuto wa mkopo usio na riba au mkopo wa riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine yaliyopendekezwa na Kamati hii ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuwepo na ukomo wa idadi ya wakopaji na maoteo yake kwa miaka mitano;

(ii) Kuweka ukomo wa kiwango cha mkopo kwa mwanafunzi kwa kila fani kwa sasa gharama ya kumsomesha mwanafunzi inatofautiana katika kila taasisi;

(iii) Kuwa na mfumo wa urejeshwaji wa mikopo ambao utahusisha kikamilifu waajiri, taasisi za fedha na mamlaka ya ukusaji wa kodi; na

(iv) Kuwa na utaratibu wa bima ya mikopo kwa ajili ya kufidia deni endapo mkopaji atafariki kabla ya kurejesha mkopo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na Kamati iliyoundwa na Wizara yangu yanafanana kimantiki na mapendekezo yaliyotolewa na mtoa hoja. Kamati hii bado inaendelea na kazi kwa kukutana sasa na wale walengwa moja kwa moja kama Mifuko ya Jamii, mabenki na kadhalika ili sasa kuweza kukamilisha mapendekezo hayo ambayo yatatoa mfumo wa fedha za kugharimia elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Waheshimiwa Wabunge, kuwa jukumu la kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya juu ni letu sote na kwamba hoja hii inalenga kuboresha utoaji wa mikopo nchini. Aidha naomba nimpongeze Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi. Kwa kuleta hoja inayochangia katika azma ya kutafuta njia mbadala za kuchangia ugharimiaji wa elimu ya juu hapa nchini. *(Makofi)*

KWA KUWA, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, iliunda Kamati ya Wataalam ya kubaini na kupendekeza vyanzo mbadala ya kugharimia elimu ya juu na kwa kuwa vyanzo vinavyopendekezwa na Kamati hiyo ni pamoja na vile vinavyopendekezwa na mtoa hoja ambavyo vinafanya utoaji wa mikopo kwa elimu ya juu uwe endelevu;

NA KWA KUWA, kwa sasa kuna mchakato wa kuhuisha Sheria Namba Nane ya mwaka 2001 ya Mfuko wa Elimu ama *Education Fund Act*, 2001 ambao moja ya majukumu yake makuu ni kutafuta mapato ya kutosha na endelevu kwa ajili ya Mfuko wa Elimu na kuishauri Serikali juu ya vyanzo vingine vya uhakika vya mapato; na

NA KWA KUWA, mapendekezo takriban yote yaliyotolewa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi, yamo katika mapendekezo ya Kamati ya wataalam.

HIVYO BASI, kwa mujibu wa Kanuni ndogo (1)(a) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la mwaka 2007, naomba kutoa hoja ya mabadiliko ya hoja binafsi ya Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuondoa maneno ilete Muswada wa Sheria ama Serikali ilete Muswada wa Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Elimu ya Juu katika Mkutano ujao wa Kumi wa Bunge pamoja na mambo mengine, sheria itakayoweka taratibu mbalimbali zitakazowezesha upatikanaji wa fedha kutoka kwa wadau wa elimu ya juu, kodi, tozo na kwenye taasisi nyingine kugharamia elimu ya juu kwa kuanzisha Mfuko wa Elimu ya juu yaani *The Higher Education Fund* na badala yake kuingiza maneno yafuatayo:

"Ilete Muswada wa marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu, Namba Nane ya mwaka 2001, *The Education Fund Act, No*. 8 *of* 2001, sura 412 na/au Sheria Namba Tisa ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, *The Higher Education Students Loans Board*, Sura 178 ili kujumuisha mapendekezo ya Kamati ya Wizara na yale ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu vyanzo mbadala vya kugharamia elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni zetu hoja inaweza kufanyiwa mabadiliko na mabadiliko haya ni lazima yaweze kuungwa mkono na kabla hatujaanza kujadili hoja ya Nchemba kwanza tukubaliane… Mheshimiwa Nchemba, unasema nini?

MHE. MWIGULU L.N. MADELU: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vizuri na kukubaliana kimantiki kwamba lengo ni kuondokana na mfumo uliopo. Sasa kwa utaratibu wowote ambao utatuwezesha kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato na utakaotuwezesha kuondokana na adha hii ya wanafunzi kutokupata fedha ya kujitosheleza na kwa wakati. Mapendekezo yoyote ambayo yatatupa mfumo ama kama niliyopendekeza ama na muunganiko wa vyanzo vingine, maadam unatupatia vyanzo vya uhakika cha kugharamia elimu ya juu, mimi nitakuwa radhi nayo na nilileta kama *skeleton* ili tuweze kupata na mawazo ya kutokea maeneo mengine mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo moja tu ambalo nimeona, mimi niliweka neno kwa haraka inavyowezekana, hata ukiangalia kwenye maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuna Tume zingine za Tangu mwaka 1998. Kwa hiyo, liangaliwe hili kwa sababu ni kweli wanafunzi wa vyuo vikuu wanapata shida sana, lakini nakubaliana kimantiki kwamba tuna-*converge* kupata mfumo ambao utasaidia elimu juu kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema kwanza itabidi tuamue hoja hii ya pili. Wanaofikiria kwamba marekebisho yaliyoletwa na Serikali yakubalike dhidi ya hoja iliyoletwa na Nchemba kwa maana ya Azimio.

Sasa naomba nirudie tena kwa utaratibu wetu ni kwamba, kama hoja imetolewa na mtu hata kama na Serikali halafu Mbunge au mtu mwingine akaleta mabadiliko juu ya hoja ile, tunajadili kwanza mabadiliko yale kama tukiyakubali mabadiliko yaliyoletwa, basi tujue hoja iliyoletwa inakuwa imefanyiwa mabadiliko au imekuwa *amended* kama yatakataliwa basi tunarudi na hoja ile ya asili.

Sasa mimi ninaomba niwahoji kuhusu mapendekezo yaliyoletwa na hoja na Serikali kwamba Serikali ilete Muswada wa marekebisho ya sheria ya mfuko wa elimu namba nane ya mwaka 2001 the education fund act no. 2001 sura ya 412 na au sheria namba 9 ya bodi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu juu *The Higher Education Students Loan Board*, Sura ya 178 ili kujumuisha mapendekezo ya Kamati ya Wizara na yale ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu vyanzo mbadala vya kugharamia elimu ya juu. Hii ndiyo hoja iliyoletewa mabadiliko.

Hoja ya Mheshimiwa Nchemba yeye alikuwa anasema, naomba Bunge lako Tukufu liazimie kuitaka Serikali kwa haraka inavyowezekana ilete Muswada wa Sheria wa Kuanzisha Mfuko wa Elimu ya Juu katika Mkutano ujao wa Kumi wa Bunge. Sasa hata mimi mwenyewe naifuta kwa sababu Mkutano wenyewe ndiyo huu, haiwezekani wakaileta safari hii. Kwa hiyo, hata mimi mwenyewe naondoa, pamoja na mambo mengine sheria itakayoweka taratibu mbalimbali zitakazowezesha upatikanaji wa fedha kutoka kwa wadau wa elimu ya juu, kodi, tozo na kwenye taasisi nyinginezo kugharamia elimu ya juu kwa kuanzisha Mfuko wa Elimu ya Juu yaani The *Higher Education Fund*.

Kwa hiyo, kuna haya marekebisho ya aina mbili. Sasa nauliza wale wanaofikiria *version* iliyoletwa na Serikali ikubalike, nitawahoji hivyo na wale wanaofikiria *version* ile ya Mheshimiwa Mbunge iendelee, pia mnaweza kupiga kutokukubaliana na hoja ya Waziri, lakini mkiangalia zote mbili kusudio lake ni kuongeza fedha, sasa na kama yoyote yule ataleta marekebisho ya sheria hiyo, hoja lazima ijadiliwe na wananchi pamoja na sisi *public hearing*. Hata hii ya Nchemba ikikubaliwa nayo pia itabidi iletwe kwa utaratibu wa kawaida wa Muswada wa kawaida. Sasa nawahoji kuhusu *version* iliyoletwa na Serikali.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Ukweli ni kwamba, hakuna tofauti kubwa huyu alipata Muswada kamili, lakini huyu anafikiria kwamba pengine tungeweza kuunganisha na hii na tukapata hii. kwa hiyo, baada ya kusema hivyo naruhusu kuendelea kujadili. Wa kwanza kabisa atakayejadili, wengine wameomba siwaoni hata kama walikuwa wa kwanza kwanza, Mheshimiwa Margreth Sitta atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nijadili hoja iliyoko mbele iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ya kutaka chombo maalum kiundwe kwa ajili ya kushughulikia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kwanza naipongeza Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa kuongeza shule nyingi nchini, bila kuwa na shule nyingi nchini tusingekuwa tunajadili mkopo hapa. Sasa hivi wanafunzi tunao wengi na wanaotaka kuendelea na elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimpongeze Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa kuleta hoja hii wakati muafaka yaani kwa neno la Kiingereza *timely,* kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii mimi nikiwa Mwenyekiti, watakubaliana nami kwamba tumeshakuwa na vikao zaidi ya vitatu na Serikali na Bodi na wanafunzi wenyewe hasa viongozi wao, hapa Dodoma na Dar es Salaam tukijadili matatizo tunayokabiliana nayo katika kukadiria mikopo ambayo wanastahili kupata wanafunzi. Kwa hiyo, nakupongeza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa kuleta hoja hii kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo limekuwa likitupa tatizo kubwa sana sisi wa Kamati ya Huduma za Jamii tunapojadili na Bodi ya Mikopo ni vigezo vinavyotumika. Kumekuwa na matatizo mengi sana katika kuangalia nani apate kiasi gani, jambo linaloleta malalamiko mengi sana kwa upande wa wanafunzi wanaopata mikopo hii. Wengine wameongeza uwongo ili wapate, wengine wamesema ukweli na wakakosa. Kwa hiyo, vigezo vimekuwa na matatizo mengi sana na kwa mfano, Serikali imeamua kwamba iwe na vipaumbele ili iwape asilimia wanafunzi wanaochukua masomo ya Sayansi, Udaktari, Elimu na mambo kama hayo. Lakini kwa wanafunzi ambao wamepitia shule hasa hizi za kata ambazo zilianzishwa kwa nia nzuri za kutoa fursa kwa wengine lakini hawakuwa na maabara na wakati mwingine ni ukweli kwamba hawakuwa na walimu wa kutosha, kwa hiyo, wameshindwa kukidhi matakwa ya kupata mkopo kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, lakini hii imetoa hisia za ubaguzi kwamba, wote ni Watanzania, wao hawakupitia shule nzuri na wameshindwa kupata vigezo vya kupata masomo ya sayansi, kwa hiyo wamekosa kupata asilimia mia moja. Kwa hiyo, napongeza sana wazo hili la kuwa na Mfuko ambao utatoa sasa asilimia mia moja kwa yeyote anayetaka; anayetaka sheria, kutokana na taaluma aliyonayo, itatusaidia sana. Kwa msingi huo, itasaidia watoto wanaotoka kwenye familia duni ambao hawakupata nafasi ya kuingia katika vigezo vya kupata asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mwigulu, kwa sababu tukiwa na chombo maalum na kikapewa meno hata katika kurejesha mikopo itakuwa rahisi kwa sababu tatizo tulilonalo sasa hivi waliokopa hawalipi. Kwa hiyo, kikiwa chombo maalum kinatoa asilimia mia lakini kina meno ya kukusanya, fedha zitapatikana na kwa msingi huo wanafunzi wengi watanufaika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyanzo vya mapato, nashukuru kwamba Serikali na mtoa hoja kwa kiasi fulani wanafanana kwamba kutakuwa na vyanzo mbalimbali vya fedha. Ombi langu mimi ni kwamba, wale watakaopata nafasi ya kuchangia humu Bungeni basi watoe

maoni mengi zaidi kuhusu vyanzo mbalimbali vya mapato ili kweli huu Mfuko wa Elimu uwe na fedha za kutosha ili wanafunzi wote wenye sifa waweze kuendelea na elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kwamba, kulikuwa na wakati Serikali ilikubali kwamba itatoa asilimia mbili kwa ajili ya Mfuko wa Elimu, lakini kadiri siku zinavyozidi kwenda ahadi ya Serikali inazidi kupungua. Ilianza vizuri kwa asilimia 0.45, lakini imeendelea kupungua mpaka sasa hivi michango ya Serikali ni asilimia 0.075, jambo ambalo linasikitisha. Tunaamini kwamba, Serikali ikitimiza ahadi yake ya kutoa asilimia mbili ya mapato yote kwa ajili ya Mfuko wa Elimu, basi utasaidia kuwa chanzo kikubwa cha mapato, kwa hiyo, wanafunzi wengi watasoma taaluma wanazotaka bila ubaguzi. Kwa msingi huo itawasaidia wanafunzi wanaotoka katika familia duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu sheria, naipongeza Serikali kwa jambo moja kwamba turekebishe sheria zilizopo, badala ya ulivyopendekeza mtoa hoja kwamba kuwe na sheria maalum. Lakini kwa Serikali kukubali kwamba, tunaweza kufanya mabadiliko yaani *amendment* katika Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001 na kufanyia pia marekebisho au *amendment* Sheria iliyoanzisha Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya marekebisho hayo, huu Mfuko unaweza kuanzishwa na kuwekewa taratibu za kufanya kazi ikiwa ni pamoja na vyanzo vya mapato kuliko kuanza na Sheria mpya. Kwa sababu sheria mpya itachukua muda mwingi, Serikali ilivyopendekeza, kuleta mabadiliko, amoja na kwamba yatajadiliwa, lakini yatachukua muda mfupi. Waheshimiwa Wabunge, wanafunzi wanapata matatizo makubwa sana ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ichukue hatua za haraka, ilete kwetu yale marekebisho, tuwaombe Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono yale marekebisho, ili Mfuko uanze wanafunzi wetu wanateseka kwa kweli, hasa wanaotoka kwenye familia duni, waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ameleta hoja yake kwa wakati muafaka, watoto wetu wanateseka hasa wanaotoka kwenye familia duni, hii hoja yake ikifanyiwa kazi, watoto wengi watapata nafasi. Kwa msingi hiyo, wanafunzi wengi wanaotoka kwenye shule za Kata, tulizoziongeza kwa wingi, watanufaika wengi, watapata Elimu ya Juu na sisi tunafahamu hakuna maendeleo kama hakuna maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Nilimwita Mheshimiwa Margareth S. Sitta, kwa sababu hili suala liko katika eneo lake. Sasa mkiangalia *nature* ya hoja hapo, tusianze kujadili Muswada ambao haupo. Hapa tunaomba, kama tunakubaliana, tuulete Muswada, basi tuiagize Serikali ilete hiyo hoja, ndiyo tuweze kuweka nyama, kuweka mifupa na kadhalika. Tusije tukaanza kujadili maudhui ambayo hayapo katika hoja hii.

Hoja hii inatutaka sisi, tunakubali kwamba Serikali ilete Muswada au marekebisho ya Mfuko huo wa Elimu. Sasa ni lini ilete, au *soon* ilete, ndiyo mambo hayo tunatakiwa tufanye. Sasa itakapoletwa ndiyo tutaongeza nyama na mifupa yote, tunayofikiria na ujuzi tulionao, kuweka katika Muswada, sio katika huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa David E. Silinde atafuatiwa na Mheshimiwa Manyanya.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nichangie hoja ya kukubali kuletwa kwa Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, niseme kwa maana ya hoja ya kuleta mabadiliko, tunaafiki, lakini hatuwezi tu kuafiki hoja bila kuweka maudhui ndani yake. Niwashukuru sana, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Shukuru J. Kawambwa na nimshukuru vile vile Mheshimiwa Mwigulu L. Nchemba**,** naamini kabisa kabla hajaleta hoja yake Bungeni, alipitia Ilani ya CHADEMA. Kwa sababu, katika uchaguzi wa mwaka 2010, Ilani ya CHADEMA, ukisoma ukurasa wa 16 na ukurasa wa 18, imeeleza wazi kabisa kwamba, mara tutakapoingia madarakani, tutaanziasha Mfuko wa Elimu. Tumeeleza vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, moja tumeeleza kuna *Uhuru Scholarship Fund*, Mfuko Maalum kabisa. Tumeeleza wazi kwamba, namna gani tutavunja Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa sababu ya utendaji mbovu. Tumeeleza wazi kwani sisi tusingependa sana kuwa na maneno mengi, tungependa vile vile kwamba, hiki kiwe ni vigezo vya kwenu mnapokuja Bunge linalofuatia. Hiyo iwe ni moja ya vigezo, kwa sababu hapa ndipo utakapopata majibu kamili ya Watanzania, namna gani elimu iendeshwe.

Mheshimiwa Spika, wakati sheria inakwenda kubadilishwa ambayo tunaiomba ije na tuibadilishe kweli kweli, naomba baadhi ya mambo yazingatiwe:-

Moja, Ripoti ya Tume ya Rais iliyokuwa chini ya *Professor* Makenya Maboko, iletwe Bungeni tuijadili, tujue maazimio yake yalikuwaje. Kwa sababu hatuwezi kuja kujadili mabadiliko ya sheria, bila kufahamu yaliyotolewa kwenye ile Tume. Kwa sababu imekuwa ni siri, hakuna mtu anayejua walipendekeza nini au maazimio yake yalikuwa ni nini. Kwa hiyo, tunaomba haya yaletwe Bungeni tuyajadili, ili baadaye tuweze kupata mustakabali mzuri na tuweze kutengeneza sheria ambayo itawasaidia wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, wakati wanaleta marekebisho hayo, kabla ya marekebisho, Serikali imekiri kwamba mfumo ulikuwa mbovu na ndiyo uliokuwa unasasabisha migogoro, ilikuwa inaleta migomo Vyuoni. Kuna wanafunzi mpaka sasa wamesimamishwa kutokana na kugomea mfumo mbovu wa Sheria za Bodi ya Mikopo. Kwa hiyo, wanapoleta sheria, wakijua kwamba hiyo sheria ni mbovu, basi na wanafunzi wenyewe wawe wamerudishwa Vyuoni. Ili tunapojadili sheria mbovu, wanafunzi waliokuwa wanapinga sheria mbovu, warudishwe shuleni, kwani wamefukuzwa bila ya kuwatendea haki. Kwa sababu walipinga sheria ambayo Serikali yenyewe leo imekiri, hivyo hilo lifanyike. Tusije tukajadili kitu ambacho tunajua kimewanyonga Watanzania, halafu tunakirekebisha wakati, hao Watanzania tuliowanyonga wanaendelea kubaki nje. Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, tungependa wazingatie, mwaka 2007/08 tukiwa wanafunzi Vyuo Vikuu, moja ya mapendekezo, kulikuwepo na *report* ya wanafunzi wa Elimu ya Juu, *TAHLISO* ya wakati huo. Yenyewe ilipendekeza namna gani tunaweza tukaanziasha Mfuko wa Elimu ya Juu, ambao bila kujadili mambo mengine ungesaidia Tanzania. Namwomba Waziri azingatie hilo, kwa sababu sijaiona hapa, nimeangalia hapa, sijaiona kabisa, hajaipitia.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mambo iliyopendekeza, ilikuwa inapendekeza, kuweka tozo kwenye kila bidhaa, kama shilingi moja. Hiyo ingechangia kwani kila Mtanzania angechangia na Serikali isingepata shida ya kupata chanzo cha fedha, kuliko huu utaratibu wa sasa wa kuleta tozo kwa wanafunzi waliohitimu Vyuo Vikuu. Kwa sababu sasa, unamaliza Chuo na inakuwa kama ni adhabu, wakati tuna vyanzo mbalimbali. Hivyo, hili liwekwe wazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo lizingatiwe, usilete sheria na riba, hatuwezi kwenda. Kwa sababu elimu siyo biashara, kwa kweli tutawashangaza watu. Nchi yetu ina vyanzo vingi, tuna madini, tuna gesi ambayo inaleta migogoro kila mahali. Tuna Maliasili na

Utalii, tuna vitu vingi ambavyo tunaweza tukatengeneza, Mfuko Maalum na vyanzo ambavyo vinaweza vikasaidia Taifa na wote tukafaidika kuliko kuweka riba, riba maana yake sasa tumefanya elimu ni biashara kama zilivyo biashara nyingine.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama kuna Mtanzania ambaye anaweza akakubaliana na suala la riba na ninyi wote mnajua. Kipindi cha Mwalimu Nyerere, watu wengi waliokuwepo kipindi hicho na waliosoma akina Mheshimiwa Samwel Sitta, wao tunakumbuka walikuwa wanagoma kwa kupinga kupewa mikate na siagi, nakumbuka Mwalimu aliwatandika viboko. Lakini wanafunzi wa sasa wanagoma kwa kupinga Sheria mbovu, zikiwemo hizi riba.

Mheshimiwa Spika, sasa tusingependa vile viboko vya Mwalimu Nyerere, vya watu kupinga mikate kukosa siagi vikajirudia leo katika riba. Kwa sababu Watanzania watatuchapa viboko kwa kuwawekea riba ambayo itawakandamiza zaidi watoto wa maskini. Hili halitawezekana kwani mpaka sasa bado tunataka kutengeneza mfumo bora wa elimu wa kuwasaidia Watanzania wengi. Wanafunzi wengi wa Elimu ya Juu wanomaliza hawana uhakika wa kupata ajira na hili ndiyo limekuwa dimbwi sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa hivi tunalalamika kukosa elimu, kuna Walimu zaidi ya elfu 28, wako nje hawajaajiriwa na tunalalamika shule zetu hazina Walimu. Tuje na sheria itakayosaidia kupata wanafunzi wengi, lakini vile vile yenye uhakika wa wanafunzi wanaomaliza vyuo vikuu kupata ajira baada ya kumaliza.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naweka maudhui kidogo katika sheria inayokuja, kwa hiyo na mimi nakubaliana na Sheria ya Marekebisho iletwe katika Bunge linalofuatia. *(Makofi)*

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia, lakini hususan kuunga mkono marekebisho ya sheria yanayotaka kuletwa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana ndugu yetu, Mheshimiwa Mwigilu L. Nchemba, lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Dkt. Shukuru J. Kawambwa, kwa kukubaliana na hoja ya msingi.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi, binafsi nakwazwa sana na Bunge letu, tunapokuwa na hoja ya msingi, halafu tunapoanza kuipeleka katika sura ya kivyama, unakuta tunahama katika *logic* yetu ya kujadili ile hoja ya msingi na matokeo yake kila mtu anajaribu kuvutia kwenye Chama chake na mwisho tunakosa kupata ile mantinki muhimu tunayohitaji kwa mustakabali wa watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba, mawazo yote mazuri yanayolenga kuboresha hatma ya elimu ya juu na maeneo mengine, itoke Kwenye Chama Tawala, itoke kwenye Chama cha Upinzani ili mradi hoja hiyo ni ya msingi, ichukuliwe kwa manufaa ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pamoja na kuangalia Mfuko huu katika sura ya elimu. Kwa bahati nzuri imekuwa ni rahisi kwangu kuunga mkono kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Dkt. Shukuru J. Kawambwa kwa hoja yake, hasa baada ya kuona kwamba, kumbe tayari hiyo sheria ipo, kwa hiyo hatuna haja ya kuanzisha sheria nyingine badala yake tunaweza tukafanya marekebisho. Isipokuwa tu, tunachojifunza ni ule umuhimu wetu wa kufanya kazi, kuharakisha maamuzi, kwa sababu kama hizi Kamati nyingine zilishatoa haya mapendekezo, halafu yanakaa mpaka tena anajitokeza Mbunge kuyaombea muafaka maalum, hiyo inakuwa haipendezi sana.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Kamati tunazokuwa tumeziunda, zikishakuwa zimefikia ushauri, basi ushauri huo tuutekeleze kwa wakati ili kuepusha manung'uniko na malalamiko yasiyo ya lazima kutoka kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hilo liende zaidi hata katika nyanja nyingine. Kwa sasa hivi tunawazungumzia hawa wa Elimu ya juu, lakini tunakopata wanafunzi wa Elimu ya juu, ni kutoka Vijijini. Nilikuwa naangalia *Employment rate* yetu, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga amenipa *data,* ni kwamba unakuta asilimia kubwa ya Watanzania, wamejiajiri kwenye kilimo, ni 45%, ni kama watu 11,250,000. Hao ndiyo wenye watoto na hao ndiyo wanaosoma katika zile shule ambazo sasa hivi ziko kwenye Kata na wakati mwingine mazingira yake ya kusoma bado yako chini. Lakini hao hao ndiyo wanaokuwa na pasi zile zisizowawezesha kuingia katika *Higher Education* na badala yake wanakuwa wamepata katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukienda maeneo ya vijijini tunakosa kupata wafanyakazi kama Wahudumu wa Afya, Walimu na watumishi wa sekta nyingine. Inapotokea ajira unakuta kwamba wanaobahatika ni wale ambao walitoka maeneo yenye mazingira mazuri. Unakuta hata pengine kumpeleka mtoto kwenye Chuo cha *Nursing* na ili aweze kurudi kuhudumia maeneo anayotoka, inakuwa ni vigumu. Kwa hiyo, unakuta Vituo vya Afya ambavyo viko huko vijijini, havina wahudumu kwa sababu wanafunzi ambao wanatoka maeneo yale hawakuweza kupata mikopo au namna ya kuwawezesha wao kusoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sababu Mfuko huu kwa kadri alivyozungumza unaitwa *Education Fund Act*, hii iliyoletwa hapa, basi iangalie katika mazingira ambayo yanahitaji watumishi wa muhimu katika maeneo hasa ya Vijijini, kwa sababu hao wananchi ambao ndiyo asilimia nyingi ni wakulima ndiyo hao wenye watoto ambao wanapasi ambazo zingewezesha kwenda katika fani nyingine, lakini hawana uwezo wa kuwasomesha.

Mheshimiwa Spika, nasema hayo kwa uzoefu mkubwa ninaoupata sasa hivi katika dawati langu. Unakuta watoto wanakuja wanahitaji walipiwe Chuo cha *Nursing*, anahitaji alipiwe labda amepata kozi ya kilimo. Wananchi wanasema kwamba, tuangalie namna ya kuweza kuwapata watu ambao wanasomea maeneo ya kilimo kama ambavyo fursa kubwa ya ajira ipo katika maeneo hayo. Kwa hiyo, Mfuko huu utakapokuja, Sheria hii itakapoletwa, iangalie kwa upana zaidi namna ya kufikia hata makundi hayo. Namna ya kupata pesa, kama ulivyozungumza Mheshimiwa tuchangie wakati huo.

Mheshimiwa Spika, lakini tu niweze kusema kwamba, kama elimu tumeona kwamba ni janga mojawapo kubwa katika maradhi makuu ya nchi, tatizo la ujinga ni jambo ambalo linatakiwa lifanyiwe kazi kwa kadri inavyowezekana. Kwa hali hiyo basi, kama elimu ndiyo ajenda yetu namba moja, iwe ni *compulsory,* iwe ni lazima kwa kila mtu kuchangia Mfuko huu wa Elimu, kwa sababu tutakuwa na vitambulisho vya Taifa, iwe ni lazima kila mtu kuchangia. Hii hoja ya kusema kila mtu ni maskini, akashindwa kuchangia hata kidogo, hiyo ifikie mahali, tusiubebee umaskini mbeleko.

Mheshimiwa Spika, mtu mzima ambaye ana viungo vilivyotimia hatusemi kwamba atakuwa ni tajiri, lakini angalau atakuwa na uwezo wa kuchangia hata kidogo. Haiwezekani useme kwamba una watoto wako watano au sita, halafu unasema mimi sina uwezo moja kwa moja. Kwa hiyo tutatumia fursa zote, iwe ni kupitia mazao yetu, iwe ni kupitia vyeti vyetu, vyeti vya kuzaliwa, lakini mtu aweze kuchangia moja kwa moja kwenye Mfuko huu wa Elimu ili kuondokana na Taifa ambalo linakua na watu ambao hawana elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, mimi naisubiri hiyo sheria kwa sababu tuna nafasi pia ya kupeleka michango yetu kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Shukuru J. Kawambwa. Wakati anaileta, basi niombe tu kwa wadau wote wa elimu, ni wakati muafaka wa kila mtu mwenye wazo jema kulipeleka, badala ya kulalamika sheria iliyotungwa ni mbaya. Naamini Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Shukuru J. Kawambwa, atapokea na ataweza kuweka vizuri katika sheria ambayo italetwa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mwigulu L. Nchemba, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Shukuru J. Kawambwa, lakini kubwa zaidi nakushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe mawazo yangu. Naomba niwapongeze wataalam wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, pamoja na mleta hoja ndugu yetu Mheshimiwa Mwigulu L. Nchemba kuhusu suala hili la mkopo katika Vyuo vya Elimu ya Juu, kwani huku ni sehemu ambako kuna kero kubwa kuliko kero zote ndani ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, suala hili limekuja wakati muafaka, nikirejea katika vikao mbali mbali ambavyo tumekaa ndani ya Kamati ya Huduma za Jamii, na-*declare interest* kidogo, mimi ni mjumbe katika Kamati ya Huduma ya Jamii, suala hili tumelipigia kelele muda mrefu, lakini nashukuru Wizara ya Elimu wamechukua mawazo ambayo tumetoa tangu mwaka 2010. Nasema hivyo kwa sababu nchi yoyote ile ambayo inahitaji kuendelea, kipaumbele namba moja ni elimu, kipaumbele namba mbili ni elimu na kipaumbele namba tatu ni elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa njia hii narejea miaka ile ya tisini nikiwa ni kiongozi wa wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es salaam, suala hili tulikwenda mara kadhaa Ikulu, tukishauri wakati wa kuchangia ni vizuri kufanya utafiti wa kina ili kusudi wale ambao hawana uwezo na wao waweze kupata fursa ya kupata elimu. Suala hili katika *mile stone* hiyo bado haijakaa vizuri. Wenzetu Kenya wao wanaangalia vipi? Wanatoa *flat rate.*

Mheshimiwa Spika, jaribu kuangalia katika Afrika, Tanzania ndiyo tunaongoza kwa kutoa mikopo ikifuatiwa na Afrika ya Kusini ambayo nao ni *flat rate* waliyopanga kama ni bilioni 68 ilivyokuwa bajeti ya mwaka jana. Mwaka juzi Kenya walikuwa na bilioni 29. Kwa hiyo, Serikali inatenga *flat rate.* Hii inatoa fursa kwa waombaji wote ambao wana sifa za kwenda Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, ukija kuangalia Sheria ya Bodi ya Mkopo ya 2004, *Cap* 178, zinagongana na Sheria Namba 8 ya 2011 ambayo inatoa fursa hata *Tanzania Education Authority (TEA*), yaani Mamlaka ya Elimu Tanzania kuweza kupata pesa kutokana na vyanzo mbalimbali na tumeshuhudia wanafanya harambee, wanapata fedha na wanasaidia kuboresha miundombinu katika elimu. Ni wazo zuri kwamba, sheria hizi zihuishwe, zitasaidia kwanza, itachukua muda mfupi kuliko wazo la mleta hoja alivyosema kwamba, kuunda Sheria mpya ya Mfuko. Yaani *Higher Education Fund Act*. Hii itachukua mchakato wa muda mrefu na kuongeza adha. Mengi ambayo tunayaona katika suala la mikopo, yako katika maeneo makuu matatu, jinsi nilivyochambua:-

Kuongezeka kwa wadahiliwa, suala zima la kuongezeka kwa fedha katika *projection* ambazo nilikuwa napiga naona katika mwaka unaofuata, yaani 2013/2014 ni dhahiri, Bodi ya

Mikopo itahitaji shilingi bilioni mia tatu na hamsini *almost* 356. Ni fedha nyingi ambazo zimesababisha kwa kweli utoaji wa elimu katika nchi kutetereka.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu, katika bajeti ya mwaka huu ambayo tuna-*operate*, 80% ambayo ni bilioni 326 zimelekezwa katika Bodi ya Mikopo. Kwa hiyo, ni dhahiri utaona ni kiasi gani maeneo mengine yameminywa. Huwezi ukatumia 20% ya fedha ya *OC* ya Wizara ya Elimu na Ufundi kwenda kufanya kazi nyingine, ndio hapo *capitation grant* inapungua katika mashule. Unakuta kukarabati vyoo inakuwa ni shida, miundombinu na vitu mbalimbali katika mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Spika, wazo hili la kuleta sheria hii, ije ihuishwe vizuri, tupate Mfuko na vyanzo mbalimbali. Lakini katika timu ambayo iko chini ya Wizara ya Elimu ya Mafunzo na Ufundi, ni dhahiri kwamba wenzetu wa Benki hawa ni wafanyabiashara lazima Serikali iwe macho. Katika kukubaliana na Benki, wanaweza wakasema kwamba Serikali imetenga fedha kiasi kadhaa ili kusudi kama huyu aliyeomba mkopo hajarejesha, Serikali iweze kulipa fedha hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sheria itakavyokuja tuchambue tuone itakuwaje, sababu watu wa Benki wanaweza ku-*sit back* na ku-*relax*, kwa sababu wanajua kuwa yule mrejeshaji kama hajaleta, Serikali italeta fedha. Kwa hiyo, inakuwa ni kipato kama sehemu ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hii ya kwamba sheria ibadilishwe haraka, lazima kuwe na kikomo. Kwa hiyo, mimi nashauri kufikia mwezi *April, or by June* basi sheria hii ihuishwe. Iletwe, tuijadili vizuri, ili tunapoingia katika mwaka wa fedha unaofuata, yaani 2013/2014 tuingie katika utaratibu mwingine mzuri.

Adha ambayo iko katika *Board* ya Mikopo, inachangia hata kuongezeka kwa janga la UKIMWI katika wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu. Maeneo mengine tumekwenda, tunatembelea vijana wanajieleza wazi kabisa; vijana wa kike wakati wa jioni wanakwenda kwenye *bar*, wanaita *conner bar,* anakaa pale ikiwa ni sehemu ya kutafuta fedha kidogo ya kujikimu. Sasa hizi *conner bar* matokeo yake ni kuleta janga la UKIMWI katika nchi yetu.

Kwa kumalizia, tukijaribu kuangalia fedha hizi ambazo zimetolewa tangu mwaka 2005/2006 takribani Shilingi trilioni 1.2. Ni fedha nyingi, lakini Wizara inatuambia kwamba, fedha ambayo imeiva ni Shilingi bilioni 160, lakini marejesho ni kidogo sana. Kwa hiyo, suala la kujipanga vizuri katika marejesho, hili lazima Serikali iliangalie kwa sababu hadi hivi sasa *recovery rate* iko kwenye asilimia 30, Shilingi bilioni 28 ni *return* ambayo ni ndogo na ya chini sana.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, atafuatiwa na Mheshimiwa James F. Mbatia.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika mabadiliko ya sheria hii ambayo yako mbele yetu. Vile vile naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mwigulu L. N. Madelu, kwa hoja yake aliyoiwasilisha na hatimaye tumeweza kupata nafasi hata ya kujadili mabadiliko haya ya sheria. Lakini kabla sijakwenda moja kwa moja kwenye hoja, ningependa, nikumbushie yafuatayo:-

Binadamu yeyote yule, kokote kule, anatakiwa awe na malengo. Kuna malengo aidha ya kijamii, yaani *social goals*. Kuna malengo ama ya kiuchumi, yaani *economic goals*, kuna

malengo au ya kiafya, yanayoitwa *physical goals*, au *heath goals* na kuna malengo ya kielimu, ambayo ni ya *academic goals*.

Sasa hili ni muhimu sana na jambo hili siyo la kupuuza. Kama Serikali, naamini kabisa ni wajibu wake kubeba mzigo wote unaohusishwa na mambo ya elimu kwa nchi yetu. Nasema hivyo kwa nini? Wakati sasa umefika kwa Serikali yetu kuanza kurudi nyuma. Ianze kurudi nyuma kwa maana kwamba, katika awamu ya kwanza, elimu ilishughulikiwa moja kwa moja na Serikali na mimi ni mmoja wa wanufaika. Miaka ya nyuma ile Serikali iliweza kusomesha wananchi wake bila kuwataka kwenda kutafuta mikopo.Kwa maana hiyo, ndiyo maana tuliweza kunufaika na tukapata elimu bila kuwa na wasiwasi wa kufikiria mkopo wangu utapita au hautapita.

Tulinufaika na humu ndani kuna wengi tu ambao walinufaika na mfumo huo hasa wale ambao nakumbuka tulipelekwa na Serikali hii kwenda kusoma nchini Urusi akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji – Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, akiwemo Mheshimiwa Rebecca Mngodo naye ni mnufaika, akiwemo Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, naye ni mmoja wa wanufaika, wakiwemo na Waheshimiwa wengine wengi kama akina Mheshimiwa Pindi Chana na yeye alikuwa mmoja wa wanufaika katika lile kundi la watu waliopelekwa Urusi kusoma na Serikali iligharamia.

Serikali haijatutaka tuombe mikopo, Serikali iliji-*commit* moja kwa moja na wote tulisoma na tulimaliza tukaondoka na elimu ambayo ndiyo tunaitumia wote kwa pamoja hata tulimo humu Bungeni. Ninaposema hivyo sipingani kabisa na mapendekezo ya Serikali ya kuleta mabadiliko katika Sheria ya Elimu, isipokuwa baada ya kuwasilisha haya mapendekezo, Mheshimiwa Waziri ameorodhesha vyanzo vya kupatia fedha, lakini mimi nasema hivi, vyanzo ni vizuri na vinafaa kabisa, isipokuwa ninapingana bado na dhana ya kusema kwamba mwanafunzi ndio afuatilie, ndio aende akakope, mwanafunzi sijui ndio aende akatafute pesa za kumsomesha. Nashauri kwamba Serikali ifanye yote haya.

Mheshimiwa Spika, ni mambo mazuri sana ambayo Serikali imeorodhesha, mojawapo naomba ninukuu kwa ruhusa yako, imesema itakuza hati fungani ya elimu. Kwa hiyo, hili lifanywe na Serikali yenyewe. Imesema kuanzisha Mfuko wa Elimu kama ilivyo mfumo wa biashara. Serikali yenyewe ndiyo ifanye haya na iweze kuwasomesha Watanzania, badala ya kuendelea kuwakopesha Watanzania, iwasomeshe kama ilivyokuwa awamu ya kwanza, sisi wote tulisomeshwa hatukukopeshwa. Naamini tumekuwa matunda bora kwa sababu tulisomeshwa. Tungekopeshwa, nadhani tusingekuwa kama tulivyo sasa hivi.

Mhesimiwa Spika, wewe mwenyewe unashuhudia Wabunge wako wale niliowataja, elimu imewasaidia na hivyo sasa ni wajibu wa Serikali kutilia maanani elimu ya juu. Hakuna nchi inayoendelea bila kuweka msisitizo kwenye elimu ya juu. Kwa hiyo, ni rai yangu kwa Serikali pamoja na marekebisho yote ya Sheria ya Elimu, wanayokusudia kufanya, wafikirie jambo la kusomesha Watanzania na siyo kuwakopesha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Haya ahsante. Mheshimiwa James F. Mbatia, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe, ndiye atakuwa msemaji wetu wa mwisho kabla sijawaita watoa hoja.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mhehimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nampongeza mtoa hoja kwa kuwa hoja aliyoitoa ni hoja nzuri yenye maslahi ya pamoja kwa Taifa letu. Kwenye suala la elimu, inabidi tufikiri kwa mapana na tufikiri chanya. Tatizo linaloikumba nchi yetu leo kwenye Vyuo vya elimu ya juu na wanafunzi wetu, ni tatizo la Serikali kutokufanya maamuzi kwa wakati sahihi.

Hoja iliyoko mbele yetu iliwahi kuzungumzwa na Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mwenyezi Mungu amweke mahali pema, alipokuwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, 1995 mpaka mwaka 2000, na tukawaita wadau mbalimbali Bungeni hapa tukafanya Semina, tukakubali kwamba tuanzishe Mfuko wa Elimu ya Juu. Kwa kuwa bajeti ya Serikali lengo lake kuu la kuelimisha lilikuwa linasuasua, na kwa kuwa suala la kuchangia gharama za elimu ya juu halikuwa ni sera ya Watanzania kama Watanzania, ilikuwa ni masharti ya *IMF* na Benki ya Dunia.

Mwaka 1992, nilisema hili kwa sababu mimi ni mwathirika wa mfumo huu, tulipopinga kwamba, Watanzania walio wengi hawatakuwa na uwezo wa kuchangia gharama za elimu ya juu, tulinyanyasika sana katika Taifa hili. Mimi mwenyewe nilikuwa nimebakiza miezi miwili na nusu nimalize elimu yangu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nikafukuzwa Chuo kwa kunyanyaswa sana, tukiwa tunayazungumza haya mwaka 1992 tarehe 10 mwezi wa Pili siku ya Jumatatu, takaonekana kwamba sisi ni waasi kwa sababu tunapingana na masharti ya *IMF* na Benki ya Dunia.

Sisi kama Taifa, kupanga ni kuchagua. Tunataka tuwe na Taifa gani? Lenye uelewa, lenye upana, lenye kutafakari; kwa Kiingereza wanasema *power of reasoning* na kuweza kusimamia Taifa letu na rasilimali tulizonazo, tukizingatia rasilimali ya kwanza kabisa ni rasilimali watu. Hasa kwenye rasilimali watu tunawekeza namna gani?

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na hoja ya mfuko huu, lakini vikwazo tunavyowekewa na Mataifa mengine, kwani ni namna ya sisi tunavyotaka kupanga utaratibu wetu wa elimu yetu kwa kutumia utamaduni wetu, kwa kutumia mila zetu, kwa kutumia desturi zetu, inakuwa ni shaka kubwa sana!

Sasa maamuzi haya yangekuwa yamefanyika tangu mwaka 1992, zaidi ya miaka 20 iliyopita, Taifa hili leo hii tusingekuwa tunasuasua panda shuka panda shuka, mpaka leo hii ndiyo tunafikiria kuwa na Mfuko wa Elimu ya Juu, inatia uchungu sana. Kwamba suala la elimu linapobinafisishwa linakuwa labda ni la Waziri binafsi, kwamba kuna kikundi cha watu wachache wanaweza wakafikiria kwa niaba ya walio wengi. Ndiyo maana nampongeza sana mtoa hoja hii na Serikali kwa wakati huu. Lakini nachelea sana kusema, kwa nini? Kulikoni? Mpaka mtu mmoja au wawili au watatu wajisikie tufanye maamuzi sasa ndiyo tufanye maamuzi!

Kasi ya kukua kwa sayansi na teknolojia dunia ya leo kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita, kusuasua huku ndiyo kumeleta athari zote hizi leo hii. Inatia uchungu na inasononesha sana tunapoona wanafunzi wa elimu ya juu leo hii, kwa mfano, Chuo cha *IFM*, waliandamana mwezi huu kwa ajili ya unyanyasaji. Inapofika mpaka watoto wa kiume wanadhalilishwa, kuingiliwa kinyume na maumbile kwa sababu hawana mahali pa kuweza kupata elimu kwenye mazingira bora, waweze kujitambua vizuri na kuwa na uwezo mzuri wa kufikiri.

Kama Mheshimiwa Mbunge asingeleta hoja hii leo: Je, Serikali ilikuwa na hata mpango gani wa kuona matatizo haya makubwa kiasi hiki? Ndiyo maana nimesema nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa moyo wa dhati kabisa. Tukisoma Katiba yetu, hakuna aliyeko juu ya Katiba hii.

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu kwa ruhusa yako naomba ninukuu: Ile Ibara ya 11 (2) inasema: “Kila mtu anayo haki ya kujielimisha na kila raia atakuwa huru kutafuta elimu katika fani anayoipenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na stahili na uwezo wake.”

Kifungu cha tatu kinasema: “Serikalii itafanya jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata furusa sawa na za kutosha kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za Shule na Vyuo.” Vinginevyo kwa mafunzo, ni Katiba. Sasa leo hii tunaanza kufikiria tukaombe huku, tukaombe huku, tufanye mikopo ya hapa na pale; Serikali inapata tatizo gani katika bajeti yake ikakusanya makusanyo yake, Bunge tukafanya maamuzi, hata kama bajeti ya elimu itakuwa ni asilimia 30 ya bajeti yote ya Taifa hili, tukawekeza tukaachana na kudunduliza huku na kule?

Let us think big for our Nation, tuangalie kwa nini? Unajua tunapofanyia elimu yetu kana kwamba tunapiga ramli, inatupa shida sana. Kwa sababu mwezi wa Tano mwaka 2006 Baraza la Mawaziri lilikaa, likafanya maamuzi kwamba wanafunzi wanaotaka kuingia Chuo Kikuu, wavulana lazima wapate daraja la kwanza, wasichana daraja la kwanza au la pili, sasa kwenye utaratibu huo, tayari kubaguliwa kukawepo kwa uwazi kabisa na hii nayo ikaleta migogoro mikubwa. Lakini ukiangalia wale wanaomaliza Kidato cha Sita kwenda Vyuo vya Elimu ya Juu, ni kigezo gani kinachotumika cha alama ili kama ni Vyuo vyetu tulivyonavyo viweze vikawa na uelewa angalau unaofanana? Wanasema ile *standardization!*

Sasa, mfuko huu una maslahi makubwa sana kwa Taifa letu. Tusifanye tu kwa sababu imeletwa, tufanye haraka haraka. Naishauri Serikali ifikiri kwa mapana, lakini tuna tatizo la urasimu la Watendaji ambao wanajifanya Miungu watu, hata kama Waziri ungekuwa na nia njema kiasi gani, wale wasaidizi ambao walitakiwa watekeleze wataalam, wewe mwenyewe unajua katika Wizara yako matatizo yaliyoko. Unajua tumeshawahi kuzungumza mara ngapi kuhusu mambo kama haya?

Mheshimiwa Spika, naomba tufikirie na tuangalie *the best practice* ya nchi za wenzetu katika kutoa elimu ya juu ikoje, na tukiweza kufanikiwa hivyo, naamini kabisa kwa sababu dunia hii ni Kijiji, Tanzania ni sehemu ya Kijiji hiki, sisi ni tone ndani ya kijiji hiki. Kasi ya ukuaji wa elimu duniani, Taifa letu tunaliandaa namna gani ili tuweze tukajitawala vizuri, tukajiongoza vizuri ili tuweze tukashindana na dunia nyingine?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono tuanzishe mfuko huu, lakini tusifanye kwa papara, baada ya siku mbili tena tunarudi. Tufikiri kwa mapana ili tuone kweli mfuko huu, au vinginevyo, itakuwa njia bora kwa ajili ya kumwendeleza Mtanzania bila ubaguzi wowote na kwa maslahi yetu sote kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe, halafu ataitwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika**,** ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Ludewa na Watanzania wote, hasa wale wazazi ambao ni masikini, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kabisa, hoja ambayo inalenga kwenye kuanzishwa kwa Mfuko wa Elimu ya Juu, ili vijana wetu; watoto wetu wanaotoka familia masikini waweze kupata elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwapongeza pia Wabunge wenzangu kwa sababu wameunga mkono hoja hii bila kujali itikadi ya vyama vyetu. Mimi niseme tu kwamba, tulipofikia sasa hivi hapa katika upande wa elimu, tumefikia mahali pabaya sana. Ukitazama sana huko mbele tunakoelekea, tutaishia kuwa na elimu inayotoa Taifa la wajinga. Kwa mfano mpaka miaka ya 1990, hapa Tanzania ulikuwa ukimwona mtu mzima au ukimwona mtu yeyote yupo kwenye jalala, tulikuwa tunajua kwamba ni kichaa. Tulipofika sasa hivi

Waheshimiwa Wabunge nyinyi mtakuwa mashahidi, Tanzania imekuwa ni nchi pekee duniani ambapo watu wazima wenye akili timamu wanakwenda jalalani kuokota makopo.

Waheshimiwa Wabunge, mnaona hili kila siku, watu wazima kule Dar es Salaam kuokota makopo jalalani! Wale watu sio vichaa! Ni watu wazima wenye akili timamu. Sasa tujiulize, kuna kitu gani? Tuna mifano mingi ya kuitolea hapa, lakini kimsingi tu ni kwamba, ni lazima tusomeshe watoto wetu elimu yenye taaluma na maarifa. Tumefika mahali sasa tunatoa elimu ambayo inatoa taaluma peke yake na maarifa hakuna.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwamba kila mtoto mwenye uwezo bila kujali ni mtoto wa masikini au ni wa tajiri, apewe mkopo kwa asilimia 100 na bila riba. Mtoa hoja ametoa vyanzo vya mapato vitoke wapi, ametaja sehemu nyingi sana. Sehemu mojawapo ni fedha kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mimi naomba kutofautiana nao, fedha zipo mahali pengine, nami niseme sehemu moja tu ambayo ipo. Ni wazi kila mmoja anaweza kufanya na Waheshimiwa Wabunge tunashiriki kwenye hili. Waheshimiwa Wabunge tunaongoza sana kwenye kuchangia harusi, tufike mahali sasa tuache tabia ya kuchangia harusi, tuchangie elimu.

Sehemu mojawapo tuwaombe Watanzania pia wafanye hivyo. Mfano mmoja mdogo, mtoa hoja amesema, takwimu zinaonyesha kwamba watumiaji simu hapa Tanzania wako milioni 28. Katika hao *Vodacom* wana wateja 12,500,000; *Airtel* wana wateja milioni 7.5; Tigo wana wateja milioni 5.6; *TTCL* wana wateja milioni 2.3 na *Benson* na *Sasatel* wana wateja 300,000. Wateja hawa milioni 28, wenye simu, kila mtu akiambiwa achange Sh. 2,000/= tu kwa mwezi, ambayo kwa mwaka itakuwa Sh. 24,000/=, Watanzaina wote tutasoma bure. Siyo elimu ya juu tu, bali ni elimu ya juu, Shule ya Msingi na Sekondari, kwa sababu kwa wateja milioni 28 kwa mwezi tutapata Shilingi bilioni 56.

Mheshimiwa Spika, Shilingi bilioni 56 kwa mwaka ni mara miezi 12. Kwa mwaka mmoja tunapata Shilingi bilioni 672. Mahitaji ya sasa ya elimu ya juu ili kusudi kila mwanafunzi asome na apate mkopo wa asilimia mia moja tunahitaji Shilingi bilioni 350, ukitoa hapo kuna Shilingi bilioni 322 zinabaki. Hizi fedha zinazobaki kwa sababu leo tunatatua sehemu moja tu la elimu ya juu, lakini elimu ya juu ili ipatikane ni lazima tuimarishe elimu ya msingi na ya sekondari. Imefika mahali sasa hivi mwaka huu wanafunzi wamefaulu na wameongezewa *marks*, siyo za ku-*standardise,* bali ni za kuongezewa ili wafaulu waende wakasome madarasa yajae. Tunatatua tatizo la elimu ya juu, lakini elimu ya msingi na ya sekondari ni mbovu, tunakwenda wapi? Kwa hiyo, fedha zinazobaki tuzipeleke Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, Walimu wakaguliwe. Idara ya Ukaguzi imesimama, fedha hakuna na kila Mbunge humu ndani anajua. Hiyo elimu ya juu tunaiimarisha, lakini kwa nini tunaisahau elimu ya msingi? Mwaka 2012 ufaulu ulipokuwa *marks 70* yaani mwanafunzi anafaulu kwa 40% tulipata wanafunzi 11,000 wasiojua kusoma na kuandika, yaani K3 kwa maana hawajui Kusoma, Kuhesabu na Kuandika. Sasa kama hawa ndiyo walifaulu na hawajui K3 wale waliofeli sijui hali ilikuwaje? Naomba sana tuimarishe pia elimu ya msingi na siyo elimu ya juu peke yake.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwigulu kwa kuleta hoja hii. Lakini pia nitumie fursa hii kuwapa changamoto wenzetu wa Wizara ya Elimu. Mbunge ametoa hoja leo, Wabunge tunaunga mkono, lakini Wizara ya Elimu mlikuwa wapi miaka yote hii kuyaona haya? Hiyo ni kazi yenu na ni dhamana yenu, mnalipwa na haki zenu mnapata, lakini wajibu hamtimizi. *(Makofi)*

Mwaka huu wanafunzi wamefeli sana. Lakini badala kuwaambia wazazi kwamba tumedondoka na kutelekeza, tujipange vizuri tuone wapi kuna changamoto kwa wazazi, shuleni

na kwa Serikali, sisi tumeamua kuongeza alama 108 kwa kila mwanafunzi ili wanafunzi waende madarasani. Nasema hayo kwa majonzi na masikitiko makubwa sana, kwamba tunapeleka wanafunzi waliofeli Kidato cha Kwanza kujaza madarasa. Tunaishia kujenga Taifa lisilo na uelewa, weledi, maarifa wala taaluma.

Waheshimiwa Wabunge, fedha zipo. Ninawasihi tuache kuchangia harusi, kwani Tanzania ni nchi pekee ambayo mwanafunzi akifeli anapewa *marks* aende akasome, yaani anajaziliziwa *marks*. Sasa iwe ni fursa pia kwa wenzetu wa Wizara ya Elimu kujitafakari. Hakuna haja ya Wabunge kufanya kazi zenu, kwa sababu hiyo mishahara yenu hamtuletei sisi. Kwa nini leo Wabunge tunafanya kazi zenu na ninyi mpo? Tume zimeundwa toka mwaka 1998, mapendekezo yapo hapa, Waziri anayaleta, mlikuwa wapi toka mwaka 1998 kuyasema haya? Miaka 10 inapita na miaka kadhaa inapita. Kila mmoja atimize tu wajibu wake! Atimize wajibu wake, kama uzalendo unashindikana! Tunapoua elimu na tunapokandamiza elimu, hatuwezi kufika.

Kule kwangu Ludewa mwezi Februari, 2012 na Januari, 2012, *capitation* zilikuja Sh. 1,400,000/= kwenye baadhi ya Shule za Msingi, tuligawa Shilingi 300 na Shilingi 500. Mheshimiwa Mbunge amezungumzia elimu ya juu, lakini mimi nataka kusema, tuimarishe elimu kwa pande zote tatu, yaani elimu ya juu, Shule ya Msingi na Vyuo vya Ufundi. Hali ya elimu kule chini ni mbaya na ni lazima Wizara itimize wajibu wake.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, yenyewe hayo, ipo hoja kesho.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, sawa!

Mheshimiwa Spika, nataka tu kusema kwamba hizi fedha tutazame pia upande mwingine. Vyuo vinavyopewa hizi fedha ni Vyuo binafsi na Vyuo vya Serikali. Vyuo vya Umma vinakaguliwa, lakini tumegundua kwamba kuna baadhi ya fedha Serikali ilikuwa inapeleka na fedha hizi zinaliwa. Kwa hiyo, Vyuo binafsi vitakavyopata fedha hizi vikubali kukaguliwa kwa sababu ni fedha za umma na ni mali ya Watanzani. *CAG* pia aende akazikague zile fedha ili kuona: Je, zinafika kwa lengo na zinafanya kazi stahiki? Ni lazima akague fedha zetu kwa sababu hata kama ni Vyuo binafsi, lakini vinatumia fedha na mali ya umma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba wanafunzi wote wapewe mkopo kwa asilimia mia moja, tena bila riba na fedha zisitoke kwenye mifuko ya jamii, tuchange sisi wenyewe na tuwe mfano. Kama tunachangia harusi Sh. 50,000/= au Sh. 100,000/= mimi nimefanya utafiti mdogo, Dar es Salaam peke yake mwaka 2012 tumechangia Shilingi bilioni 720, kwenye harusi. Hiyo ni Dar es Salaam peke yake. Sasa tuna Mikoa mingapi Tanzania? Hiyo ni Dar es Salaam peke yake, lakini ukienda Mbeya, Mwanza na maeneo mengine, kwa nini tunakuwa wepesi kuchangia harusi na tunakuwa wagumu kuchangia elimu? Tena siyo pesa nyingi, tuchange Sh. 2,000/= na Sh. 24,000/= kwa mwaka, siyo tu kila Mtanzania atasoma bure, lakini kila Mtanzania atapata elimu bora yenye maarifa na yenye weledi na yenye taaluma.

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tuwe wa kwanza, fedha zipo na tuchange kwa kutumia simu zetu Sh. 2,000/=, Watanzania wakielimishwa watachanga. Watanzania hawana shida, lakini shida tunayo sisi ambao wametupa dhamana ya kuwatumikia na kuwaongoza. Tuwaongoze wananchi wa Tanzania, kwani hawana shida kabisa!

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri na nitampa dakika kumi na tano tu.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, nitangulize kumshukuru sana mtoa hoja Mheshimiwa Nchemba kwa kuleta hoja kwa wakati muafaka na hoja ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Pia namshukuru sana yeye pamoja na Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii na hasa kwa kukubaliana na kupendekeza badiliko la Azimio la Bunge kwa hoja hii binafsi ili tufanye kazi hiyo katika sheria tunazo ili ziweze kukidhi haja ya kuwapatia mikopo wanafunzi wa elimu ya juu nchini kwetu kwa kiasi kikubwa zaidi kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Spika, mzigo wa elimu ya juu ni mkubwa sana, tunaweza tukaungalia kwa idadi ya wanafunzi ambao walikuwa wanaongezeka mwaka hadi mwaka. Hii ni kazi nzuri na kubwa ambayo imefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka kadhaa tangu TANU mpaka hivi sasa CCM. Ni kwa kupitia Serikali za Chama cha Mapinduzi tu ndiyo tumeweza kupata ongezeko hilo kubwa la wanafunzi katika elimu ya juu na hatumalizii hapo tu, bali tutaendelea zaidi na zaidi tuongeze fursa hizi ili tupate wananchi wengi zaidi, wawe wanasoma masomo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tu katika idadi ya wanafunzi waliopata mikopo kwa miaka 10, yaani kuanzia mwaka 1999 - 2004 ilipoanza kutolewa mikopo ni wanafunzi 48,378. Hiyo ni miaka kumi. Lakini kwa mwaka huu wa masomo peke yake, waliopata mikopo jumla yao ni 94,773. Miaka 10 ni wanafunzi 48,378 na mwaka mmoja ni 94,773. Idadi ya mikopo imeongezeka kwa kiasi kikubwa mno na gharama ya mikopo imekuwa ni kubwa mno. Pesa hizi ni nyingi mno! Serikali hii ingependa kufanya kama ilivyokuwa inafanya huko nyuma kutokuwapa mikopo na kugharamia elimu ya juu kwa fedha ya Serikali peke yake, lakini mzigo huu kwa vile umeendelea kuwa mkubwa na mkubwa zaidi, hivyo basi, Serikali imelazimika kufanya mabadiliko na kuwahitaji wananchi kuchangia katika gharama hizi kama ambavyo nchi nyingine zinafanya.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010/2011 bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto jumla yake ilikuwa Shilingi bilioni 16, lakini bajeti ya mikopo ya elimu ilikuwa ni Shilingi bilioni 317 ukilinganisha na Wizara nzima kujiendesha na mipango yake ya maendeleo kwa mwaka mzima ni Shilingi bilioni 16 na ukachukua bajeti hii ya Shilingi bilioni 317 ambayo siyo ya Elimu yote bali, ni bajeti ya mikopo peke yake ni Shilingi bilioni 714, maana yake katika mikopo inaingia karibu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ni kama Wizara 20.

Huu ni mfano mdogo tu nimetoa ili kuonesha ni namna gani Serikali imeelemewa na mzigo huu mkubwa na hali inaonesha wazi kuwa ni vigumu kwa Serikali hii kuendelea kubeba mzigo huu kama vile ambavyo Serikali nyingine duniani ikiwemo Serikali ya nchi ya Afrika Kusini, ambayo ina uwezo mkubwa zaidi kiuchumi kushinda Tanzania, ambayo imeingia kwenye mpango huu wa kuchangia elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu hiyo tu imepelekea Serikali hii kuamua kuingia kwenye sera hii. Uchangiaji huu ni uchangiaji wa kiuendeshaji, lakini Serikali inagharamia miundombinu katika Vyuo hivi kama vile majengo, vyumba vya mihadhara, maabara, karakana na kadhalika. Hii hailipiwi na uchangiaji wa wanafunzi kama ambavyo wanachangia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili adhimu na kubwa ni muhimu sisi kama wananchi tulipe kipaumbele na kuchangia Serikali yetu ili wale ambao hawamudu sasa hivi kupata elimu ya juu kwa sababu ya kutokuwepo kwa fedha, zipatikane fedha ambazo zitawawezesha nao pia kujiunga na elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba Serikali ilishaanza mchakato kama ambavyo nimeelezea katika taarifa yangu na haikukaa kimya kungoja mpaka labda Bunge ama mwananchi mwingine atoe hoja.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ya mwisho ambayo tumeiunda na inafanya kazi sasa hivi, ni Kamati ya Wataalamu. Ndani ya Kamati hii kuna Wajumbe kutoka Benki Kuu, kuna Wajumbe kutoka Hazina. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, na Mabenki ya Kibiashara ambayo wanafanya kazi ya uhakika ili kuweza kuhakikisha kwamba yale ambayo yanapangwa ndiyo yale ambayo yanaweza yakafanyika. Sasa hivi wameingia katika mchakato wa kuweza kuhuisha maeneo yale ambayo tunasema yatakuwa chanzo kwa majadiliano ili kuwa na uhakika kuwa yatakuwa ni chanzo.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kwamba baada ya kazi hii, bila shaka tutakuwa na mfuko. Siyo mfuko tu, lakini mfuko wa elimu ikiwa ni sehemu moja, lakini ukijumuisha na vyanzo vingine, *bonds* za elimu na kadhalika ili kuweza kuwa na wigo mpana zaidi ambao utawezesha kila mhitaji apate mkopo. Siyo lazima achujwe na kadhalika, lakini akisema anahitaji, aweze kukopa katika mifuko hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba kazi hiyo tutaifanya kwa juhudi zetu zote na nichukue nafasi hii kutoa ahadi kwamba baada ya hoja hii Wizara yangu na Serikali kwa ujumla inatoa ahadi kwamba tutaharakisha katika mchakato wa kuwasilisha Muswada wa mabadiliko ya sheria kama tulivyoahidi ili isichukue muda kuweza kufikisha Miswada hii na Bunge lako Tukufu liweze kujadili na kuridhia mabadiliko tutakayoyafanya ili kuwezesha vijana wetu wengi ama wote watakaokuwa wanahitaji waweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Unaunga mkono hoja siyo?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Kutokana na kwamba hivi sasa wanafunzi hawana uhakika wa kupata mkopo kwa wakati na kiwango ambacho kitaweza kukidhi masomo yao, ni jambo bora tuwe na Mfuko wa Elimu.

Mfumo huu wa sasa wa kutoa mikopo kwa wanafunzi unawapa usumbufu sana, wanahangaika kupata hii mikopo kutokana na Bodi kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi zake. Ukopeshaji wa sasa unashindwa kuwajua wale wenye uwezo na wale wasiokuwa na uwezo.

Tatizo lingine kubwa ambalo linawakabili wanafunzi ni kusoma yale masomo ambayo siyo wanayotarajia kuyafanyia kazi ilimradi wanasoma ili wapate mkopo. Pia kuna yatima ambao wanapata asilimia mia moja, wakati wengine wanao urithi mkubwa.

Tukiwa na huu Mfuko hatutakuwa na chanzo cha uhakika na havitokani na Bajeti peke yake, pamoja na kwamba Serikali itatoa asilimia fulani kwenye hii mikopo.

Tatizo ninaloliona ni hili la riba, sijui wanafunzi watalipokea vipi? Hili linataka itolewe elimu ya kutosha.

Changamoto itakayoukabili Mfuko huu ni kutafuta vyanzo vya kupata pesa kwa ajili ya huu Mfuko na pia wingi wa pesa zitakazohitajika katika huo Mfuko.

Tahadhari pindi ukikubalika kuanzishwa Mfuko huu, lazima tupate watu ambao ni waaminifu na wenye uchungu na nchi yao ili kusimamia huu Mfuko. Tusitafute mafisadi kusimamia Mfuko huo wakaja kuzidi kutufisadi na hii dhamira nzuri isionekane. Katika vyanzo ni pamoja na kupata asilimia kumi ya misamaha ya kodi. Hili tayari ni tatizo kubwa kupatikana hizi fedha, kwani mfumo mpaka hivi sasa ni mbovu. Kwanza, tuwe na mfumo mzuri wa hii misamaha halafu tujikite kupata hiyo asilimia kumi kwa wale wanaopata misamaha.

Kwenye makampuni ya simu ninakubaliana na wewe ni kweli Makampuni ya Simu hayaweki wazi mapato halisi. Mapato yao huwa wanadanganya na hiyo ya kufunga mitambo ambayo itatupa uhakika wa mapato yao ili waweze kusaidia Mfuko huu ninakubaliana na wewe.

Natoa ushauri mwingine kuwa Sekta ya Uvuvi ipewe kipaumbele ili iweze kukusanya mapato na iweze kupatikana *percentage* fulani ya Mfumo wa Elimu.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya uanzishaji wa Mfuko wa Elimu ya Juu. Mfuko huu utasaidia kuinua elimu. Suala hili nalikubali kwa asilimia mia moja na hata hivyo imechelewa kuja. Kwa hiyo, ni wazo zuri sana na mapendekezo yote yaliyopendekezwa ninakubaliana nayo.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kwa kuleta hoja hii hapa Bungeni. Pia naipongeza Serikali kwa kukubali uzito wa hoja na kuleta marekebisho ya kuongezea nguvu katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nashauri katika kutoa mikopo, mikopo isiwekewe riba, kwani kuna baadhi ya Watanzania hawawezi kukopa kwa riba kutokana na imani yao ya kidini. Kuwekewa riba kutawanyima baadhi ya Watoto wa Kitanzania fursa ya kupata mkopo; hivyo, kushindwa kupata Elimu ya Juu.

Nampongeza sana Mheshimiwa Nchemba, kwa hoja hii. Naunga mkono hoja.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ninashauri maeneo yafuatayo:-

(i) Mfuko wa *Revolving Fund;*

(ii) Bodi ya Mkopo ipewe mamlaka ya kushtaki wale ambao hawataki kurudisha mkopo;

(iii) Mfuko uzingatie *In-Service;* na

(iv) Kufanyike marekebisho ya sheria zilizopo badala ya sheria mpya kuletwa.

MHE. DKT. HAMISI A. KINGWANGALLA: Awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa kuanzisha mjadala huu muhimu wa namna ya kuongeza vyanzo vya mapato kwenye elimu ya juu. Japokuwa alitaka uletwe Muswada kabisa wa Uanzishaji wa Mfuko wa Elimu ya Juu, na Serikali kimsingi haipingi sema imeboresha kupendekeza ilete mabadiliko tu. Naunga mkono ushirikiano huu na ninawapongeza.

Mheshimiwa Spika, kuwekeza katika elimu ni jambo la lazima kwa Taifa letu na jambo hili hatuwezi kuliacha mikononi mwa Serikali peke yake, ni lazima kila mmoja wetu achangie.

Naunga mkono hoja ya kuweka ulazima wa kuchangia elimu kwa *private sector* ili kuongeza vyanzo kwenye mfuko huu. Hii ni kwa sababu siku hadi siku idadi ya wanafunzi wanaohitaji mikopo inazidi kuongezeka, jambo ambalo litapelekea Serikali kulemewa na mzigo huu. Wakati ambapo nchi yetu inaendelea na jitihada za kukuza uchumi, ni lazima tukiri kwamba ni jambo gumu kwa watu wenye kipato cha chini kugharamia elimu yao, hususan ya juu, na kwa kuwa nchi yetu imejengwa katika misingi ya haki, usawa na mshikamano wa kitaifa, na kwa kuwa tunaamini sana katika uwezo sawa wa watu wote kitaaluma, ni lazima tutafute suluhu ya tofauti zetu za kipato ili tuweze kutoa usawa na haki katika Taifa kwa watu wetu wote.

Mheshimiwa Spika, hoja hii inalenga kutafuta namna ya kuhakikisha hilo likifanikishwa, na hivyo basi, naiunga mkono na kupendekeza maazimio haya yatekelezwe haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SILYVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Spika, nakupongezwe wewe na Bunge lako kwa kuuona mwaka mpya. Nampongeza Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba kwa hoja hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo wazi na nia njema ya Serikali yoyote ulimwenguni kuelimisha wananchi wake kuwa ni kazi muhimu ya Serikali, na kwa kuwa gharama za elimu na hasa elimu ya juu ni kubwa ukilinganisha na kipato kidogo cha Watanzania walio wengi na kwa kuwa asilimia kubwa ya vijana wanaosoma na kufaulu au kukidhi vigezo vya kusoma elimu ya juu ni watoto wa Watanzania wanyonge na wenye uwezo mdogo, ni muhimu kuwa na mpango mahsusi wa kupata fedha na kuhakikisha kuwa wanafunzi hawa wanawezeshwa kwa mikopo.

Mheshimiwa Spika, ni wazi fedha zinazohitajika ni nyingi na uwezo wa Serikali ni mdogo. Kuna njia nyingi ambazo ni pamoja na kuimarisha mtandao wa kukusanya kodi *(broadening of tax base)* kwa kuangalia nyanja mbalimbali za uzalishaji na utoaji huduma ambazo bado hazijafikiwa kwa utozwaji wa kodi, kwa mfano, Makampuni ya Simu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wabunge tumehimiza sana namna ya kuboresha Elimu ya Msingi na Sekondari katika Majimbo yetu.

Tumeanzisha Mfuko wa Elimu wa Jimbo ambao wananchi wote watachangia na wale wenye uwezo wa kiuchumi kulingana na shughuli za kiuchumi wazifanyazo katika Jimbo hilo, hawa watapangiwa kiwango maalumu cha kuchangia mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, nami ningeshauri pia kuwe na utaratibu maalum wa kuchangia Mfuko huo kama inavyofanyika katika michango ya Maendeleo ya Elimu ya Ufundi, yaani *VETA*. Kila Mtanzania achangie kiasi fulani Makampuni na Mashirika wapewe kiwango maalum na hivi ndivyo tunaweza kuwafanya wenye uwezo mkubwa kusaidia kusomesha watoto wa walio wanyonge.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi sasa ni kuweza kukidhi ongezeko la Vyuo na wanafunzi ambalo sasa ni zaidi ya asilimia 15.

Kubwa zaidi sasa ni mpango kabambe wa kufuatilia na kuhakikisha kuwa fedha hizo zinarejeshwa na kukidhi mzunguko ili vijana wengi Watanzania waweze kupata nafasi za kusoma Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu kwa kuona kuna haja ya msingi ya kuwasilisha hoja binafsi ya kuitaka Serikali iwasilishe Bungeni Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Elimu ya Juu *(The Higher Education Fund Act).*

Mheshimiwa Spika, sababu na faida ya kuanzisha kwa Mfuko wa Elimu ya Juu zinajitokeza kabisa bila shaka yoyote.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika sasa wa kutoa mkopo haufai na haueleweki na vijana wanaopata mikopo kwa ajili ya elimu ya juu, ni wachache sana pamoja na sifa walizokuwa nazo.

Pia vijana wengi watalazimika kusoma taaluma ambazo hawazipendi, kwa sababu ndiyo vipaumbele vya Serikali katika kutoa mikopo. Hivyo inakuwa vigumu sana kupata ufanisi mzuri wa kazi pindi vijana hawa wanapokuwa wamemaliza masomo yao na wameajiriwa katika sehemu mbalimbali za kazi.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu umekuwa wa kibaguzi na kuunda matabaka mbalimbali hapa nchini.

Haki ya msingi ya vijana wetu kupata elimu ya juu imekuwa ya ubabaishaji, inatoa nafasi na mwanya kwa mazingira ya rushwa kutumika. Pia inatoa fursa, mikopo mingi kwenda kwa watu wenye "*influence"* au madaraka badala ya mikopo hii kwenda kwa watoto wa watu wasio na uwezo.

Mheshimiwa Spika, wengi wa wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitihani yao ni wale waliosomeshwa katika shule bora *(International Schools)* ambazo zinafundishwa kwa kiwango cha juu na vifaa bora vya ufundishaji vinapatikana na walimu wa kutosha ili haki itendeke. Ni vyema tukubaliane na hoja iliyotolewa hapo juu.

Mwisho, naipongeza Serikali kwa kukubali kuunda Mfuko wa Elimu ya Juu kwa kuzingatia vyanzo vyote vya mapato vilivyopendekezwa na hasa kufuatilia mapato ya Makampuni ya Simu na Migodi.

Naunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu pamoja na mabadiliko ya Serikali ya kuleta Muswada hapa Bungeni.

SPIKA: Mheshimiwa Mchemba! Nimemwita kwanza huyu!

MHE. MWIGULU L. M. MADELU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwatambua kwa kuongea, nikianza na Mheshimiwa Waziri wa Elimu - Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Margareth Sitta, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Eng. Stellah M. Manyanya, Mheshimiwa Stephen Kebwe, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Deo Filikunjombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue pia waliochangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Amina Amour, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Khamis Kigwangalla, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Suleiman Jafo na Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge imeelezea kwenye msingi ule ule wa hoja wa kutaka tuwe na chanzo cha uhakika cha mapato na wameunga mkono mtazamo mpana wa kutokuwa tu na mfuko, bali kuwa na vyanzo ambavyo vitawezesha wanafunzi wa elimu ya juu kupata mkopo wa kuridhisha kwa wakati bila usumbufu. Baadhi tu ya mambo ambayo wameyaelezea na wale waliochangia kwa maandishi imejitokeza kwenye upande wa riba, nilitaka nilitolee ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili la riba ni tofauti na lilivyoongelewa na ndugu yangu Mheshimiwa Silinde kwamba tunakwenda kuwatoza wanafunzi wa Chuo Kikuu. Siyo hivyo! Siyo dhana ya riba! Dhana ya riba tunayoongelea, tunasema kwenye Bodi ya Mikopo sasa hivi, wanafunzi wanaotokea kazini hawapewi kipaumbele, bali wanaopewa kipaumbele ni wale wanaotokea *Form Six*. Lakini kuna wanafunzi wanaotoka kazini ambao tayari wapo kazini na wana kipato. Pia kuna wanafunzi wengine wanaokwenda Vyuo Vikuu ambao wanatokea kazini na tayari wanachangia kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii, wana fedha zao ambazo wanachangia kule, hawatokei shuleni. Tayari wana kipato!

Sasa tunasema tukianzisha dirisha lingine kwamba kwa hawa watu waliokuwa wanakosa mikopo kwenye Bodi ya Mikopo, kukiwa na dirisha kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii kwa watu ambao tayari walishachangia na wana kipato tayari, ama kwa mtu anayetokea kazini akapata dirisha kwenye Benki ambayo na riba yenyewe ni ndogo kuliko ya Benki za Biashara nyingine kwa sababu Benki hiyo itakuwa imekopa kwa riba nafuu kutoka Benki Kuu kwa mpango maalum wa Serikali wa kupanua elimu, kwa hiyo, si kitu cha kuumiza kama kinavyochukuliwa kwamba mwanafunzi atatoka tu *Form Six* aende akakutane na riba na wengine tutachochea kama vile watafuatwa pale pale Vyuoni kutozwa riba. Siyo hivyo! Kwa hiyo, ni dirisha maalumu ili kupunguza msongamano wa kutumia dirisha moja na halitawahusu, kwamba mwanafunzi bado yupo Chuoni anakwenda kudaiwa ama anaongezewa mzigo ambao kwake utakuwa mkubwa.

Kwa upande mwingine tuliokuwa tunasema kwenye kulinda thamani, tulikuwa tunasema watu hawa kama wanakopa halafu wanarudisha baada ya miaka kumi, yupo kazini na ana kipato, mtu yule huwezi kumsemea kwamba unakwenda kumdai mwanafunzi Chuoni ama Mtanzania aliyepo shuleni ama mtoto wa masikini.

Kwa hiyo, ni mtu ambaye kuliko mtu aliyepo kazini akakosa kabisa mkopo wa kwenda shuleni, ni vyema kukawepo dirisha kwa sababu ile ni Taasisi ya kifedha, lakini ikawekewa muundo ambao utaruhusu wafanyakazi wake wakakopa na watakaporudi kule watakuwa wameshaongezewa mshahara. Kwa hiyo, nyongeza ile ndiyo itakayolipa tu ile fidia. Kwa hiyo, tulikuwa tunaangalia tu kuweka mtindo wa kisasa kuliko hawa watu kutoka kazini na kwenda kushinda nje ya jengo la Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, hili la ndugu yangu Silinde, anajua kabisa kwamba *once you provoke on issues concerning the parties* anajua ambavyo huwa naitetea CCM. Alitaka kunitoa kwenye agenda. Hiki kitu anachosema sheria, alichokuwa anasema ni kwamba wao walisema kwenye Ilani yao kwamba wangeanzisha Mfuko wa Elimu. Huo Mfuko tayari ulishaanzishwa tangu mwaka 2001.

Mimi nilichokuwa nasema, ilikuwa ni kutoka kwenye huo Mfuko twende kwenye Mfuko wa Elimu ya Juu. Sasa ndiyo hivyo tena, kule kwetu *when men are talking, actually boys should listen.* Sasa hiki ni kitu kingine tofauti kabisa! Tunaongelea Mfuko wa Elimu ya Juu na Mheshimiwa Waziri ameelezea kwamba ni Sheria Na. 8 ndiyo itakayorekebishwa ili tuweze kupata na Mfuko wa Elimu ya Juu mle mle kufuatana na sheria ile. Sasa tukienda kwenye mazingira mengine, imeelezewa kwamba mazingira ambayo yalikuwa yanatumia vigezo, Wabunge wamesema

kwamba yana harufu ya rushwa, yana harufu ya watu wenye *influence* watoto wao kuweza kupata mikopo. Ni kweli! Sasa tukienda kwenye mfumo ambao utatupatia vyanzo vingi vya kutosha, hii itatusaidia, tutakuwa tumeshaondokana na vigezo vyote vilivyokuwa vinatumika.

Kwa hiyo, vigezo pekee vitakavyotumika, cha kwanza itakuwa ni ufaulu wa mwanafunzi, lakini cha pili awe ameshapata Chuo kwamba fedha ile ni kwa ajili ya elimu. Kwa hiyo, awe ameshapata Chuo, atatumia kitambulisho cha kuwa amedahiliwa na kitambulisho cha uraia na hiyo itaweza kusaidia kupunguza mlolongo mwingi wa wanafunzi kutoa maelezo mengi kutafuta vigezo vya kukopeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuongezea vyanzo vingine kama hiki alichokisema Mheshimiwa Deo Filikunjombe. Ni kweli, tuwe tu na nia, tusiwe tunashindwa kabla hatujajaribu. Tusiwe tunashindwa kabla hatujathubutu kwa sababu tukisema tu kila wakati kama alivyosema Mheshimiwa kwamba Serikali ilifanye hili jukumu mia kwa mia, kuna utofauti mkubwa sana wa enzi ile ambayo wanafunzi walikuwa wachache ukilinganisha na sasa. Huu ni ukweli usiopingika kwamba, wakati ule wanafunzi walikuwa wachache sana. Kwa sasa ukiamua kufanya hivyo, mipango mingine yote itakwama.

Kwa hiyo, kwa kuwa kipimo cha utu ni kazi, tuchangie. Tuchangie lakini kwa utaratibu huu ambao utakuwa na mfuko. Serikali itakuwa imefanya kwa kiwango kikubwa sana kwa sababu hivi vyanzo vitakuwa vinatokana na mipango ya Serikali itakayotokana na rasilimali. Lakini kitakachokuwa kinafanyika ni kuufanya mfuko uwe endelevu, ndiyo maana tunasema aliyenufaika kama mnufaika itakuwa ni sehemu yake ya kutumia elimu aliyoipata kuwaendeleza na wengine waweze kupata elimu. Kwa hiyo, ni jambo tu la kushirikiana katika kuijenga nchi yetu sote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka hata katika hali ya kawaida, idadi ya watu inapoongezeka, ukiruhusu matumizi yote yakaenda kwenye kipengele kimoja, kwingine mambo yatakwama. Sasa nilichokuwa nasema, wengine wameelezea kuhusu elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Deo Filikunjombe amesemea vizuri kwa kufafanua kwamba, tukipata fedha ya kutosha tutakuwa tumesaidia elimu ya msingi pamoja na sekondari, tuweze kwenda kwa pamoja. Uwepo wa mfuko huu una lengo lile lile kwamba kama fedha nyingi ilikuwa inakwenda kwenye elimu ya juu, uwepo wa mfuko ukawa unajitegemea kwa ajili ya elimu ya juu, maana yake tutakuwa na fedha inayotosheleza kusaidia elimu ya msingi kutokana na bajeti na kusaidia elimu ya sekondari. Unaona hata matatizo yanayojitokeza kwa sasa, mengi ni ya kibajeti. Hata malipo kwa walimu ni ya kibajeti kwa sababu fedha inayotengwa ni ile ile inakwenda kusomesha wanafunzi Vyuo Vikuu.

Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo kama tutabainisha kwenye vyanzo, tutakuwa tumesaidia sana kuhakikisha kwamba elimu kwa ujumla inakwenda sambamba na tutaondoa usumbufu huu unaojitokeza.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana pia na mapendekezo yaliyotolewa ya vyanzo vingine kama hii *revolving fund* ambayo kimsingi ndiyo Mheshimiwa Deo Filikunjombe ameisisitiza.

Mheshimiwa Spika, pia kuwepo kwa marekebisho ya sheria. Waheshimiwa Wabunge wengi hata walioandika wameelezea mazingira kwamba kuleta sheria mpya kutachukua muda mwingi zaidi kuliko kufanya marekebisho.

Sasa niiombe tu Serikali kama ahadi iliyotolewa kupitia kwa Mheshimiwa Waziri kwamba jambo hili lifanyike haraka. Kama alivyoahidi lichukuliwe hatua haraka kwa sababu kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati - Mheshimiwa Margaret Sitta, ni kweli wanafunzi wanapata shida. Ukizungukia Bodi ama kwenye Vyuo utayaona mazingira wanayokutana nayo. Wanafunzi anakuwa na kiu ya kusoma, lakini mkopo hata kile kidogo kinachelewa ama wakati mwingine anakuwa na kiu ya kusoma lakini hapati mkopo. Kwa hiyo, jukumu hili lifanyike mapema, tuainishe hivyo vyanzo. *(Makofi)*

Nia ya kuainisha hivi vyanzo, umuhimu wake unatofautisha na jinsi Bodi ilivyo, kwamba Bodi inatumia fedha iliyopatikana au iliyowekwa tu. Niliisemea katika mazingira mengine kwamba Bodi haina tofauti sana na *ATM*, inatumia fedha zile ambazo zimewekwa, zikiisha hizo hizo basi. Lakini tunapokuwa na Mfuko na ukawa na vyanzo vya uhakika kama Waheshimiwa Wabunge tulivyoainisha, ni dhahiri kwamba tatizo hili tutakuwa tumeliondoa na wanafunzi wa Vyuo Vikuu watasoma kwa hadhi ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika mazingira haya mimi nitajumuisha mchango huu ili niende sambamba kwenye *conclusion* iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwamba watajumuisha mapendekezo ya wataalam, Waheshimiwa Wabunge pamoja na haya niliyoyatoa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nishukuru na niipongeze Serikali na Wabunge wote kwa kuwa na mtazamo chanya kwenye jambo hili la kitaifa, na twende kwa muundo huu, maana yake na hoja nyingine zitafuata ili tuweze kuisaidia nchi hii. Hiyo tutakuwa tumepiga hatua zaidi.

Niwapongeze kwa mara nyingine Waheshimiwa Wabunge waliosema jambo hili litolewe elimu. Mheshimiwa Silvestry Koka ameongelea kwenye kupanua wigo wa kodi na ameelezea na ni jambo zuri kwamba kwenye kila kinachokusanywa kuwe na asilimia ambayo inakwenda moja kwa moja kwenye kugharamia elimu.

Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwenye michango yenu mmeonesha umuhimu wa Watanzania wote kushiriki kwenye jambo hili la elimu. Kwa hiyo, kwa muundo huo na michango hii inaonesha jinsi ambavyo wananchi watakuwa wamehamasika na jambo hili.

Kwa hiyo, tunaomba Wizara mlifanyie uamuzi haraka ili tuweze kupiga hatua na kuondokana na utaratibu wa sasa ambao ukichelewa kuna wahitaji wengi watabakia bila kuwa na mkopo wakati wana sifa za kwenda Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja kama ilivyowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Rajab, mwongozo!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Ahsante Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, natumia Ibara ya 68 (7) ya Kanuni za Bunge.

SPIKA: Mheshimiwa Silinde, ukishasimama Spika atakuona.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako namna utaratibu ulivyotumika leo katika kuchangia hoja hii ili tupate ufafanuzi ni namna gani leo mmetumia utaratibu wa kuita majina na kuwapa watu nafasi za kuchangia.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba suala hili la elimu ya juu...

SPIKA: Kama ni mwongozo, unaniuliza, hunihutubii. Wewe umeishauliza, sasa kaa.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naendelea kidogo kukupa ufafanuzi.

SPIKA: Hapana! Umeshaniuliza, sasa ukae nikueleze, maana ukinihutubia...

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa sababu hili suala ni la kimuungano, tunashangaa...

SPIKA: Mheshimiwa Rajab, kaa chini, kubishana siyo utaratibu. Mwongozo kama ulivyoniuliza swali, mimi nitakujibu. Sasa ukinihutubia, huo siyo Mwongozo, hiyo ni hotuba.

TAARIFA

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Silinde!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 67(8), nilitaka tu kutoa taarifa kwa mhitimishaji wa hoja Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kuhusiana na hoja iliyopo mbele yetu, kuhusiana na kutoza riba itakayoweza kulinda thamani ya fedha.

Hoja ambayo tulikuwa tunajadili mbele yetu ilikuwa ni hoja ya marekebisho ya Waziri aliyoyaomba. Ukipitia hoja ya nne ya Mheshimiwa Waziri inaeleza wazi kwamba tozo hii itatozwa kwa wanafunzi wote wa elimu ya juu tofauti na maelezo aliyokuwa anatoa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Sasa na marekebisho tunayoyapitisha ni kwa ajili ya marekebisho ya Serikali ambayo yameelezea wazi kwamba wao watalinda thamani ya fedha na kutoza tozo kulingana na kiwango cha soko cha wakati husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa tu taarifa kwamba yale maelezo ya Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ni tofauti na haya anayotoa Mheshimiwa Waziri, *unless otherwise* watueleze hapa ni nini ambacho tunabeba? Tunabeba ya Mheshimiwa Mwigulu au maelezo ya Serikali?

SPIKA: Waheshimiwa wote mnapoteza wakati. Hoja hii inahusu Serikali ilete marekebisho kusudi tupate Mfuko wa Elimu. Hayo yote mliyokuwa mnayasema yalikuwa ni mapambio tu. *(Makofi/Kicheko)*

Hoja ndiyo hiyo. Ninapowauliza hapa sijui amesema kodi, sijui amechukua mfuko au fedha wapi, hayo yalikuwa ni mapambio ya hoja ile iliyoletwa na Serikali. Hiyo ndiyo hoja na ndiyo tunaiagiza Serikali ikaifanyie kazi.

Sasa huyu Ndugu yangu Mheshimiwa Rajab anaposema utaratibu ni upi; itakapoletwa hoja sasa yenyewe, Muswada huo, ndiyo itabidi uandikwe vizuri, utimize siku 21, uende kwa

wananchi wa kawaida wazungumze, upate *public hearing,* uende kwenye Kamati tena mje muuzungumzie hapa. Ndivyo itakavyokuwa hiyo itakayoletwa. Kwa hiyo, ombi letu sisi ni kwamba Serikali ijitahidi kwa sababu hata ile *Miscellaneous amendment* iliyokuja kipindi fulani ilisababisha *the whole bill* ikataliwe kwa sababu kulikuwa na kifungu cha Mfuko wa Mikopo. Kwa hiyo, tunasema Serikali ichukue muda. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rajab hii hoja wote wameunga mkono, sasa nyie mngeongea nini? Ni *repetition*. Mimi Kanuni inaniruhusu kama kuna kujirudiarudia, basi tunamaliza. Hakuna aliyepinga hoja hii. Lakini ninawahoji sasa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Wote wameafiki. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ichukue hatua *seriously* kwa sababu kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, kuna matatizo makubwa ya mikopo. Tujaribu kushirikishana hapa tuweze kupata kitu ambacho pengine kitatusaidia kwenda mbele. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imepita, tuombe Serikali ifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa matangazo niliyonayo, kesho tutakuwa na hoja nyingine itakayoletwa na Mheshimiwa James Mbatia inayohusu Udhaifu wa Elimu nchini. Kwa hiyo, nayo mkajiandae kwa sababu maelezo yako kwenye kile kitabu cha hoja. Wakati tunamaliza Bunge, kilitolewa kitabu cha hoja zote za Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamezileta. Naomba msome ili mweze kuchangia mantiki na siyo kubisha. Kwa sababu hiyo, tumeona saa 11.00 turudi twende kwenye Ukumbi wa Msekwa tupate *briefing* kutoka kwa *Prime Minister* kutokana na ziara yake aliyoifanya kule Mtwara.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote hata kama halitakuwa Bunge humu ndani, tutakuwa kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa, naomba mkashiriki kwa sababu jambo lililotokea Mtwara lilikuwa kubwa sana la kutikisa nchi. Waziri Mkuu amekaa kule karibu siku tatu, kwa hiyo, naomba mfike jioni saa 11.00 kule katika Ukumbi wa Msekwa ili tuweze kumsikiliza kuhusiana na yale yaliyojiri huko alikokwenda.

Kwa hiyo, naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 6.50 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 31 Januari, 2013 Saa Tatu Asubuhi)